

Ushirika Wa Huduma Ya Ufalme
Kitabu cha Mchungaji

Yaliyomo

Theologia Ya Biblia:

Utaratibu Wa Maandiko (Jinsi Tulivyoipata Biblia).

Mtazamo Wa Biblia (Pitio La Historia Ya Wokovu)

Injili Ni Nini?

Hadithi Ya Injili Ya Ufalme

Mamlaka Ya Maandiko Matakatifu

Theologia Ya Agano Jipyा (Kutoka Katika Biblia Ya ESV)

Ni Kwa Jinsi Gani Agano Jipyा Linanukuu Na Kutafasiri Agano La Kale

Utatu – Mungu katika Utatu

Jinsi Ya Kusoma, Kutafasiri Na Kuyatumia Maandiko (Kwa Wanaoanza Kuchambua Biblia)

Ubatizo Wa Maji, Historian A Maana Yake

Usalama Wa Muumini

Mila (Tamaduni) Na Injili

Baraka Na Laana Na Injili Ya Neema Katika Maandiko

Utii Wa Imani

Karama Za Roho –Ni Kwa Jinsi Gani Wawezza Kutambua, Kutumia Na Kuendeleza Karama Zako Za Roho

Theologia Ya Somo La Mateso Kutoka Katika Kitabu Cha Ayubu

Ushirika Wa Huduma Ya Ufalme

Yaliyomo

Mfumo Wa Maisha Ya Mchungaji:

Shauku Ya Kitume

Kuandaa Mahubiri Na John Stott

Kuandaa Mahubiri Kutoka Katika Neno La Mungu

Tumezaliwa Ili Tuzae

Mchungaji Kama Mfanya Wanafunzi

Kanisa, Ufalme Wa Mungu Na Upandaji Makanisa (Church Planting Pro-Forma)

Mambo Makuu Kuhusu Viongozi Wema

Kiongozi Mtumishi

Utangulizi Wa Ushirika Wa Huduma Ya Ufalme:

Maelezo Ya Kmf – KMF Ni Nini ?

Tamko La Maono Na Tamko La Ujumbe Wa KMF

Maelezo Ya Imani Ya KMF

Shabaha Ya KMF

Utaratibu wa Maandiko

Maelezo yafuatayo yamenakiliwa kutoka katika Biblia ya English Standard Version Study Bible na Crossway publishers. Maelezo haya na mengine ni msaada kwa wanaojifunza.

Utaratibu wa Agano la kale

Neno “canon” (Kiyunani ni “Kanuni au Mpangilio”) limetumika katika Biblia katika njia mbili: Kwanza, kwa kuiangalia Biblia ni kipimo cha Imani ya Kanisa na utendaji wake, na Pili, Kama lilivyo lenyewe ni *mkusanyiko sahihi na orodha* ya vitabu vilivyovuvuviwa. Neno hili lilitumika mwanzo katika kutambulisha vitabu vya Biblia sehemu za mwisho katika karne ya NNE B.K; tukirejea kweli kwamba kumekuwa na hitaji la kusawazisha mawazo ya wakristo katika jambo hili. Kabla ya hapa wakristo walikuwa wakiita “Agano la kale” na “Agano Jipy” Kama “Maandiko matakatifu” na ilikuwa hivyo badala ya kuvichanganua na walisema kuwa ni sahihi havina mapungufu.

Sababu zilizofanya vitabu vya Agano la kale visikubalike

Agano la kale lilihusiana na Biblia ya Kiyahudi ambayo Yesu na Wakristo wa kwanza walirithi kutoka kwa Wayahudi. Kipindi cha watu wa mataifa ilikuwa ni lazima kutumina Septuagint (Tafasiri ya Agano la Kale iliyokuwa imewekwa kwa ajili ya Wakristo wa kwanza waliokuwa wakizungumza kiyunani wayahudi wa Alexandra. Kwa sababu ufahamu wa wayahudi haukuwa wa kawaida katika kanisa (na hasa nje ya Siria na Palestina), tafasiri ya kwanza ya Kiratini ya Agano la kale ilitokana na Septuagint na siyo katika Asili ya kiebrania. Mahali ambapo hapakuwa na mila za kiyahudi na hata mazingira ya Kiyahudi ilikuwa ni vigumu kutofautisha vitabu vya Biblia na vitabu vingine vya kidini vilivyokuwa vikisomwa na kuzunguka katika Lugha ya kiyunani na Kilatini. Hii ilileta mchanganyiko mkubwa katika kuyakusanya maandiko na ndipo neno hili “Canon” likawepo ili kuleta ulinganifu.

Je Biblia ya Kiyahudi ilikuwa na vitabu vilevile ambavyo Biblia ya Leo inavyo?

Mchanganuo wa juu unasema kwamba Biblia ya kiyahudi ambayo kanisa la kwanza lilirithi katika karne ya kwanza ilikuwa na vitabu tulivyo navyo leo. Vitabu vitano vya sheria vilikuwa viko katika mpangilio. Yalifuata matukio kwa mpangilio kulingana na sheria ya Musa na Historia kuanzia uumbaji hadi kufa kwa Musa. Zaidi ya hapo, Manabii na Maandiko kama yanepangwa katika asili yake ya Talmud, pia navyo havikuwa katika mpangilio sawa. Manabii wanaanza, vitabu vya Historia—Yoshua, Waaamuzi, Samweli, na Wafalme—ikituleta katika historia nyingine, ya kuingia katika nchi ya ahadi hadi kwenda uhamishoni. Vitabu vya mashairi—Yeremiah, Ezekiel, Isaya, na vitabu vya manabii kumi kumi na mbili—katika mpangilio wa kushuka chini. Maandiko ya Historia yanaanza na vitabu sita vya Hekima—Zaburi, Ayubu, Methali, Muhubiri, Wimbo ulio bora, na maombolezo—vimepangwa katika mfumo wa kushuka chini kufuatana na ukubwa, na kuishia vitabu vya masimulizi—Danieli, Estha, Ezra—Nehemia, na nyakati—kukamilisha kipindi cha tatu cha historia, kipindi cha uhamishoni na kurudi. (Vitabu vinavobaki vya maandiko, Ruthu, kiliwekwa kabla ya Zaburi, na kinaishia na ukoo wa mwana Zaburi Daudi.) Vitabu vinne vya masimulizi vya Hagiographa viko katika sehemu ya pili ili kwamba Nyakati ikamilishe historia nzima ya Biblia, Tangu Adamu

hadi kurudi kwa waliokuwa uhamishoni, na kwasababu hii pia Ezra–Nehemiah iliwekwa kabla ya Nyakati na siyo baada yake. Kitu cha pekee ni kwamba Wimbo ulio bora ni kifupi kuliko maombolezo si sana lakini kimewekwa mwanzoni ili kuvifanya hivi vitatu viungane pamoja na Wimbo ulio bora.

Yesu na waandishi wa Agano jipya walinukuu maneno ya Agano la kale mara 300; hii ni kwa sababu ya mifano michache ambayo haikueleweka vizuri na ndiyo maana walinukuu Agano la kale ili ieeweke kwa kutumia maneno yaleyale. Walinukuu ili kuwe na mamlaka ya Mungu, maneno kama vile “Imeandikwa” “maandiko yanasema” na “Mungu anasema” na hakuna maandiko mengine yaliyonukuliwa kwa mfumo huu. Hata hivyo waandishi wa Agano jipya walinukuu waandishi wengine, hata waandishi wa kiyunani wasioamini lakini hawakunukuu katika maandiko mengine tofauti na uandishi wa neno la Mungu (Tazama [Mdo 17:28](#); [Tito 1:12–13](#); [Yuda 8–10, 14–16](#)), walipokuwa wakiandika mpangilio wa neno la Mungu katika Agano la kale. Masomo ya Historia yanaonesha kwamba Agano la kale la kiyahudi linampangilio wa kanuni sahihi alizozisema Yesu na mitume kwa wayahudishi wa karne ya kwanza. Hakuna kitabu kilichosahaaulika kitakachoongezwa au kilichoongezwa.

Mpangilio (Canon) wa Agano Jipya

Msingi wa Agano jipya uko katika neema ya kumfunua Mungu mwenyewe ambaye neno lake limebeba mamlaka ya Kiungu. Likiwa ni uvuvio mpya wa Neno la Kiungu linalofuata na kuleta ukombozi katika historia ya watu wa Mungu (Agano la Adamu na Eva, Agano la Ibrahimu, kukombolewa kutoka Misri, kuwekwa kwa ufalme, uhamisho na urejesho), alipokuja masihi aliyeahidiwa uvuvio mpya ultokea (Tazama [2 Tim. 1:8–11](#); [Titos 1:1–3](#)).

Idhini ya Agano la Kale

Ukweli wa Agano jipya kuwiana na Agano la kale, ulidhihirisa na hata uliidhinishwa katika Agano la kale lenyewe katika mpango wa ahadi ya ukombozi, kwa njia ya Masihi katika uaminifu wa Agano la lake ([Yer. 31:31–33](#); na [Waebr. 8:7–13; 10:16–18](#)). Yesu aliwafundisha wanafunzi wake baada ya kufufuka kwake kwamba “Sheria ya Musa na Manabii na Zaburi” hazikutabiri mateso ya masihi na kufufuka kwake tu bali hata toba na msamaha wa dhambi utatangazwa katika Jina lake kwa mataifa yote kuanzia Yerusalem (“[Luka 24:44–48](#)”). Sura za manabii kama vile [Isaya 2:2–3; 49:6](#); na [Zaburi 2:8](#) zinazungumzia nyakati ambapo Nuru ya neema ya Mungu katika ukombozi utatangazwa katika mataifa yote. Katika asili inaleta kwamba tangazo hili linahitimisha ukusanywaji mpya wa maandiko yaliyoandikwa yaliyokamilisha vitabu vya Agano la kale—Tangu ukombozi wa Mungu katika Agano la kale (imetajwa hapo juu) na tangu nyaraka zilizoandikwa za huduma ya Yesu na mitume (na wasaidizi wao) katika kutimiza utume wao.

Utume wa Yesu

Mungu, aliyesema katika namna mbalimbali hapo kale sasa anasema nasi kwa njia ya mwana wake (Tazama [Waebr. 1:1–2, 4](#)). Inaleta hii neema ya ukombozi kwa Waisrael na Mataifa; na hii ilikuwa ni sehemu ya huduma ya Yesu ([Isaya. 49:6](#); [Mdo 26:23](#)), Neno akafanyika Mwili

([Yohana 1:14](#)). Aliweka ujumbe wake kwa mitume ambao aliwachagua kuwa wawakilishi wake ([Math. 10:40](#), “Yeyote atakayewapokea amenipokea mimi”). Kazi yao ilikuwa ni kuwaletea ... kumbukumbu,” kwa njia ya kazi ya Roho mtakatifu Neno lake na kazi yake ([Yohana 14:26; 16:13–14](#)) na kuwa mashahidi wa Yesu “katika Yerusalem, Yudea yote na Samalia na hata mwisho wan nchi” ([Mdo 1:8](#); cf. [Mat. 28:19–20](#); [Luka 24:48](#); [Yohana 17:14, 20](#)). Nyakati hizo, mahubiri ya mitume yakaandikwa katika mfumo wa vitabu na kufanya Agano jipyga na sasa linatenda kazi kama “Amri ya Bwana na Mwokozi kupitia mitume” ([2 Pet. 3:2](#)).

Paulo na mitume wengine waliandika kama vile walivyohubiri kwa kuzingatia Agizo la Yesu. Tangu mwanzo mamlaka yote ya mitume (na manabii) kupeleka Neno la Mungu kulitambuliwa na wengi ([Mdo 10:22](#); [Waefeso. 2:20](#); [1 Wathesalonike. 2:13](#); [Yuda 17–18](#)). Utambuzi huu unakumbkwa na wale waandishi wa kwanza. Kwa mfano, Clement wa Rumi alisema kwamba “Mitume walipata injili kwa ajili yetu kutoka kwa Yesu kristo; Yesu Kristo alitumwa kutoka kwa Mungu Hivyo Kristo anatoka kwa Mungu na mitume wanatoka Kwa Kristo na hivyo wote hawa wawili wanatokana na mapenzi ya Mungu kwa makusudi mema” (*1 Clement* 42.1–2 iliandikwa c. B.K. 95). Katika mawazo juu ya baadhi ya vitabu vinavyofanya mpangilio wa maandiko, kanisa halikuvibagua” au “kuchagua” kwamba kipi linakipenda zaidi—iwe katekisimu, mashindano, ritulijia au marekebisho bali kanisa liliona kana kwamba limewezeshwa kupokea na kutambua kile Mungu amekiweka kaika vitabu hivyo vilivyotoka kwa mitume na washirika wao (Mfano, Irenaeus, *Against Heresies* 3.preface; 3.1.1–2). Na nadiyo maana majadiliano juu ya kile kinachoitwa mpangilio wa maandiko kinaweza kutupotosha. Vitu kama “Utume,” “migawanyiko,” “Orthodoxy,” “matumizi ya ritulijia,” na “makanisa” si kigezo ambacho kanisa bila kujua linaweza kushutumiwa. Mambo haya matatu ya kwanza, kanisa linayatambua kwa njia ya sauti ya mwokozi wake na kwa hiyo kanisa linaweza kutii (“Kondoo wangu waisikia sauti yangu ... na wananiyuata,” [Yohana 10:27](#)).

Injili kama ilivyoandikwa na Mathayo, Marko, Luka na Yohana (Injili za kwanza kabisa zinazofahamika) zilikubalika ulimwenguni kipindi kumeibuka mabishano ndani ya kanisa. Ikiwa hii kazi , Injili ya Yohana iliandikwa kipindi cha mwisho wa karne ya kwanza (kama wasomi wengi wanavyodai), miaka ya 100 B.k. Inaonesha kwamba maneno yake yamekuwepo tangu katika maandishi ya Ignato wa Antiokia ambaye pia alimfahamu Mathayo na yumkini Luka. Na kwa wakati ule ule, Papias wa Hierapolis katika Asia ndogo alipokea asili juu ya asili ya kitabu cha Injili ya Mathayo na Marko na hata Luka na Yohana . Katikati mwa karne ya pili, Justin Martyr katika Rumi alilipoti kuwa Injili (na hasa hizi nne)—ambazo alizita “kumbukumbu za mitume”—zilisomwa na na kuwekwa wazi kwenye ibada za Wakristo wanapoabudu.

Katika [2 Petro 3:16](#), mkusanyiko wa vitabu vya Paulo mtume ulikuwa tayari umesha julikana na kutambuliwa kama maandiko na kuruhusiwa kuwekwa katika mpangilio wa maandiko. Zaidi ya hapo, mkusanyiko (wa vitabu visivyojulikana waandishi) nyaraka za Paulo zilizokuwa zikijulikana kwa Clement wa Rumi na kwa wapokeaji wa nyaraka zake huko Korintho kabla ya kuisha kwa karne ya Kwanza na baadaye kwa Ignatius wa Antiokia na Polycarp wa Smyrna na wasomaji wao mapema kabisa mwa karne ya pili. Nyaraka za kichungaji (1–2 Timotheo na Tito), zilikataliwa kuwa si za Paulo na watu wa sasa na zikarejeshwa tena katika nyakati za Polycarp.

Mwishoni mwa karne ya pili mkusanyiko wa vitabu 21 kati ya 27 vya Agano jipya ulikuwa umetambuliwa: Injili nne, Matendo, Nyaraka 13 za Paulo, 1 Petro, 1 Yohana, na Ufunuo. Kipindi hiki Waebrania (ilikubalika upansde wa mashariki na Irenus na Tertullian upande wa magharibi lakini ilihojija upande wa Rumi juu ya nani aliandika), Yakobo, 2 Petro, 2 na 3 Yohana, na Yuda ziliangaliwa katika kanisa na viongozi. Hili swala baadae lilileta mashaka kwa babu zetu wa baadae (e.g., Eusebius, *Ecclesiastical History* 2.23.25). Wakati fulani katika karne ya tatu, viambatanisho (Watangulizi wa vitabu vya sasa vilivyopingana na vile vya kwenye magome) zina vitabu vyote saba “nyaraka za jumla” zilitolewa na hivi 11 vyote vilijulikaa kwa wote.”

Nyakati za 240s B.K. Origen (akiishi Kaisaria Palestina) alishukuru vitabu vyote 27 vya Agano jipya lakini akaarifu kwamba Yakobo, 2 Petro, 2 na 3 Yohana na Yuda zilileta mijadala. Hali ilikuwa ile ile Kwa Eusebius, aliandika miaka 60 baadae, ambaye pia alitoa mashaka yaleyale waliyokuwa nayo juu ya kitabu cha waebrania na ufunuo. Bado haya mawazo yake mawili ya kutiliwa mashaka na kutotiliwa mashaka yalijulikana kwa wengi na yalibaki katika vitabu hivi 27 na si zaidi ya hivyo. Alivipa majina hivi vitabu vitano (*Mtendo ya mitume, Mchungaji wa Herma, Apocalypse ya Petro, Barua ya Barnaba*, na *The Didache*) which were known to many churches but which, he believed, had to be judged as spurious.

Mwaka wa 367 B. K. the Alexandrian askofu Athanasius, katika barua yake ya mwaka wa pasaka alitoa orodha ya vitabu vya Agano jipya ndani yake hapakuwa na salio la vitabu vingine, vitabu vyote 27 vilifaa na vingine hakuvihesabu kama ni vitabu vilivyo na uvuvio hivyo si maandiko matakatifu. Baada ya karne nyingine kama nne kuna orodha nyingine ilijitokeza lakini vilikuwa nje na hivi vingine muhimu (Injili nne, Matendo, Nyaraka 13, 1 petro, na 1 Yohana). Sinodi tatu za kiafrica—Hippo Regius B.K. 393 na Carthage miaka ya 397 na 419—na askofu wa kiafrica mwenye ushawishi mkubwa Augustine alisibitisha kuwa vitabu hivi 27-ndiyo Canon. Vilikuwa katika kilatini, the Vulgate, na ndiyo ikawa Biblia ya kawaida katika kanisa la magharibi. Katika makanisa ya mashariki kuthibitishwa kwa kitabu cha Ufunuo. Makanisa ya Ashuru hayakukikubali kitabu cha ufunuo, 2 Petro, 2 na 3 Yohana, au Yuda hadi karne ya tano (Siria ya magharibi) au sita (Siria ya mashariki).

Neno la kitume lilileta matokeo kwa kanisa ([Warumi 1:15–17; 10:14–15; Yakobo 1:18; 1 Pet. 1:23–25](#)), na neno kama hili lilioandikwa lilibaki moja kwa moja, na kama Agano la Mungu. Inaweza kusemekana kwamba ni vitabu 27 vya agano jipya vilijidhihirisha vyenyewe vikishabiana na vile vya asili vya Agano la kale, vya msingi na shuhuda za kitume. Vimejidhihirisha vyenyewe kuwa ni neno la Mungu kwa ajili ya kanisa la ulimwengu katika vizazi vyote. Haya ni malisho ambayo kondoo wa Yesu katika huduma nyingi watakuja kuisikia sauti ya mchungaji wao na kumfuata.

Apocrypha

Nyongeza kubwa za Biblia ya kiingereza—Kutoka katika Biblia kubwa ya Tyndale na Coverdale (1539) na kuendelea—zimekuwa na sehem ya ziada kati ya Maagano yote mawili ya Agano la kale na Agano jipya na nyongeza hiyo inaitwa “Apocrypha,” iliyo na vitabu vya ziada vyenye sehemu ya vijitabu tena. Biblia ya Kilatini iliyotafasiliwa na Jerome (Alianza a.d. 382, akamaliza 405) ameviweka vyote katika agano la kale peke yake—vingine vinajitegemea vingine vimeunganishwa na vitabu vya Biblia vya Esther, Yeremia, na Danieli. Katika tafasiri ya

Biblia ya kiromani kama vile toleo la Douay Version na Biblia ya Yerusalem, vitabi hivi bado vimo. Kwa Waprotestanti Apocrypha yaweza kuwa imetanganishwa au imeunganiswa pamoja.

Yerome alivipa jina “apocrypha” (Kiyunani. *apokrypha*, “yaani vilivyokuwa vimefichwa”). Kuhusiana na mafundisho yake—Kwa uelewa wa Agano la kale kwamba Yesu ndiye anayezungumziwa , watanzi wa Agano jipywa na wayahudi wa karne ya kwanza kwa hiyo Wakarimani wa karne ya kumi na sita hawakufikiri kuwa hivyo navyo vilikuwa ni sehemu ya Agano la kale bali walivitenga na kuviweka pamoja na wakavipa jina la Yerome, “Apocrypha.”

Njia ambayo waandishi wa kikristo, walikitumia kitabu cha Apocrypha kinathibitisha mchangano ulio hapo juu. Agano jipywa linaonekana kukubaliana na ufahamu na wazo moja au jingine la maandishi ya Apocrypha, lakini hayana mamlaka kama vile vitabu vingine vya canon ya Agano la kale vilivyo. Agano jipywa likinukuu zaidi ya mara 300 mambo ya Agano la kale lakini hakuna linachonukuu kutoka katika kitabu cha Apocrypha ([Yuda 14–16](#) hainukuu kutoka katika kitabu cha Apocrypha bali kutoka katika maandishi mengine ya kiyahudi, *1 Enoch*; katika karne ya pili, Justin Martyr na Theophilo wa Antioki, ambaye mara zote alinuku kutoka Agano la kale kamwe hakuwahi kunukuu kutoka katika kitabu cha Apocrypha. Mwishoni mwa hekima ya karne ya pili, *Tobit*, na *Sira pia nayyo vilitumika kama sehemu za maandiko lakini siyo maandiko ya Apocrypha*. Ukubalikaji matukio yake ulikuwa ni wa taratibu sana. Na ndivyo ilivyokatika Agano la kale pia kwamba ni mambo machache sana yanayokubaliana na kitabu hiki cha Apocrypha; na hata vingine vya zamani vya Melito (B.K. 170).

Mwishoni mwa karne ya nne Yerome aliona kuna umuhimu wa kutenganisha kabisa kitabu hiki kilichovuviwa cha Agano la kale na kitabu cha Apocrypha lakini waandishi wachache waliendelea kukiingiza katika kipindi cha zama za kati mpaka Waprotestanti walipoinuka na kuweka mkazo juu ya swala hili ili Biblia iwe kama ilivyokusudiwa kwa ajili ya mafundisho yao matakatifu. Kwenye baraza la Trent (1545–1563), hata hivyo kanisa la Rumi lilijaribu kupinga mabadiliko ya kukitoa kitabu hiki na kukiweka kitabu hiki cha Apocrypha (kwa mitazamo ya kitabu cha *1 na 2 Esdras* na maombi ya Manase) kwa kusema kuwa vimevuvuviwa kama vile Agano la kale ilivyovuviwa. Haya yalikuwa ni madhara ya (1) kuinua tamaduni za Warumi, (2) mtazamo wake kwamba kanisa ndilo lililotengeneza maandiko na (3) kukubali kwake mawazo ya upotoshaji (hasa. Mafundisho ya pagatori, malezi, haki ya matendo kuwa ni sehemu ya kuhesabiwa haki) yaliyotokana na sura fulani kwenye kitabu cha Apocrypha. Mafundiso haya yalileta nguvu sana kwenye kanisa la Roma likapelekea Martin Luther na viongozi wengine kugoma na kuleta uporotestant mwaka 1517.

Mtazamo wa Biblia: Pitio la Historia ya Wokovu

Biblia inalinganaje kwa ujumla? Matukio yaliyotokea katika Biblia yalitoke miaka maelefu iliyopita katika mazingira tofauti tofauti. Ni nini kinachoyaunganisha?

Kitu kinachoiunganisha Biblia ni ule utunzi wake wa Kiungu. *Kila kitabu katika Biblia ni Neno la Mungu.* Matukio yaliyoandikwa katika Biblia yapo kwa sababu Mungu alitaka yaandikwe na yakaandikwa na watu wake aliwaelekeza.: “Kwa kuwa yote yaliyotangulia kuandikwa yaliandikwa ili kutufundisha sisi ili kwa saburi na faraja ya maandiko tupate kuwa na matumaini” ([Rum. 15:4](#)).

Mpango wa Mungu kwa ajili ya Historia

Biblia pia inaweka wazi kwamba Mungu ana mpango mmoja katika historia yote. Kusudi lake muhimu “Mpango wa ukamilifu wa wakati” ni kuunganisha vitu vyote katika yeye (Kristo” vitu vyta mbinguni na duniani” ([Ef. 1:10](#)), “kwa ajili ya sifa za utukufu wake” ([Ef. 1:12](#)). Mungu amekuwa na mpango huu tangu mwanzo: “kumbukeni mambo ya zamani za kale maana mimi ni Mungu wala hapana Mungu mwingine Mini ni Mungu wala hapana aliye kama mimi Nitangazae mwisho tangu mwanzo na tangu zamani za kale mambo yasiyotendeka bado nikisema shauri langu litasimama nami nitatenda mapenzi yangu yote”” ([Isaya. 46:9–10](#)). “Hata ulipotimia utimilifu wa wakati Mungu alimtuma mwanawe aliyezaliwa na mwanamke amezaliwa chini ya sheria kusudi awakomboe hao waliokuwa chini ya sheria ili sisi tupate kupokea hali ya kuwa wana” ([Gal. 4:4–5](#)).

Kazi ya kristo hapa duniani na hasa kusulubiwa kwake na kufufuka kwake ni kilele cha Historia ni sehemu nzuri ya mabadiliko ambapo Mungu hakika alikamilisha wokovu kitu ambacho historia imekuwa ikikisema katika Agano lote la kale. Nyakati za sasa zinaangalia kazi ya Yesu iliyokamilika lakini pia inatarajia matunda ya kazi yake Yesu atakaporudi mara ya pili ambapo kutakuwa na udhihirisho wa “mbingu mpya na nchi mpya ambapo haki hukaa” ([2 Pet. 3:13](#); Tazama [Ufunuo. 21:1–22:5](#)).

Moja wa mpango wa Mungu unamfanya afae aingize Ahadi na matarajio mapema kabisa, na hata utimilifu wa haya kuja baadae, wakati mwingine ahadi huwa katika mpangilio kama vile Mungu alipomwahidi Masihi mwokozi mkuu ambao Israeli walimtegemea ([Isa. 9:6–7](#)). Wakati mwingine ahadi huwa katika mfumo wa alama kama vile Mungu alivyoamuru wanyama watolewe kwa ajili ya msamaha wa dhambi ([Walawi 4](#)). Wanyama hawakuweza kusafisha dhambi moja kwa moja ([Waeb. 10:1–18](#)). Zilimwakilisha Yesu ambaye ndiye mwisho na dhabihu kamili kwa ajili ya dhmabi.

Kristo katika Agano la Kale

Kwa kuwa mpango wa Mungu unamlenga Kristo na utukufu wake ([Ef. 1:10](#)), ni kawaida kwamba ahadi za Mungu na alama zote katika agano la kale zote zinamlenga yeye. “Maana ahadi zote za Mungu zilizomo katika yeye [Kristo]” ([2 Kor. 1:20](#)). Baada ya Yesu kuwatokea

wanafunzi wake baada ya kufufuka mafundisho yake yalikuwa yanahu su kuwaonesha jinsi Agano la kale lilivyokuwa linamzungumzia: “Akawambia enyi msiofahamu wenyewe miyo mizito ya kuamini yote waliyoyasema manabii je haikumpasa Kristo kuyapata mateso yote haya na kuingia katika utukufu wake akaanza kutoka Musa hadi manabii wote akawaeleza katika maandiko yote mambo yaliyomuhusu yeye mwenyewe ” ([Luka 24:25–27](#)). waweza kuangalia [Luka 24:44–48](#): “Kisha akawaambia hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali nanyi yakwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika torati ya Musa na katika manabii na Zaburi ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na maandiko anawaambia ndiyo ilivyoandikwa kwamba kristo atateswa na kufufuka siku ya Tatu na kwamba mataifa yote watahubiri kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi kuanza tangu Yerusalemu nanyindiyo mashahidi wa mambo haya.””

Biblia inaposema *Ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na maandiko*” ([Luke 24:45](#)), haimaanishi sehemu chache tu za Biblia katika Agano la kale bali maandiko yote ya Agano la kale, Akieleza migawanyiko yote mitatu ya Agano la kale ambayo wayahudi walikuwa wanaitambua. “Sheria ya Musa hii ni mwanzo hadi Kumbukumbu la Torati, “Manabii” inaingiza “Manabii wa kwanza” (Vitabu vya historia Joshua, Waaamuzi, 1 &2 Samweli na 1 & 2 Wafalme) na “Manabii waliokuja” (Isaya, Yeremia, Ezekiel, na Manabii wadogo 12, , Hosea–Malaki). “Zaburi” inawakilisha kundi la tatu la wayahudi liliitwa “Maandiko” (Kitabu cha Danieli kiliingizwa katika kundi hili.) katika kiini cha kuvielewa vitabu vya Agano la kale ni kweli kwamba yote yalikuwa yanataja mateso ya Kristo, kufufuka kwake, na hata kuenea kwa Injili “Mataifa yote” ([Luka 24:47](#)). Agano la kale kwa ujumla ahadi zake zote na taswira yake ya wokovu, zinaelekeza katika kukamilisha wokovu tendo lililofanyika mara moja kwa ajili ya wote, kifo na kufufuka kwa Yesu Kristo.

Ahadi za Mungu

Ni katika namna ipi Agano la kale linamtazama Kristo? Kwanza linataja moja kwa moja *Ahadi ya wokovu na ahadi zinazohusiana kujitoa kwa Mungu kwa wat wake*. Mungu alitoa ahadi fulani katika Agano la kale kuhusiana na kuja kwa Kristo kama Masihi Mwokozi katika ukoo wa Daudi. Japo Nabii Mika Mungu aliahidi kwamba Masihi atazaliwa Bethelehemu mji wa Daudi ([Mika. 5:2](#)), Unabii ukatimia katika Agano jipya ([Mat. 2:1–12](#)). Lakini pia Mungu ametoa ahadi za jumla kuhusiana na siku kuu ya wokovu bila kueleza ni kwajinsi gani atafanya (Mfano, [Isa. 25:6–9; 60:1–7](#)). Wakati mwengine aliahidi kwamba atakuwa Mungu wao (Tazama [Mwanzo. 17:7](#)).

Kiitikio cha kawaida ni kwamba, “Nitakuwa Mungu wao nao watakuwa ni watu wangu” (cf. [Yer. 31:33](#); [Hos. 2:23](#); [Zek. 8:8; 13:9](#); [Waeb. 8:10](#)). Mabadiliko katika makusudi haya mapana yanaweza kulalia kwa watu zaidi na jinsi watakavyokuwa wakati mwengine, yanamwelekea Mungu zaidi na kile atakachokifanya. Mungu aliahidi kuwa “Mungu wao”na hii ni kujitoa kwake dhahiri kabisa kuwa pamoja na watu wake, kuwajali, kuwaonya, kuwalinda, kuwapatia mahitaji yao, na kuwa na mahusiano nao. Ikiwa kujitoa huko kunaendelea matokeo yake ni wokovu ambao Mungu anautenda kupitia Kristo.

Kanuni zimesimama katika ahadi zote katika Agano la kale. “Maana ahadi za Mungu zilizomo katika yeye ni Ndiyo [Kristo]” ([2 Kor. 1:20](#)). Wakati mwengine Mungu hutoa Baraka za haraka

na za muda. Hizi Baraka ni utangulizi wa kuyajua mema yake, Baraka za milele huja kwa njia ya Kristo: “Atukuzwe Mungu Baba wa Bwana wetu aliyeubariki Baraka za Rohoni katika ulimwengu wa Roho” ([Ef. 1:3](#)).

Maonyo na Laana

Mahusiano ya Mungu kwa watu wake hayahusiani na baraka tu bali hata maonyo, vitisho na laana. Haya ni muhim kwa sababu ya haki ya Mungu na anavyoichkia dhambi. Yanaonesha na kumumulika Kristo kwa namna mbili tofauti. Kwanza, *Kristo ni mwanakondoo wa Mungu, abebae dhambi* ([Yohana 1:29](#); [1 Pet. 2:24](#)). Hakuwa na dhambi, bali alifanyika kuwa dhambi kwa ajili yetu na kuibeba laana ya Mungu msalabani ([2 Kor. 5:21](#); [Gal. 3:13](#)). Kila mfano wa ghadhabu ya Mungu dhidi ya dhambi na adhabu yake juu ya dhambi inalenga ile ghadhambu aliyoimwaga juu ya Kristo pale msalabani.

Pili, *Kristo kuja kwake kwa vita ya mara ya pili dhidi ya dhambi na Kuharibu*. Kuja kwa mara ya pili na uangamifu ni nyakati ambapo hukumu ya mwisho dhidi ya dhambi itaachiliwa. Hukumu za awali dhidi ya dhambi zilikuwa zinaashiria hukumu ya mwisho. Kristo kipindi cha maisha yake hapa duniani alionesha hukumu hii pale alipokuwa anakemea mapepo na pale alipozikana dhambi za viongozi wa dini.

Maagano

Ahadi za Mungu katika agano la kale haziko tu katika Mungu kujitoa kwa ajili ya watu wake bali pia katoa melekezo kwa watu wake jinsi ambavyo wanaweza kujitoa kwa Mungu. Nuhu, Ibrahim, na wengine amba Mungu alikutana nao hakuwaita wamwitikie tu bali hata wawe na maisha yenye kuzaa matunda katika ushirika wao na Mungu. Mahusiano ya Mungu na watu wake yamejumuishwa katika maagano mbalimbali ambayo Mungu alifanya na watu wake. Agano kati ya watu wawili ni makubaliano ya uaminifu kati yao (Kama vile Yakobo na Labani [Mwanzo. 31:44](#)). Mungu anapofanya Agano na Mtu, Mungu ni mwenye mamlaka kwa hiyo huweka maelekezo pande zote mbili. “Nitakuwa Mungu wao” Ni jukumu la Mungu upande wake, lakini “watakuwa watu wangu” ni jukumu la mwanadamu. Lakini kunamabadiliko katika maelezo.

Kwa mfano Mungu alipomwita Ibrahimu Mara ya kwanza alimwambia, “Toka wewe katika nchi yako na jamaa zako na nyumba ya baba yako uende katika nchi nitakayokuonesha” ([Mwanzo. 12:1](#)). Hii ni amri iliyotolewa kwa Ibrahimu peke yake na Ibrahimu ndiye mtekelezaji, hivyo huo ni upande wa mwanadamu. Mungu naye anaonesha sehemu yake: “Nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki na kulikuza jina lako, nawe uwe Baraka” ([Gen. 12:2](#)). Kujitoa kwa Mungu huwa ni ahadi, Baraka na laana. Ahadi na Baraka zote zinamwakilisha Kristo ambaye ndiye utimilifu wa Ahadi na chanzo na hatima ya Baraka. Laana zinamwakilisha Kristo katika kubeba laana na katika mtazamo wa hukumu na laana dhidi ya dhambi na hasa katika kuja kwake mara ya pili.

Utekelezaji wa Agano upande wa Mwanadamu linahusiana na Kristo. Kristo ni mwanadamu na ni Mungu. Kama Mwanadamu husimama na watu wake upande wao. Alitimiza upande wa

Mungu kwa kutii ([Waeb. 5:8](#)). Alipokea thawabu ya utii kipindi cha kufufuka na kupaa kwake (Tazama [Wafilipi. 2:9–10](#)). Agano la kale katika upande wa mwanadamu unamwakilisha Yesu.

Kwa kushughulika na ghadhabu ya Mungu dhidi ya dhambi Kristo alibadili mazingira ya hasira ya Mungu na kuleta amani. Aliwapatanisha waumini na Mungu ([2 Kor. 5:18–21](#); [Rum. 5:6–11](#)). Aileta urafiki na Mungu na kutufanya tuwe wana wa Mungu ([Rum. 8:14–17](#)). Urafiki hu ndiyo ulielezwa na Agano la kale. Katika Isaya Mungu alisema kwamba mtumishi wake Masihi atakuwa ni Agano la watu (Tazama [Isa. 42:6; 49:8](#)).

Uzao

Ni vizuri sana kulenga jambo moja katika Agano la kale, majina ahadi inayohusu Uzao. Katika kufanya Agano na Ibrahimu Mungu alimwita na kumwambia “Nenda mbele yangu na usilaumiwe” ([Mwanzo. 17:1](#)). Hilo ni jukumu la mwanadamu katika agano hili. Katika sehemu ya Mungu, Mungu aliahidi kwamba atamfanya Ibrahimu “Baba wa mataifa mengi” ([Mwanzo. 17:4](#)), na akamwita Ibrahimu ([Mwanzo. 17:5](#)). Agano la Ibrahimu linaenda zaidi hadi kwenye mafanikio yake: “Agano langu nitalifanya Imara kati ya Mimi na wewe na uzao wako baada yako na vizazi vyao kuwa Agano la milele kwamba nitakuwa Mungu kwako na kwa uzao wako baada yako. Nami nitakupa wewe na uzao wako nchi hii inayoikaa ugeni nchi yote ya kanaani, kuwa milki ya milele nami nitakuwa Mungu wao” ([Gen. 17:7–8](#)).

Ahadi iliyofaywa kwa Ibrahimu ni muhimu sana katika Agano la kale kwa sababu ni msingi wa taifa la Israeli. Historia ya Ibrahimu inaonyesh kwamba Ibrahimu alikuwa na mtoto Isaka kama utimilifu wa Ahadi kwa sara. Isaka ilikuwa ni matokeo ya utimilifu wa ahadi ya Mungu ya uzao utakao irithi nchi. Isaka naye alipata mtoto Yakobo na Yakobo alikuwa ni baba wa watoto 12 na baadaye walikuja kuwa ni mataifa kumi na mbili ya Israeli. Taifa la Isareli ilikuwa ni hatua nyingine ya uzao ambao Mungu aliuhidi.

Lakini hili linahusiana viyi na Kristo? Kristo ni uzao wa Daudi na Ibrahimu kama vile vizazi vinavyoonekana katika mathayo ([Mat. 1:1](#)). Kristo ni uzao wa Ibrahimu na ni uzao kwa njia ya kipekee sana: “Basi ahadi zilinenwa kwa Ibrahimu na kwa mzao wake hasemi kwa wazao kana kwamba ni wengi bali kana kwamba ni mmoja kwa mzao wako yaani Kristo” ([Gal. 3:16](#); tazama maelezo katika [Mwanzo. 22:15–18](#)).

Abrahamu aliambiwa “kwenda mbele bila lawama” ([Gen. 17:1](#)). Abrahamu alikuwa ni mtu wa Imani aliye mtumainia Mungu ([Gal. 3:9](#); [Waembrania. 11:8–12, 17–19](#)). Lakini Ibrahimu alikuwa na mapungufu yake na dhambi zake. Atakaye kwenda mbele za Mungu kwa njia iliyo sahihi ? Si Ibrahimu. Wala hakuna mwingine katika dunia hii bali ni Kristo mwenyewe ([Waembrania. 4:15](#)). Wale wengine wanaowakilisha uzao wa Ibrahimu na hawakuweza kuwa wasiolalamika. Kwa hiyo Agano la Ibrahimu halivunjiki katika Kristo. Unaweza kufuatilia vizazi hivyo tangu Isaka, Yakobo na baadaye watoto wa Yakobo. Katika uzao huu Yuda ni kiongozi wao ambaye atakuwa na ufalme ([Mwanzo. 49:10](#)). Daudi ni uzao wa Abrahamu na Yuda ; Sulemani ni uzao wa Daudi; na baadae anakuja Rohoboamu na wengine waliokuwa ni ukoo wa daudi na solemani ([Math. 1:1–16](#)).

Kristo si uzao wa wote kisheria lakini pia ni mkuu kuliko wote maana hana hatia wala lawama. Kwa njia ya Kristo waumini wote wameunganishwa naye na kuwa wana wa Ibrahimu” ([Gal. 3:29](#)). Waumini, Wayahudi na watu wa mataifa wako sawa wote wamefanywa kuwa ni warithi wa Ahadi” ([Gal. 3:28–29](#)).

Kristo kama Adamu wa Mwisho

Kristo si tu uzao wa Ibrahimu, lakini—tukirejea katika ahadi za Mungu—ni uzao wa Mwanamke: “Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke na kati ya uzao wako na uzao wake huo utakuponda kichwa nawe tamponda kisigino” ([Mwanzo. 3:15](#)). Kumshinda nyoka hivyo ni kumshinda shetani, ni kupitia uzao wa mwanamke. Naweba kuungalia uzao huu kuanzia kwa Hawa hadi Sethi na uzao wake, Nuhu hadi Ibrahimu ambako ahadi za Mungu zinaonekana dhahiri kupitia uzao wa Ibrahimu (Tazama [Luka 3:23–38](#), inayouleta uzao wa Yesu na kuurudisha hadi kwa Adamu. Hivyo Yesu si uzao wa Ibrahimu tu bali Adamu wa Mwisho ([1 Kor. 15:45–49](#)). Kama Adamu anawawakilisha wote walio wake na kurejea katika anguko la Adamu

Vivuli, Taswira, na “Aina”

Agano jipya linazungumzia juu ya Kristo na wokovu aliouleta. Hiyo ni dhahiri. Kitu kisichokuwa ni sawa ni kwamba, historia ni ileile tangu Agano la kale isipokuwa yameoneshwa kama utangulizi. Inatupa “Vin vuli” na “Aina” ya mambo yaliyopaswa kuja (Tazama [1 Kor. 10:6, 11](#); [Waeb. 8:5](#)).

Kwa mfano, [1 Kor 10:6](#) inaonesha kwamba matukio waliyokabiliana nayo Waisraeli jangwani ilikuwa ni “mifano yetu.” na [1 Kor 10:11](#) inasema, “Basi mambo hayo yalikuwa ni mifano kwetu kusudi sisi tusiwe watu wa kutamani mabaya kama vile wale nao walivyotamani , yaliandikwa ili kutuonya sisi tuliofikiliwa na miisho ya zamani.” Katika [1 Kor 10:6 and 11](#), Neno la Kigiriki “Mfano” ni *typos*, ambalo kwa kiingeleza linamaanisha “Aina” (cf. [Rum. 5:14](#)).

“Aina,” katika Lugha ya theologia ni, *mfano maalumu, alama, au taswira ambayo Mungu aliifanya kabla ya ulimwengu na kuiingiza katika historia hapo kale ili kuonesha yajayo yaliyo ni utimilifu wa makubwa*. Dhabihu za wanyama ziliwakilsha taswira ya Kristo. Hivyo dhabihu za wanyama zilikuwa ni “aina” ya kristo. Hekalu kama makao ya Mungu lilimwakilisha Kristo ambaye ndiye hekalu la mwisho la Mungu ambaye kupitia yeye Kristo Mungu anakaa na watu wake ([Math. 1:23](#); [Yohana 2:21](#)). Makuhani wa Agano la kale walikuwa ni aina ya Kristo ambaye ndiye kuhani mkuu wa mwisho ([Waebra. 7:11–8:7](#)).

Utimilifu unatokea kikamilifu katika Kristo ([Ef. 1:10](#); [2 Cor. 1:20](#)). Lakini katika Agano jipya wanaoweka imani yao katika Kristo na kuwa na ushirika wake na hata Baraka zake hupokea faida za yale aliyoyakamilisha na hivyo mtu anaweza kuona “aina” ya Agano la kale inavyoliwakilisha kanisa, watu wote katika Agano jipya walio katia Kristo. Kwa mfano hekalu katika Agano la kale haliwakilishi Kristo tu ambaye yeye ni hekalu ([Yohana 2:21](#)), lakini pia inawakilisha kanisa ambalo pia linaitwa hekalu ([1 Kor. 3:16–17](#)), kwa sababu linakaliwa na roho mtakatifu. Alama zingine za Agano la kale zinaweza kuwakilisha matunda ya wokovu ya siku ya mwisho yatakayotokea katika mbingu mpya ambayo haijatokea ([2 Pet. 3:13](#); [Uf. 21:1–22:5](#)).

Yerusalemu ya Agano la kale inawkilisha Yerusalemu mpya “itakayoshuka kutoka mbinguni kwa Mungu” ([Ufunuo. 21:2](#)).

Kristo Mpatanishi

Biblia inaeleza wazi kwamba tangu anguko la Adamu dhambi na madhara yake imekuwa ni shida katika maisha yote ya mwanadamu. Ni kusudi kuu la Biblia yote. Dhambi ni uasi dhidi ya Mungu na inastahili kifo: “Mshahara wa dhambi ni mauti” ([Rum. 6:23](#)). Mungu ni mtakatifu, mwanadamu mwenye dhambi au mtu ye yote mashuhuri kama Musa anaweza kusimama katika uwepo wa Mungu bila kufa: “Huwezi kuniona uso wangu maana mwanadamu hataniona akaishi” ([Kutoka. 33:20](#)). Mwanadamu mwenye dhambi anahitaji Mpatanishi atakayemfikia Mungu kwa niaba yake. Kristo, ambaye ni mwanadamu na ni Mungu hana dhambi na ndiye anaweza kutumika: “Mpatanishi kati ya Mungu na mwanadamu na Mungu ni mmoja ambaye alijitoa mwenyewe kuwa ukombozi wa wote” ([1 Tim. 2:5–6](#)).

Japo kuna mpatanishi mmoja katika mtazamo lakini kwa namna mbalimbali kuna wapatanishi wengi katika Agano la kale waliokuwa na uwezo. Musa ni mmoja wao. Alipanda mlima Sinai na kukutana na Mungu na watu wote walimsubiri chini ya kilima ([Kutoka 19](#)). Wana wa Israeli walipoogopa sauti ya kutisha ya Mungu iliyotokea katika mlima walimwambia musa awe anawaleta maneno anayoyasema Mungu ([Kutoka. 20:18–21](#)). Mngu alimkubali Musa na akawa anawapelekea watu maneno ([Kumb. 5:28–33](#)).

Lakini ikiwa kuna mpatanishi mmoja kama vile [1 Timotheo 2:5](#) ilivyosema , kwa nini Musa alikuwa ni mpatanishi pia? Musa hakuwa ni mpatanishi mkuu bali alikuwa anamwakilisha kristo. Kwasababu Musa alikuwa ni mwenye dhambi asingeliweza kuukabili uwepo wa Mungu bila msamaha inamaanisha alitakiwa awe na mtu kwa niaba yake asiye kuwa na dhambi. Mungu alimkaribisha Musa atika uwepo wake kwa sababu kulingana na mpango wa Mungu Kristo aikuwa anakuja ilikuwa kwa ajili ya Musa. Faida za Kazi ya Kristo zilitambulikana tangu zamani kwa ajili ya faida ya Musa. Na ndivyo ilivyokuwa kwa watu wote wa Agano la kale. Sasa waliokolewaje? Mungu ni mtakatifu, na wote walipaswa kukamilika. Ukamilifu ulitolewa kwa neema kwa sababu ya Kristo aliye kuwa anakuja.

Hii inamaanisha kwamba kuna njia moja tu ya wokovu, Agano la kale lote kama ilivyo katika Agano jipy. Kristo ndiye peke yake anaweza kutuokoa. “Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote kwa maana hakuna jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo” ([Mdo 4:12](#)). Mifano yote ya wokovu katika Agano la kale imelalia kwa Kristo. Tungu Agano la kale wokovu umepatikana kupitia mpatanishi mtu au jambo lililosimama kati ya Mungu na mwanadamu. Mifano yote midogomidogo ya upatanishi katika Agano la kale inamwakilisha Kristo. Itakuwaje kwakuwa kunampatanishi mmoja na njia moja ya wokovu?

Kuelewa umoja wa Biblia kunapanua mtu anapoelewa *mifano ya jinsi Mungu alivyoleta wokovu kati ya mwanadamu na Mungu*. Mifano hii haihusishi tu Mungu kuleta wokovu wa kiroho katika mfumo wa ushirika wa binafsi, ushirika wa kiroho na ahadi ya uzima wa milele na Mungu. Zinahusisha pia mifano ya muda mfupi, na ukombozi wa nje—“Wokovu” katika ulimwengu

unaoonekana unatoa taswira ya wokovu katika ulimwengu wa Roho . Ukristo si kitu cha Kiroho tu. Wakristo wanategemea sana ufufuo wa miili na mbingu mpya na nchi mpya abapo haki inaishi” ([2 Pet. 3:13](#)). Wokovu binafsi unaanza kwa kuhuishwa moyo lakini mwisho itajulikana wazi na katika mtazamo wa kiuumbaji. Agano la kale linapozungumzia nchi inayoonekana, afya inavyoonekana hii inawakilisha mafanikio ya waumini katika ulimwengu mpya na nchi mpya inayoonekana.

Mifano ya wapanishi katika Agano la kale ni pampja na Manabii, wafalme na makuhani. *Manabii* walileta maneno ya Mungu kwa watu. *Wafalme*, wanaponyenyeka kwa Mungu sheria ya Mungu inakuwa juu ya watu. *Makuhani* waliwaandaa watu katika kuingia kwenye uwepo wa Mungu. Kristo ni nabii wa mwisho, mfalme na kuhani anayekamilisha kazi zote tatu katika utimilifu wa mwisho ([Waeb. 1:1–3](#)). Waweza kuwaangalia hata watu wa Hekima waliokuwa wanaleta hekima ya Mungu kwa wengine; *Mashujaa*, walileta ukombozi wa Mungu kutoka kwa Adui; na *waimbaji*, waliokuwa wanamsifu Mungu kwa niaba ya watu na kuzisema sifa zake mbele ya watu.

Upatanishi haufanyiki kwa sura ya mwanadamu, lakini kupitia idara. *Maagano* yanahusika katika upatanishi kwa kulileta neno la Mungu kwa watu. *Hekalu* linaleta uwepo wa Mungu. *Dhabihu za wanyama* inaleta msamaha wa Mungu kwa watu. Unaposoma Biblia unapaswa kuangalia jinsi Mungu anavyoleta Neno lake katika uwepo kwa watu kwa njia alizozikusudia. Njia zote hizi zinahusika na jukumu la upatanishi na kwasababu kunampatanishi mmoja ni dhahiri kwamba zote zinamlenga Kristo.

Injili Ni Nini ?

Injili ni hadithi. Ni hadithi ya Mungu. Marko 1:14 = inatuambia Yesu alivyo toka katika majoribu yake huko jangwani, “Akihubiri Injili ya Mungu”

Mathayo 4:23, Inatueleza Yesu alikuja akihubiri “Injili ya Ufalme.” Tazama Mathayo. 9:35; na Mathayo. 24:14.

1st Wakorintho 15:1-4 Inaeleza “Injili” ni Yesu, Jinsi alivyo na kile alichokikamilisha.

Moja ya njia ya kujifunza kitu kilivyo – ni kueleza kisicho Injili. Sina kitu kizuri ninachowezwa kukifikiria zaidi ya upotofu wa Wagalatia.

Historia ya Wagalatia inapatikana katika kitabu cha Matendo. Paulo anafika katika eneo ambalo kwa leo tunaliita ni Uturuki. Paulo alifundisha Injili safi ya neema, iliyokamilishwa kwa njia ya zawadi ya Mwana wake Mtakatifu Yesu. Kwa Paulo, maisha ya Kristo, Kifo, na kufufuka kunapokelewa kwa njia ya Imani na toba; haya yote yanahitajika kwa Mungu kwa ajili ya Msamaha wa dhambi.

Baada tu ya Paulo kuondoka eneo hilo lililokuwa linajulikana kama Galatia, Wakristo/ Wayahudi kutoka Yerusalem walimfuata Paulo kwenye haya makanisa mapya, wakiwaambia watu kwamba wanapaswa kutii “sheria” zilizowekwa na wanadamu za dini zao, kama vile kutahiliwa, sheria za Kiyahudi za Kosha, kuheshimu sherehe za kiyahudi na siku. Paulo akayaita mafundisho yao kuwa ni, “Injili nyingine.” (1:6)

Hii aina ya injili potofu bado inaendelea hadi leo. Makanisa mengi na madhehebu kwa namna moja wameiharibu Injili ya kweli. Mistari ya neema na matendo ni kusudi lililorudiwa rudiwa katika waraka huu = kuwapinga “hawa ndugu wa uongo” 2:4, na ile Injili tofauti waliyohubiri, 1:6

Ni injili tofauti kwa sababu iliibadili Neema = 1:7

Ni Injili tofauti kwa sababu iliuia Neema = 2:21

Ni Injili tofauti kwa sababu ilimpinga Kristo = 1:6

Ni Injili tofauti kwa sababu iliichafua Neema = 6:13; Warumi 6:1, 2

Paulo, aliyekuwa ni Myahudi mshika dini alielewa ni kwajinsi gani ilivyo rahisi kuchanganya dini na Injili

1. Maisha ya kale ya Paulo kama Myahudi mshika dini = Mistari 1:10-14

Zangatia: Sauli alikuwa na shauku ya mila na destruti zake. = 1:14

Hii inamanisha kwamba alikuwa na orodha kubwa ya matendo na hakujaribu kumpendeza Mungu!

Talmud= Sheria 613!!

Matumizi: Wakristo wa siku hizi wanaorodha yao na haujazivuka au unazo! Makanisa ya kimadhehebu yana sifa hizi za kuwa na “Injili tofauti.”

A. Mifano ya Injili isivyo:

1. Injili siyo falsafa inayokufanya kuwa mtu mwema.

Maelezo: Injli siyo kitu cha wewe kujiimarisha. Injili siyo kuhusu wewe! Haikuimalishi, Bali itakubadilisha! Tazama **2Kor. 5:17**, badiliko hili linakufanya uwe kama Yeye.

Matumizi: Uwe makini na Injili iliyobadilishwa “Inayoongeza” mambo fulani katika maisha yako badala ya kumwongeza Yesu mwenyewe!

Kielelezo: Wale wanaohubiri” Joel Osteen” Injili ya kujisikia vizuri, wanakwambia ni Injili. Hio si Injili.

2. Injili siyo kibali cha kuingia mbinguni (Tiketi ya kuingia mbinguni)

Maelezo: Wengi “Wamempokea Yesu” kwa njia ya maombi ya imani kama vile katika mikutano ya Billy Graham, wakidhani kwamba ni majumuisho ya Injili. “Niliomba, achana nayo” Nina tiketi ya kwenda!

Matumizi: Injili ni zaidi ya tiketi ya kwenda mbinguni; ni uvamizi wa mfalme na ufalme wake katika maisha yako.

3. Injili siyo mafanikio

Maelezo; Tatizo liko katika kuchukua mafundisho ya Agano la kale, kuhusu Baraka na laana na kuyaleta katika kanisa la Agano jipya.

Matumizi: Unadhani kama wewe ni mwema, au mzuri, unapata Baraka na kama ni mbaya unapata laana.

4. Injili si kwa ajili ya mambo ya baadae- (maisha ya baadae)

Maelezo: Wengi hawana matumaini ya nguvu iliyopo au faida ya kuokolewa kwao. Kwao Injili ni kwa ajili ya yajayo tu. Ni mbingu tu tena kwa Mungu wangu!

Matumizi: Injili ni ya Mungu na Ufalme wake. Tuko katika Kristo na utawala wake, ufalme na urejesho unaendelea ndani yetu sasa.

5. Injili siyo Upendo (Kwa Jirani yako)

Maelezo: Makanisa ya kidhehebu yanaishi kwa aina hii ya ujumbe wa uongo kuhusu upendo tu. Mpende Mungu na mpende jirani yako!

Hii ni injili nyingine kwa sababu ni vigumu kufanya! Yesu anaweza kuwapenda adui zake si wewe!

Hadithi Ya Injili Na Ufalme Wa Mungu

Utangulizi: Neno “*Injili*” linamanisha “Hadithi” au “hadithi ya Mungu.” Injili nne ziko katika uhalisi wa hadithi ya Mfalme na Ufalme wake. Kila kitu kinaleza hadithi kutoka katika mtazamo tofauti.

Utendaji: Mawazo ya magharibi yaani nchi za wazungu- Tunajaribu kuchayachanganua na kuifanya injili kuwa ni maelekezo kwa ajili ya maisha yaliyo fanikiwa. Hatari ni kwamba inaweza kukuweka katika hukumu haraka sana. Ni vizri kuiacha kila injili ijieleze yenewe na kuweka hoja zake yenewe.

Injili zinazofanana- Injili hizi tatu -Mathayo Marko na Luka zinaitwa “synoptic-Zinazofanana” kwa sababu zinaleza injili ya Yesu kitofauti lakini kwa njia ya kufanana (synoptic inamanisha “kuona sawa”)

Mathayo= Wazo “limetimizwa.” Yesu ni utimilifu wa ahadi za Agano la kale la kuja masihi. Kwa mfano hadithi ya Mathayo inaanza na vizazi vinavyoanzia kwa Ibrahimu na hivyo Yesu ni mwana wa Israeli, Masihi wake.

Marko= Yesu mwenye maajabu/ mtenda kazi amekuja, Yeye ni mtumishi/ mfalme alikuja kuokoa watu wote. Marko hana vizzazi bali anaanza na yohana mbatizaji

Luka=Vizazi vyake vinaanza na Adamu akionesha kwamba ni mwokozi wa ulimwengu. Yuko kwa ajili ya watu wote na si wayahudi.

Injili ya nne-Yohana= Yesu ni neno la Milele, neno la mwisho kwa mwanadamu. Ni neno lililofanyika mwili. Hadithi yake anaanza milele nyuma kabisa.

Injili zote nne zinatueleza hadithi ya Yesu:

I. Zinatueleza hadithi moja.

Hadithi ni kwamba uumbaji wote utafikia kilele katika kuja kwa ufalme wa Mungu. Wanatangaza kwamba, kizazi kipyä kimekuja na tukio kubwa limeshatokea katika kuja kwake Mfalme yesu. Hii haitakuwa hivo tena!

II. Zinatueleza hadithi yote iliyobaki -

Agano la kale limetimia katika Agano jipya. Israeli ya zamani imeshindwa, lakini sasa inatimia kwa watu wa Mungu wapya – Kanisa. Injili zote tazama ufalme wa Mungu kama matokeo ya Agano la kale. Biblia yote siyo kwamba imejaa hadithi mbalimbali bali zimeungana na kuwa hadithi moja kubwa, kwamba Agano la kale limetimia katika Agano jipya.

III. Wanatueleza hadithi za Wokovu – Mfalme mkombozi amekuja kumkomboa mwanadamu na kuweka ufalme wake.

maelezo: hadithi inaanza kwenye bustani ya Edeni ambapo Mungu anamuumba mwanadamu kwa sura yake. Adamu alikuwa mfalme na mtawala wa bustani . Tazama

Mwanzo 1:2

Kielelezo: neno moja la Mungu kwa Adamu = “Wewe ni mfalme tawala na Umiliki.”

Neno moja la shetani kwa Adamu = “wewe si mfalme wewe ni Mungu”

Utendaji: hadithi ya injili ni kwamba Mungu ni Mfalme na Yesu ni Adamu wa pili, (Tazama **Warumi 5: 12- 19**) Alipanda msalabani na kufanya kuwa ni Enzi yake na kuushinda utawala wa shetani. Adamu wa pili anatawala na Enzi yake ni msalaba! Yesu amekuja na wokovu kwa wanadamu wote unawezekana kwa wale watakaokubali neema yake ya msamaha.

IV. Agano la kale **Hadithi ya Kutoka**.

Maelezo: Hadithi ya Israeli ni kwamba Mungu ameikomboa Israeli kutoka utumwani misri. Hadithi hiyo ni wazo endelevu katika Injili –Mfalme atawaokoa watu wake. Kutoka kwetu ni tukio la kifo cha msalabani, kuzikwa na kufufuka na kupaa kwa mfalme yesu ambaye alituoa kutoka katika vifungo vya dhambi. Katika maana hii wokovu ni kukombolewa kutoka katika vifungo vya dhambi.

Injili & Ufalme wa Mungu

Wokovu kwa wayahudi ilikuwa kwamba Mfalme mwema na mwenye nguvu (Kama daudi) amshinde mfalme mbaya. Somo la uhamisho ni hukumu ya Mungu dhidi ya mtawala mbaya (farao) aliyekuwa akiwatawala. Utimilifu wa hadithi ni kwamba mfalme wetu yesu ameyatoa maisha yake kwa ajili ya ukombozi wetu.

Kielelezo: katika kitabu cha **Daniel** anapata maono anaiona siku ambapo MUngu ataweka Mfalme wake (Mwana wa Mtu) katika enzi yake ili kusimika ufalme usio na mwisho na kutawala falme zote za wanadamu. Mfalme mkuu wa Mungu na ufalme wake anakuja.

Zingatia: Wayahudi waliona ufalme huu na mfalme ila wazo lao lilikuwa kwamba Masihi atakuwa ni mpiganaji wa vita vya duniani. Tazama **Isaya 9:6, 7**

Kielelezo: Yohana Mbatizaji aliwapatia Israeli **Mwanakondoo/Mfalme**, wayahudi walikuwa **simba/Mfalme!** Yesu alikuwa ni mwokozi wao /mfalme wa kuwaokoa Israeli, lakini wayahudi waliona Rumi tu na wakataka wakombolewe kutokas katika utawala wa Rumi.

V. Hadithi ya injili ni kwamba **“Masihi”** yuko hapa.

Yesu ni Israeli (Mfalme Mungu) aliyetimizwa. Kama vile ilivyokuwa kwamba taifa la Israeli lilikuwa ni mwana aliyechaguliwa kwa maana hiyo hiyo Yesu ni Israeli Mwana wa Mungu aliyeahidiwa. Yesu ni mwana wa Daudi tu bali na daudi mkuu.

VI. Injili inatuambia kwamba watu wapya wa Mungu (Israeli?Yesu anakaa ndani yao) wanawenza kufanya kile ambacho Israeli ameitiwa kufanya. Wito wa kanisa ni kusimika utawala wa mfalme katika kila taifa.

Muhitasari na Utendaji:

1. Mfalme amekuja na ameleta ufalme wake pamoja naye.

Hii inamanisha “Ufalme uje’ tayari uko hapa. Malai Yesu “yupo” utawala, nguvu na uwepo wake unaweza kuonekana. Neno “tayari” na “hapana bado” limeanzia katika mauti, kuzikwa na kufufuka kwa Mfalme Yesu.

2. Ufalme uko hapa sasa na uko ndani yako – Mtoto wa Mungu.
Ufalme uko kwa kila motto wa Mungu aliye zaliwa mara ya pili. Kristo ndani yako ni tumaini la utukufu.
3. Utawala wa ufalme unapatikana kwa wote walio na Roho wa Mfalme. Somo la ufalme lina “Utawala.” Hatutawaliwa na mazingira bali tunatawaliwa na nguvu na uwepo wa ufalme. Yesu ametupatia mamlaka yake (Tazama **Mathayo 28:18**)
4. Hadithi ya Mungu (Injili) inasema kwamba kama Adamu wa kale unajukumu la kuhusika katika ufalme huu. Unapaswa kutoka na kwenda kuanza kuwaita “majina wanyama wote.” Unamamalka ya “Kuja kwa ufalme” kufanya mapenzi ya Mungu na kutawala dunia na kusambaza sura ya Mungu kwa mataifa yote.
5. Unapaswa kuamini, kuitenda na kuleta “Ufalme uliokuja” kwenye maisha yako.

Mamlaka ya Maandiko Matakatifu

Biblia na Ufunuo

Jua kuwa Mungu ni kitu Muhimu katika maisha. Mungu kaumba watu kwa lengo la mahusiano na Yeye mwenyewe. Mahusiano haya yanategemea Yeye ni nani kwasababu kajidhihirishwa mwenyewe. Mungu ni nafsi, inamaanisha ana akili, Hisia, mahusiano na utambuzi. Kwa sababu ni nafsi na si nafsi isiyo na utambuzi na hivyo Mungu lazima ajifunue kwetu. Ameyafanya haya katika ufunuo wake wa jumla (Dunia) na ufunuo maalumu (Neno la Mungu).

Ufunuo wa Jumla

Ufunuo wa jumla ni ufunuo wa Mungu kwa watu wote wakati wote. Ufunuo huu unaonekana katika uumbaji wake wa vitu vinavyoonekana ([Zaburi. 19:1](#), “Mbingu zauhubiri utukufu wa Mungu”)kuwa dhahiri kwao ([Rum. 1:19–20](#), “Kwa kuwa mambo ya Mungu yanayojulikana yamekuwa dhahiri ndani yao kwa maana Mungu aliwadhihirishia kwasababu mambo yake yasiyoonekana tangu kuumbwa ulimwengu yanaonekana na kufahamika kwa kazi yake yaani uweza wake wa milele na uungu wake hata wasiwe na udhuru”). Ufunuo wa jumla huonesha sifa za Mungu — kama vile, uwepo wake, nguvu, ujuzi, na hata hakima, kwa nyongeza ushuhuda wa ufahamu wa mwanadamu unatoa maadili ya kimungu kwa wanadamu wote ([Rum. 2:14–15](#)). Hii inamaanisha kwamba ufunuo wa jumla unawapa watu kujua kwamba Mungu yupo, ufahamu wa sifa zake, na hata ufahamu wa maadili yake. Hii inatupa umakini wa kushtakiwa tunapokuwa mbele za Mungu kwamba tumemkosea tunapokwenda kinyume na maadili yake. Katika dini nyingi za uongo zilizokuja watu wengi wamekuwa wakijifariji katika dhamira zao.

Lakini ufunuo wa jumla hautoi ufahamu wa jawabu la kweli juu ya dhamira ya mwanadamu mbele za Mungu: msamaha wa dhambi unaopatikana kwa njia ya Yesu kristo. Hii inamaanisha kwamba ufunuo wa jumla hautoi ufahamu binafsi wa Mungu kama Baba mwenye upendo wa kuwakomboa watu wake na kuweka Agano nao. Kwa hili, mtu anahitaji Ufunuo maalumu ambao Mungu kaufanya katika historia kwa njia ya pekee, katika Biblia, na hata katika Yesu kristo.

Ufunuo Maalumu

Biblia ni ufunuo wa Mungu ulioandikwa kwamba yeche na nani na kile alichokifanya katika historia ya ukombozi. Wanadamu wanahitaji uungu huu, mtazamo ambao utaharibu kabisa malengo yao binafsi, vifungo ya asili na hali ya kuanguka. Kwa njia ya Neno la Mungu lililo andikwa watu wake wanaweza kushinda upotofu, kukuwa katika utakaso, kutumikiana kwa nguvu na kuishi maisha ya milele kama Mungu alivyokusudia.

Uvuvio wa Maandiko

Biblia ni “Neno lililovuviwa na Mungu” (cf. [2 Tim. 3:16](#)) na kupokea mamlaka yake ya kweli, nguvu, sifa takatifu kutoka kwa Mungu mwenyewe ambaye aliwavuvia wanadamu kuandika kwa hakika kile alitaka waandike. Badala ya kuwapa maneno Mungu alitumia utu wao wa kipekee na hata matukio. Maandiko ni ya kibinadamu na ni ya Kiungu kabisa. Ni ushuhuda wa watu kwa ufunuo wa Mungu na ufunuo wa Mungu mwenyewe. “*Mkijua neno hili kwanza, ya kwamba hakuna unabii katika maandiko upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu Fulani tu. Maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu bali wanadamu waliyanena yote yaliyotoka kwa Mngu wakiongozwa na roho Mtakatifu*” ([2 Pet. 1:20–21](#)). Kwa kuwa Biblia ni neno la Mungu kwa njia ya maneno ya wanadamu inaweza kuaminika kama Ufunuo halisi kutoka katika kinywa cha Mungu.

Usahihi wa Maandiko

Usahihi wa mafundisho inamaanisha kwamba Biblia yote ni kweli na kamilifu katika asili yake. Njia nyingine ya kulizungumzia hili ni kwamba Biblia haijipindi. Kwa kuwa Mungu ndiye mwandishi mkuu wa maandiko na kwa sababu yeye ni kweli hivyo hata neno lake ni kamilifu na kweli pia : Yeye ni “Mungu asiyedanganya” ([Tito 1:2](#)). Itakuwa inapingana na sifa zake tukisema kwamba anaweza kusema kitu cha uongo. Mungu anjua yote,yeye ni mweli na mwema, ana nguvu zote, yeye anajua na ansema kwelina anaweza kuwasiliana na kulitunza neno lake. “Ee Bwana Mungu , Wewe ni Mungu , na maneno yako ni kweli na umeahidi mambo mema kwa watumishi wako ” ([2 Sam. 7:28](#)). “Kila neno la Mungu linasema kweli” ([Methali. 30:5](#); cf. [zaburi. 12:6; 119:42](#); [Yohana 17:17](#)).

Usahihi hauhitaji ukweli wa karne ya ishirini na moja au lugha ya kisayansi. Nukuu zifuatazo kutoka katika tamko la chikago juu ya ukweli wa Biblia inaeleza nini Usahihi haumaanishi:

Tunathibitisha kwamba matumizi sahihi ya inerrancy kama neno la kitheologia pamoja na rejea ya ukweli kamili wa maandiko. Tunakataa kwamba ni sahihi kuyatathimini maandiko kulingana na kiwango cha ukweli na mapotofu yaliyokaribiana na matumizi au makusudi yake. Tunaendelea kukataa kwamba inerrancy na imekataliwa na mambo ya Kiblia kama vile maelezo sahihi ya sasa , hali isiyo ya kawaida, misamiati au maneno, maelezo asili ya mitazamo, taarifa za uongo, matumizi ya uongo, mpangilio wa vitu, mchanganuo wa vitu mfuatano au utumiaji wa maeneo (*Chicago Statement on Biblical Inerrancy*, Art. XIII).

Inerrancy ya maandiko inampatia Muumini ujasiri katika Biblia kwa kuwa msingi wake wa uelewa ule Mungu anaotaka auelewe na kile anachokihitaji katika uungu na uzima wa milele.

Uwazi wa Maandiko

Biblia yenye kujifunza inakubali kwamba kuna sehemu nyingine katika Biblia ni “Ngumu kuzielewa” ([2 Pet. 3:16](#), inagusia mitazamo ya nyaraka za Paulo). Kwa ujumla, kwa ufunuo wa maandiko kwa njia ya roho mtakatifu ([2 Tim. 2:7](#)), mafundisho ya Boiblia ni wazi kwa wale walio na lengo la kumjua na kumtii Mungu. Neno lake linasema “Kuwaelimisha walio wa kawaida” ([Zaburi.](#)

[19:7; 119:30](#)). Yesu mafundisho yake yalilalia katika Agano la kale: Alimaanisha maandiko yake ni wazi na mara zaote alisema , “Hamkusoma … ?” (cf. [Math. 12:3, 5; 19:14; 21:42; 22:31](#)).

Kwa sababu ya uwazi wa maandiko Wakristo wanaposhindwa kukubaliana juu ya aya ya maandiko wanasema kwamba tatizo siyo katika maandiko bali ni wao jinsi wanavyoitafasiri na kuelewa. Mungu katupatia watu wanaoweza kutusaidia katika uelewa ([1 Kor. 12:28; Ef. 4:11](#)). Waumini wanajukumu la kusoma, kutafasiri, na kuelewa Biblia kwasababu ni wazi. Hili ndilo lilikuwa ni wazo la waanzilishi wa uporotestanti walioona watafasiri Biblia katika lugha za kawaida za wanadamu. Waliamini kwamba wakristo wote ni makuhani walio na uwezo wa kumjua Mungu kwa njia ya Neno lake na kuwasadia wengine.

Ukamilifu wa Maandiko

Maandiko yanatupatia maneno yote yanayohitaji tumjue Mungu kabisa na kibinagsi, na kila kitu anachotaka kutueleza ili tuweze kuishi maisha tele ya Kimungu ([Zaburi. 19:7–9; 2 Tim. 3:15](#)). Mungu kawapatia watu ufunuo wake wa kutosha ili kwamba waweze kujua, kumtegemea, na kumtii. “*Kila andiko lenye pumzi ya Mungu lafaa kwa mafundisho na kwakuwaonya watu makosa yao na kwakuwaongoza na kwakuwaadibisha katika haki. Ili mtu w Mungu awe kamili amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema*” ([2 Tim. 3:16–17](#)). Mungu anaamuru kwamba kisiwepo kitu cha kuongezwa au kupunguzwa inayoonesha kwamba Biblia ni kamili kile alichokihitaji katika kila hatua katika historia yote ya maandiko hadi wokovu.. “*Msiliongeze neno niwaamuruo wala msilipunguze mpate kuzishika Amri za Bwana Mungu wenu niwaamuruzo*” ([Kumb. 4:2](#); cf. [Kumb. 12:32; Metha. 30:5–6](#)). Uharibifu mkubwa dhidi ya usahihi katika hitimisho la Biblia yote ([Ufunuo. 22:18–19](#)) inatumika zaidi katika kitabu cha ufunuo lakini katika maana nyingine inaweza kuwa katika Biblia yote: “*Namshuhudia kila mtuayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki mtu yeyote akiyaongeza Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyo andikwa katika kitabu hiki. Na Mtu yeyote akiondoa lolote katika maneno ya unabii wa kitabu hiki Mungu atamwondolea sehemu yake katika mti ule wa uzima na katika ule mji mtakatifuambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki*” ([Ufunuo. 22:18–19](#)).

Waumini wanapaswa kuona uhuru na kutiwa moyo katika kushukuru kwamba Mungu amefanya maelekezo yote yenya mamlaka yanayohitajika ili kumjua na kuishi kama alivyokusudia. Hivyo waumini wanapaswa kutisherezwa na kile Biblia inachofundisha na kile ambacho haijakisema. “*Mambo ya siri niya Bwana Mungu wetu lakini mambo yaliyofunuliwa ni yetu sisi na watoto wetu milele ili tuyafanye maneno yote ya sheria hii*” ([Kumb. 29:29](#)).

Mtazamo wa Yesu wa Maandiko

Sababu inayotushawishi tuamini kwamba Biblia imevuviwa, kamilifu, wazi, na haina upungufu ni kwasababu hiki ndicho Yesu aliamini. Mafundisho yake yalisema kwamba Agano la kale lilikuwa ni mamlaka ya Baba yake: “*Mlidhani ya kwamba nimekuja kuitangua sheria au Manabii, sikuja kuitangua bali kuitimiliza, kwa maana nasema hakika, mpaka mbingu na nchi zipite yodi moja wala Nukta moja ya torati haitaondoka hata yote yatimie*” ([Mathayo. 5:17–18](#)). Yesu anazungumzia dazeni za matukio na watu wa Agano la kale na aliquwa anaichukulia kwamba agano la kale na historia yake ni sahihi. Alinukuu katika kitabu cha Mwanzo kama maneno ya Baba yake aliposema, “Hamkusoma ya kwamba ye ye aliye waumba mwanzo

aliwaumba mtu mme na mtu mke. Akasema kwa sababu hiyo mtu atamwacha babaye na mamaye ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja? Hata imekuwa si wawili tena bali mwili mmoja basi aliowaunganisha Mngu mwanadamu asiwatengenishe” ([Mathayo. 19:4–6](#)). Yesu hadhani kwamba swla la uumbaji lilikuwa so kweli lakini alinukuu maneno kutoka katika kitabu cha Agano la kale ambayo Mungu mwenyewe alisema

.”Ilikuwa ni kawaida theologia ya Yesu kunukuu ukweli wa Agano la kale ([Mat. 5:12; 11:23–24; 12:41–42; 24:37–39](#); [Luka 4:25–27; 11:50–51](#); [Yohana 8:56–58](#)). Mtazamo wa Yesu katika Agano la kale linalojisema lenyewe.

Yesu alijiona kwamba yeche ni mtimizaji wa maandiko ([Math. 26:54](#); [Marko 8:31](#)). Maisha yake yote, Yesu alitumia maandiko kushinda majaribu ([Mat. 4:1–11](#)) na kukanusha ubishi ([Math. 19:1–12; 22:39; 27:46](#); [Mark 7:1–13](#); [Luka 10:25–26](#)). Mwishoni mwa maisha yake Yesu alikufa akinukuu Agano la kale (cf. [Matt. 27:46](#) pamoja [Zaburi. 22:1](#)). Wakati wa kufufuka kwake alieleza maandiko akiwa katika njia ya Emausi na kwa wanafunzi wake katika Yerusalem ([Luka 24:13–17, 44–47](#)).

Utambuzi wa jinsi alivyo kama Mungu Bwana Yesu aliona kwamba mafundihso yake yanauvuvio sawa na ule wa Agano jipya. Yesu alifundisha kwa mamlaka tofauti na walimu wengine wa sheria. Aliitafasiri sheria kwa mamlaka yake bila kutegemea vyanzo vya rabi ([Math. 5:21–48](#)). Alieleza sheria na mafundisho yake kama kitu sawa: “*Mbingu na nchi zitapita lakini maneno yangu hayatapita kamwe*” ([Mathayo. 24:35](#), cf. [Mathato. 5:17–18](#); [Yohana 14:10, 24](#)). Yesu alitazama Agano la kale na mafundisho yake kama yote ni maneno ya Mungu. Ushuhuda wa kitume ulikuwa ni matokeo ya Roho Mtakatifu kuweka kweli za kiroho katika uandishi na si maneno yam domo tu ([Marko 3:13–19](#); [Yohana 16:12–14](#); [Mdo 26:16–18](#); [1 Kor. 2:12–13](#)).

Yesu aliyachukua maandiko na kuyafanya kuwa ni mamlaka ya mungu aliyoyaweka katika maisha yake yote. Wale wanaomfuata Kristo wanahimizwa kuyatendea maandiko (Agano la kale na Agano jipya) kwa namna ile ile. Kwa wakristo, Biblia ni Nguvu na Furaha yetu. Mungu anapaswa kutafakariwa katika Neno lake ([1 Petro. 2:2](#)). Neno la Mungu ni hazina nzuri inayopaswa tujifunze, tuitafakari na kutii:

Mwanangu kama ukiyakubali maneno yangu na kuyaweka akiba maagizo yangu hata ukatega sikio lako kusikia Hekima ukauelekeza Moyo wako upate kufahamu, Naam ukiita busara na kupaza sauti yako upate ufahamu ukiutafuta kama fedha na kuutafutia kama hazina iliyositirika ndipo utakapofahamu kumcha Bwana na kupata kumjua Mungu ([Methali. 2:1–5](#)).

THEOLOGIA YA AGANO JIPYA

Imehaririwa kutoka katika maelezo ya Biblia ya kujifunzia ya ESV

Theologia ya Agano jipya ni tawi la kile wasomi wanakiita “Theologia ya Biblia.” Theologia maalumu na Theologia ya Biblia zinaungana kwani zote zinaonyesha theologia inayopatikana katika Biblia. Theologia ya biblia hata hivyo inazingatia sana katika maelezo ya historia ya Biblia na inaeleza hatua mbalimbali katika mpango endelevu wa kazi za Mungu katika historia ya ukombozi. Katika kitabu hiki moja ya mada kuu ya theologia ya Agano jipya imeonyesha.

Tayari lakini Bado kidogo

Ujumbe wa Agano jipya hauwezi kutenganishwa na ule wa Agamo la kale. Kama utasoma tu Agano jipya Bila kulielewa Agano la Kale hutaweza kuelewa kabisa Yesu ni nani na kile alichokuja kufanya. Agano la kale linaeleza kwamba Mungu atakuja kuwaokoa watu wake akianza na ahadi ya uzao wa mwanamke kuwa utashinda uzao ule wa nyoka. (**Mwa. 3:15**). Ahadi za Mungu za kuokoza ziliendelezwa hasa katika Agano alilolifanya na watu wake (1) Agano la Ibrahim liliwaahidi watu wa Mungu nchi, uzao na Baraka za duniani (**Mwanzo.12:1-3**; (2) Agano la Musa likaonesha Baraka kama watu watatii sheria (**Kutoka 19-24**); (3) Na Agano la daudi liliahidi Mfalme katika ukoo wake milele na kwamba kupitia mfalme wake ahadi zote zilizofanywa kwa Ibrahim zitatimia (**2 Samweli 7; Zaburi 89; 132**) na (4) Agano jipya liliahidi kwamba Mungu atamwaga Roho wake kwa watu wakena kuandika sheria zake katika mioyo yao ili wapate kutii mapenzi yake (**Yer.3:31-34; Ezek. 36:26-27**).

Yohana mbatizaji na Yesu walifika katika tukio moja ilikuwa wazi kwamba ahadi ya Mungu iokoayo ilikuwa bado hajatambulika. Warumi walikuwa wakiwatawala waisraeli na Mfalme wa daudi alikuwa bado hajatawala katika nchi. Baraka za dunia zilizokuwa zimeahidiwa kwa Ibrahim zilikuwa ni wazi japo katika Israeli ilikuwa ni dhambi, hakuna haki, iliyyotawala. Yohana Mbatizaji akawahutubia watu wa Israeli watubbu na wapokee ubatizo wa maji kutangaza kwamba walikuwa tayari kumpokea Masihi. Walipaswa wajiandae kwa ajili ya yeye ajaye atakayeachilia Roho na kuwashukumu waovu.

Yesu mnazarethi anakamilisha kile Yohana mbatizaji alikitabiri. Yesu kama Yohana alitangaza ujio wa ufalme wa Mungu (**Marko 1:15**), ambayo ni njia nyingine ya kusema kwamba ahadi ya ukombozi ilioonekana katika Agano la kale ilikuwa mbioni kutambulika. Ufalme wa Mungu hata hivyo ulikuja kwa namna ambayo haikutegemewa. Wayahudi walikuwa wameeleza kuwa ufalme utakapofika maadui wa Mungu wataondolewa haraka iwezekanavyo na uumbaji mpya utashuka (**Isa. 65:17**). Yesu alifundisha kwamba ufalme ulikuwa umeshakuja katika nafsi ya Kristo na huduma yake (**Luka 17:20-21**) nab ado maadui wa ufalme hawakuondoshwa. Ufalme haukuja na nguvu ya kijeshi lakini ulikuwa kidogo kama mbegu ya haladali na baadae ungekuwa kama mti mkubwa ambao ungeenea dunia yote. Haukulikana kama amira iliyochanganywa na Unga lakini amira inaumua ndoge zima la unga (**Math. 13:31-33**). Kwa maneno mengine Ufalme tayari ulikuwa kwenye huduma ya yesu lakini ulikuwa haujamilika kabisa.

Ulikuwa “tayari – lakini bado.” Ulikuwa umeshasimikwa lakini haujaanza kutumiwa. Yesu alkikamilisha majukumu ya mtumishi wa Bwana katika **Isaya 53**, akichukua dhambi za watu na kifo cha mateso kwa ajili ya msamaha wa dhambi zao. Siku ya hukumu bado ilikuwa inakuja hapo baadae japo kulikuwa na kipindi katikati cha Mungu kuanza kutimiza ahadi zake katika Kristo (ufalme unasimikwa) na hatima ya kutambua ahadi yake ya mwisho (ufalme unatumwiwa). Yesu ambaye amekuwa akitawala tangu alipofufuka atarudi na kukaa katika kiti chake cha utukufu na kuhukumu mbuzi na kondoo (**Mat. 25:31-46**). Kwa hiyo waumini wanaomba kwa ajili ya ukuaji endelevu na hatima ya ufalme kwa maneno kwamba “*Ufalme wako uje*” (**Mat.6:10**).

Injili zinazofanana (Mathayo, Marko, na Luka) wametazama sana katika ahadi za ufalme na Injili ya Yohana inaeleza kweli ile ikitumia neno “*Uzima wa Milele.*” Uzima wa milele ni uzima wa kizazi kijacho ambacho kitatambuliwa pindi uumbaji mpya utakapoletwa. Kitu cha kukumbuka katika Injili ya Yohana ni yale madai kwamba wale wanaomwamini mwana wanafurahia maisha ya kizazi kijacho sasa. Wale ambao wamekwisha kuweka Imani yao katika Yesu wamepita mauti na kuingia uzima (**Yohana 5:24-25**), Maana yeye ni ufufuo na uzima (**Yohana 11:25**) Bado Yohana anatazama mbele kwenye siku ya ufufufuko wa mwisho ambapo kila mtu atahukumiwa kulingana na vile alifanya (**Yohana 5:28-29**). Kwa kuwa mtazamo wa Yohana uko katika mwanzo wa utimilifu kimtazamo pia.

Neno “tayari –ila bado” limetawala Agano jipyga na linatenda kama msingi ili kuelewa habari nzima ufufuko wa Yesu unaonyesha kwamba kizazi kilichotakiwa kuja kimeshawasili na kwamba sasa ni saa siku ya wokovu. Kwa namna hiyo hiyo karama ya roho Mtakatifu inaonyesha ahadi ya mwisho ya nyakatio za Mungu. Waaandishi wa Agano jipyga walitangaza kwamba ahadi ya kumwagiwa Roho Mtakatifu imekwisha kukamilika (Mfano., **Matendo 2:16-21; Warumi. 8: 9-16; Waefeso.1:13-14**). Siku za Mwisho zimekwishga kuja kupitia Yesu Kristo (**Waeb. 1:1-2**), Kupitia Yeye ambaye tumepokea Neno la Mungu la mwisho. Kwa kuwa kufufuka kumeshapenya sana katika Historian a Roho amekwisha kutolewa tunaweza kufikiri kwamba Historia ya wokovu imekwisha kukamilika lakini ielewewe kwamba bado kuna neno “*bado.*” Yesu ameshafufuka kutoka wafu lakini waumini wanashubiri kufufuliwa kwa miili yao na wanapaswa kupambana na dhambi hadi siku ya ukombozi (**Rum. 8:10-13 23; 1kor. 15:12-28; 1 Pet. 2:11**). Yesu anatawala juu katika mkono wa kuume wa Mungu lakini vitu vyote bado havijatiishwa kwake (**Waeb. 2:5-9**).

Utimilifu kwa Njia ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu

Agano jipyga linaeleza utimilifu wa ahadi ya ukombozi wa Mungu lakini inapanua ahadi hizo na maagano yanatambulika kupitia mwana wake Yesu Kristo.

Yesu ni nani? Kulingana na Agano Jipyga yeye ni Musa mpya na Bora neno la Mungu linamtangaza kama **mtafasiri mkuu wa sheria ya Musa** (**Mat. 5:17-48; Waeb. 3: 1-6**).

Kiukweli sheria na manabii

wanamwonyesha Yesu na kupata utimilifu wao katika yeye, Yesu ni Yoshua mpya anayetoa pumziko la mwisho kwa watu wake (**Waeb. 3:7-4:13**). Yeye ni hekima ya kweli ya Mungu akitimiza na kuleta nia ya hekima kutoka katika Agano la kale (**Wakol. 2:1-3**) Katika Injili Yesu ametambuliwa kama nabii. Kiukweli yesu ni nabii wa Mwisho aliyetabiiwa na Musa (**Kumb.18:15; Matendo, 3: 22-23; 7:37**). Miujiza ya yesu, Uponyaji na mamlaka juu ya mapepo inaonyesha kwamba ahadi ya ufalme imetimizwa katika yeye (**Math. 12:28**), Lakini miujiza yake inaonesha kwamba anashiriki mamlaka ya Mungu nay eye mwenyewe ni Mungu, na Pekee Muumbaji–Bwana anweza kutembea katika maji na kutuliza bahari (**Math. 8: 23-27; cf. Zaburi. 107:29**). Yesu ni masihi anayetupa kujua ahadi kwamba yuko mtu atakaa katika kit cha daudi milele. Kumontambua Yesu kama masihi ni msingi wa Injili zote na mahubiri ya kimisionari katika matendo ya Mitume na ni kweli inayokubalika katika nyaraka na ufunuo. Kusema Yesu ni Masihi ni kutangaza kuwa Yesu ni Mfalme. Wanafunzi wake walipomwita “Bwana” walikuwa wanamtambua kama Mungu mfalme wa mamlaka.

Sura ya Yesu inaonyekana katika maelezo yote ya Agano jipyka kwa ajili ya wito wenye mamlaka ya kuwaita wengine waje wawe ni wanafunzi anawahutubia waweze kumfuata (**Math. 4: 18-22; Luka 9:57-62**). Kiukweli mwitikio wa mtu kwa Yesu unategemea na hatima yake (**Math.10:32-33; cf, 1 Kor.16:22**) Yesu ni mwana wa Mtu ambaye atapokea ufalme kutoka kwa mzee wa siku (**Dan. 7:13-14**) na atatawala milele. Injili inakazia hata hivyo utawala wake umekwisha kutambulika kwa njia ya mateso kwa maana yeye ni mtumioshi wa Bwana ambaye aliteseka kwa ajili ya dhambi za wanadamu (**Isa. 52:13-53:12; Marko 14:24; Rum. 4: 25; 1Pet.2:21-25**).

Mtu anayeteseka kwa ajili ya dhambi ni Mungu kamili na ana uungu. Anamamlaka ya kusamehe dhambi (**Marko 2:7**). Matukio mengi ya Agano jipyka yanaonekana na neno “Jina” inaonesha uungu wa Yesu: watu wanatabiri katika jina lake (**Math. 7:22**). Wanatumaini katika Jina lake (**Math. 12:21**). Na wokovu unapatikana katika jina lake peke yake (**Mdo.4:12**). Lakini katika Agano la kale linaonesha kwamba Watu walitabiri katika jina la Mungu. Tumaini pekee katika Bwana, tunapata wokovu katika Yeye na hivyo utumiaji wa Jina la Yesu unaonesha uungu wake.

Tafasiri ya kiyunani ya Agano la Kale (the Septuagint) inaonesha kwamba Yahwe kama “Bwana”. Kwa kunukuu katika maelezo ya Agano la kale maneno yanayoeleza Yahwe katika yalikuwa na maana ya jina “Bwana” ambaye ni yesu na katika agano la kale yalitumika kwa msisitizo sana (e.g., **Mdo.2: 21; Wafil. 2:10-11; Waeb. 1: 10-12**). Kwa hiyo sifa ni sehemu nyingine inayoonesha uungu wa Kristo kwamba Yesu niu sura ya Mungu (**Wakol.1:15 cf. Waeb. 1:3**). Yeye yuko katika sura ya Mungu na ni sawa na Mungu japo wakati mwingine alionekana kama mwanadamu ili apate kutuokoa (**Wafil.2:6-8**). Yesu ni Mwana wa Mungu (**cf. Math.28:18; Yohana 20:31; Rum. 8:32**) na anaabudiwa kama Baba aabudiwavyo (**cf. Ufunuo 4-5**) Ufalme wako unakumbukwa kwa kushiriki chakula cha meza ya Bwana (**Marko 14: 22-25**) na kwa watu kubatizwa katika Jina lake (**Matendo 2: 38; 10:48**). Mwana wa Mungu ni kazi ya Milele ya Mungu (Kiyunani Logoz) ambaye alifanyika mwili na akatambuliwa kama

Mwanadamu ambaye ni mwana wa Mungu (**Yohana 1: 1, 14**). Mwisho katika maelezo mengi Yesu anaitwa “Mungu” (e.g., **Yohana. 1:1, 18; 20:28; Rum.9:5; Tito 2:13; Waeb. 1:8; 2 Pet. 1:1**). Shaya maandiko hayana michanganyiko ya upotofu kwamba ni mfano au kwamba ni watatu. Bali maelezo haya yanachukua vitu ambavyo mafundisho ya utatu yalianzishwa.

Theologia ya Agano jipya ni kitovu cha Kristo na Mtazamo kwa Mungu kwa maana ya kwamba kile Yesu anafanya duniani kinampa Mungu utukufu (**Yohana 17: 1; Wafilipi.2:11**). Agano jipya limeangalia sana kazi za Yesu msalabani kwamba aliwakomboa na kuwaokoa watu. Hadithi zote katika kila Injili zimeangalia kifo cha Yesu na ufufuko wake. Kiukweli maelezo ya mteso ya Yesu na kifo imechukua nafasi kubwa sana katika Injili ikionesa kwamba kwamba msalaba na kufufuka ndiyo kiini cha habari. Katika matendo tunaona kukua kwa kanisa na kupanuka kwa Huduma pale mitume na wengine walipokuwa wakimtangaza msulubiwa na aliyefufuka Bwana. Nyaraka zinazeleza umuhimu wa kazi ya Kristo msalabani na ufufuko wake ili kwamba waumini wapate kujua urefu, kina, upana na urefu wa upendo wa Mungu (**Rum. 8:39**). Umuhimu wa msalaba umkeelezwa kwa ukiendana na misingi kama uumbwaji, kufanywa mwana, msamaha wa dhambi, kuhesabiwa haki, kupatanishwa, ukombgozi, kutakaswa na hata kulipiwa deni kiukamilifu, na misingi hii pamoja inafundisha kwamba Wokovu unatoka kwa Bwana. Na kwamba yesu kama Kristo amewakomboa watu wake kutoka katika dhamira na vifungo vyta dhambi.

Ahadi ya Roho Mtakatifu

Tumeungamanishwa na kazi za Kristo ambazo ni kazi za Roho Mtakatifu. Yesu aliahidi kutuma Roho Mtakatifu kwa wale walio wanafunzi wake wa Kweli. (**Yohana 14:16-17, 26; 15:26**). Na akamwachilia Roho Mtakatifu kwa watu wake siku ya Pentekoste (**Mdo 2: 1-4; 33**) Baada ya kuwa ameinuliwa katika mkono wa kuume wa Mungu Baba. Roho alitolewa ili ampe utukufu Kristo (**Yohana 16: 14**) Ili kwamba Kristo atukuke kama mwokozi mkuu na mwokozi. Luka na Matendo wanakazia sana kwamba Roho Mtakatifu ametolewa kwa ajili ya huduma ili kwamba kanisa liweze kuimalishwas lishuhudie Yesu Kristo. Kwa wakti huo huo kuwa na Roho Mtakatifu ni alama ya kwamba mtu anakuwa ni sehemu ya watu wa Mungu (**Mdo. 10:44-48; 15:17-9; Rum. 8: 9; Wagal. 3:1-5**). Roho pia anawaimarisha wakristo ili wawezeshwe kuishi kwa namna ambayo inampendeza Mungu. Kuwa katika sura ya Kristo ni kazi ya Roho Mtakatifu (**Rum. 8:2, 4:13,14; Kor. 3:18; Wagal. 5:16,18**).

Mwitikio wa Mwanadamu

Kwa sababu ya dhambi wanadamu wote wanahitaji wokovu ambao Kristo anauhitaji. Nguvu ya dhambi inaonyeshwa katika Biblia kwamba hata Israel; I ambao ni taifa teule la Mungu waliishi kwa kutawaliwa na dhambi ikionesa kwamba sheria ya Mungu iliyoandikwa kwa nguvu zake haiwezi kumwokoa mwanadamu kutoka katika vifungo vyta dhambi. Paulo anakazia kwamba dhambi na kifo ni ndugu wanaowatawala wanadamu wote ili kwamba waone uhitaji wa ukombozi wa Kristo (**Tazama Rum, 1:18-3:20; 5:1-7:25**). Dhambi haimaanishi tu

Sheria za Mungu bali ni uwakilisho binafsi wa kumwasi Mungu na ukuu wake (**1 Yohana 3:4**). Asili ya dhambi ni sanamu, ambapo watu wanakataa kushukuru kwa Mungu na kuamua kuabudu miungu badala ya kumwabudu Muumbaji (**Rum. 1:18-25**).

Lakini dhambi siyo neno la Mwisheso kwa kuwa Kristo alikuja kuwaokoa watenda dhambi na kwahiyio anaonesha rehema na neema ya Mungu. Kitu cha msingi Mungu anachotaka ni Imani na toba. Wito wa imani na toba ni dhahiri katika huduma ya Yohana Mbatizaji. Katika tangazo la Yesu la ufalme (**Marko 1:15**). Katika Hotuba katika Matendo, katika nyaraka za Paulo na katika Aganop lote jipya. Wale wanaotamani kuwa katioka jamii mpya ya Yesu (kanisa) na kuwa sehemu ya ufalme wa Mungu (Mungu atawale katika mioyo yao na maisha yao) wanapaswa kuacha miungu, wakane ibada hizo za kibinafsi na waache maovu na warudi kwa Yesu kama Bwana na Mkuu. Wito wa toba ni unamanisha kuacha dhambi na kuweka imani binafsi ya kuatumainia kazi za Yesu peke yake na waondoe mawazo ya kwamba wao wanaweza kujikoa. Watu wote kila mahali wameshavunja mapenzi ya Mungu na hivyo wanapaswa kutafuta kazi ya wokovu ya Kristo kwa ajili ya kukombolewa kutoka katika ghadhabu ya Mungu. Kiukweli kabisa Agano lote jipya linaweza kueleweka kwamba ni wito wa kukombolewa na imani. (**cf. Waebrania 1:10**)-. Hata wale ambao tayari ni waumini wanapaswa kuwa katika imani na toba kwani maisha yanaisha kwani hii ndiyo alama ya mwanafunzi wa Yesu. Waandishi wa Agano jipya waliwahimiza wasomaji wao wadumu katika imani hadi mwisheso na wakatahadharishwa na kila aina ya hatali itakayowaqpelekea kumkataa Yesu. Waumini wa Kweli wanashuhudia kwamba wokovu ni wa Bwana na kwamba Yesu Kristo ni yeze Yule aliywakomboa kutoka katika ghadhabu ijayo.

Watu wa Mungu

Ahadi ya Mungu iokoayo imeshaanza kutimia katika jamii mpya, kanisa la Yesu Kristo. Kanisa linajumuisha waumini katika Yesu Kristo wayahudi na wayunani kwa sabau sheria katika agano la kaleiliwatenganisha wayahudi na watu wa mataifa (mfano, Kutahiriwa, Sheria za usafi, sherehe maalumu na siku kuu) hazina nguvu tena. Kanisa ni hekalu jipya la Mungu linalokaliwa na Roho Mtakatifu na limeitwa kuishi maisha matakatifu ya Injili kwa kuonesha alama kuu za mwanafunzi wa Yesu Kristo; kupendana (**Yohana 13:34-35**).

Kanisa linatambua hata hivyo litadumu katika hali ya umilele. Linasubiri kurudi kwa Bwana Yesu Kristo na hukumu ya makusudi yote ya Mungu. Katika kipindi hiki cha hapa duniani kanisa linapaswa kuishi kwa utakatifu maana lenyewe ni bibi harusi na mtangazaji wa wa habari njema za wokovu hadi mwisheso wa nchi ili kwamba wale wengine wanaoishi katika giza ya dhambi waweze kuhamishwa kutoka katika ufalme wa shetani na kuingia katika ufalme wa Bwana. Kanisa linatazamia siku ambayo litaona ya Bwana, uso kwa uso na kumwabudu Yesu Kristo milele. Uumbaji mpya ndiyo itakuwa hali halisi. Vitu vyote vitakuwa vipyta na Bwana atatukuzwa milele kwa ajili ya upendo na Rehema zake na Neema—Kwa maana Agano jipya ni kwa ajili ya Kumtukuza na Kumsifu Mungu.

Ni kwa jinsi Gani Agano Jipyä linanukuu na kutafasiri Agano la kale

“Matumizi” ya Aina mbalimbali

Tunaanza kwa kuangalia njia mbalimbali jinsi ambavyo waandishi wa Agano jipyä wamelitazama Agano la kale. Wamerinukuu kama ([Mat. 1:23](#) miji [Isa. 7:14](#)); wameligusia kama ([Yoh 1:1–5](#) wamegusia kama [Mwanza 1](#)); wanawenza kutumia misamiati ya Agano la kale kama ilivyokuwa imeamuriwa katika Agano la kale (e.g., “haki ya Mungu”); wanawenza kulitumia kulingana na mtazamo wa Agano la kale (maka vile Mungu mmoja na uumbaji); na wanawezz kurejea katika hadithi tata za Agano la kale ambazo niza msingi (mfano., [Rom. 1:1–6](#)).

Mtazamo wa pili hakuna maelezo ya aina moja yanayoweza kukamilisha mifano yote ya Agano jipyä kwa Agano la Kale. Kwa mfano mwandishi anaweza kuwa amekusudia kueleza kifungu Fulani cha Agano la kale kutokana na kile alichokusudia kukionesha. Anaweza kueleza wazo Fulani kutoka katika tukio Fulani (e.g., [Mark 2:25–26](#)), na anaweza kutafuta uwiano kati ya watu wake na wale wa zamani (e.g., [1 Kor. 10:6–11](#)). Anaweza kueleza jinsi ambayo wakristo wa mataifa wanavyoweza kuzirithi Baraka za Israeli ([1 Pet. 2:9–10](#)), Au anaweza kuwa anataka kueleza kwa nini Wakristo hawapaswi kutunza mambo ya yaliyopita katika Agano la Kale (e.g., [Marko 7:19](#); [Ef. 2:19](#)). Paulo anaueleza wito wake kwa mazingira yanayotukumbusha katika utumishi wa Bwana ([Gal. 1:15](#) kuamsha [Isa. 49:1](#)): kwa kuwa utumishi w Isaya ni sura ya Masihi (kama Pauol alivyojua, cf. [Mdo 13:47](#); [Rom. 10:16; 15:21](#)), ni vyema kuona kwamba Paulo anaupenda wito wake kwa namna Fulani kama vile Yule mtumishi zaidi ya kuona ilivyokuwa akijiita Mtumishi.

Kwa namna ya maandishi

Sehemu hii inautata kidogo. Kama sheria ya jumla, waandishi wa Agano jipyä huliweka Agano la kale katika mfumo wa Kiyunani ambao unaitwa Septuagint ambayo ndiyo inapatiaka leo (Tazama [The Septuagint](#)). Kuna sehemu nyingi ambapo waandhishi wa Agano jipyä hutofautiana katika swala la Septuagint: kwa kuwa waandishi wamekuwa wakirekebisha baadhi ya maandishi ili kuoanisha na maana ya kile walichokikusudia kulingana na kusudi alilolipanga kulifikisha utakuta kwamba hawezo kuitazama sana Septuagint. Atatumia kiyunani na kuikwepa maana kidogo iliyokuwa imekusudiwa katika Agano la kale.

Mtazamo wa Agano jipyä katika matumizi ya Agano la kale

Maandishi mengi ya Agano jipyä yanaangalia sana kile wakristo wanachofanya kwa mtazamo wa Agano la kale. [Warumi 1:1–6](#), ambapo Paulo anaieleza “Injili ya Mungu” ilitabiliwa hapo kale kupidia vinywa vya manabii katika maandiko matakatifu.” Sehemu inayofuata inamweleza Yesu anaingia katika Enzi ya Daudi kwa njia ya kufufuka, na utume wa Paulo kama utendaji wa Kristo katika kuleta utii wa Imani kwa ajili ya jina lake kwa ajili ya mataifa yote”: Palo anaieleza tukio la ushindi wa Yesu na usuhuda wa Wakristo wa Kwanza ni matokeo ya kile kilichoelezwa katika Agano la kale. Hii ni aina ya usomaji ambao Agano la kale unahitaji. Baadae tena katika Barua ileile ([Rum. 15:4](#)), Paulo anasema, “Kwa kuwa yote yaliyotangulia kuandikwa (Agano la Kale) ili kutufundisha sisi(Wakristo) ili kwa saburi na faraja ya maandiko tupate kuwa na

Amani anaendelea katika Mstari wa ([.9–13](#)) ili kuonesha maandiko ya Agano la kale juu ya makosa yanayoweza kutokea ambapo mataifa watapokea Nuru na kuungana na waaminifu wa Israeli. Kongamano hili mchanganyiko la Wayahudi na watu wa mataifa ni utimilifu wa tumaini hilo.

Katika [1 Kor 10:1](#), Paulo anagusia matukio ya Agano la kale anasema “Baba zetu” walikabiliana nayo. Kanisa katika Korintho hata hivyo nalo lilikuwa na watu wa mataifa waliokuwa wameongoka; Hivyo hiyo inamaanisha kwamba Paulo alikuwa anawahudumia hawa wakristo wa mataifa na kuwaambia kwamba wamejumuishwa.” ([Rum. 11:17ff.](#)) Kwenye mti wa mizeituni (watu wa Mungu, cf. [Yer. 11:16](#)), Kila hatua na warithi wa habari kama Wakristo wa kiyahudi walivyo. Baada ya kuorozesha njia ambazo Mungu alizitumia kuwaadhibu watu wasio waaminifu kati ya watu wale wa kale ([1 Kor. 10:6–10](#)), Paulo anaeleza kwamba “Basi mambo hayo yaliwapata kwa njia ya mifano yakaandikwa ili kutuonya sisi tuliofikiliwa na miisho ya zamani.” Mungu anategemea wale wanaosema kuwa ni Wakristo wawe na uhakika kwamba Imani yao ni kweli kama vile alivyofanya kwa wale watu wa kale.

[Waebrania 11](#) inaonesha waaminifu wengi katika Agano la kale mbele za wasikilizaji wake (Yumkini ni Wayahudi Wakristo) kuwaelza kwamba wanapaswa kuvumilia katika imani kama vile wale watakatifu wa kwanza.

Katika [Luka 24:25–27, 44–47](#), YESU “alitafasiri kwa [Wanafunzi wake] katika maandiko yote ya Agano la kale yote yaliyoandikwa yanamuhusu yeye. Baadhi ya wakristo wanaotafasiri walielewa kwamba ni rahisi kuona katika kila andiko la Agano la kale “utangulizi wa Yesu” na hata kazi zake. Hata hivyo wakarimani wengine wanasema inatosha na kutambua kwamba kuna baadhi ya mistari katika Agano la kale inayoeleza kazi za Masihi na kwamba Historia yote ya Agano la kale inaeleza habari za Yesu , ushindi katika mateso yake nainaweka dhahiri juu ya watu wa mataifa kuipokea nuru ya Mungu ([Luka 24:47](#), “mataifa yote”).

Orodha Muhimu ya matumizi ya Agano Jipyka Katika Agano Kale

Mitume walipokuwa wakilitumia Agano la kale katika Agano jipyka walikuwa wakinukuu maandiko ya mwanzo kabisa kwa kuangalia yale matendo yaliyofanywa katika Agano la kale. Kwa mfano waandishi wa Agano la kale waKigusia sura za kwanza kabisa na kuzielezea (e.g., [Zaburi 8 na 104](#) tumia [Mwanzo 1–2](#)); wangegusia sura za awali na kutoa tofauti ndogondogo (kama [Zaburi. 72:17](#) inaeleza jumla [Mwanzo. 22:18](#) na kuziweka kwa nyumba ya Daudi peke yake). Walizitambua ahadi (Mfano. [Dan. 9:2](#) inapatikana katika [Yer. 25:12](#) ahadi ya tawala wa babeli na tawala wake mrefu). Waliona mambo ya Mungu yalivyorudiwa (Mfano. Mfano Zaburi nyingi zinagusia [Kutoka. 34:6–7](#) kama njia ya Mungu kushghulika na watu wake). Walichukua maandiko kutoka katika vizazi vya kwanza na kuzitumia katika mazingira mapya (e.g., [Neh. 8:14–17](#) inaonekana kutenda sheria za [Mambo ya walawi. 23:39–42](#) kwa kuhusiana na [Kumbukumbu la Torati. 16:13–15](#); cf. na mistari maaru ya [Yer. 22:24–27](#) na [Hag. 2:23](#)).

Waaandishi wa Agano jipyka pia wanatumia matumizi haya kutokana na kuona kwamba Wakristo ni Warithi wahistoria ya Israeli; Manatumia matumizi mengine pia kwa uona kwamba ufufuko wa Yesu umetumika katika enzi mpya, kipindi cha masihi—“Siku ya mwisho ilitabiliwa mwanzo kabisa na manabii. Waandishi hawa walijiona kwamba wao ni waandishi walioruhusiwa

na Mungu katika kipindi hiki cha agano jipywa ambacho Mungu amekifngua kwa ajili ya historia ya watu wake.

Wakristo wamisionari wa kwanza walienda katika masinagogi kuthibitisha kwamba Yesu ni Kristo (cf. [Mdo 17:1–3; 18:26–28](#)). Hii inaonesha kwamba walitegemea na kutumia mijadala ya hadharani kutoka katika maandiko yenewe na si tu katika mitazamo binafsi ya kibinadamu — Vinginevyo ingekuwa si haki kumwaibisha mtu kwa kitu ambacho hakikuwa ni kweli. Luka anawasifu wayahudi wa Beroya ambao waliyachunguza maandiko ya Agano la kale kuona kama ile Paulo na sila wanachokisema kilikuwa ni kweli ([Mdo 17:11](#)): hii inaonesha kwamba Agano jipywa linashabiana na matumizi ya Agano la kale na si kwamba linajitegemea lenyewe tu kwa mtazamo wake.

Kwa kuyachanganua matumizi haya maswali ya msingi ni:

- Ni kitu gani katika Agano kale kilichowawezesha waandishi wa Agano jipywa kuandika kama alivyotaka?
- Nini msimamo wa wandishi wa Agano jipywa kutokana na Maana halisi ya gano la kale?
- Nini lengo la kuzuia kwa waandishi wa Agano jipywa wanapajaribu kupata kutokana na habari za Agano la kale?
- Katika njia zippi waandishi wa Agano jipywa wanatofautiana katika kanuni za ufasiri zilizo kwa wafasiri wengine waliokuja kutoka katika kipindi kimoja na hasa waandishi wa hekalu la kiyahudi ambao hawakuwa ni Wakristo?

Mpangilio katika orodha hii umekusudiwa kuwa mpana na wakufikirika; hakuna mbadala katika sura na sura.

Ahadi na utimilifu. Katika njia nyingi waandishi wa Agano jipywa walifahamu Agano la kale kwa kuelewa ahadi ambazo zilikuwa zimeahidiwa na kuyatambua matukio maalumu kama utimilifu wa ahadi. Kwa mfano, [Mathayo 12:17–21](#) alielewa huduma ya Bwana katika [Isaya 42:1–3](#) Kama masihi, kuwa Kristo ndiye mtu aliye ahidiwa. Vivyo hivyo, Katika [Warumi 15:12](#) Paulo anaona kusambaa kwa imani ya Kikristo kati ya mataifa kama utimilifu wa matarajio ya [Isaya 11:1–10](#).

Kielelezo na utimilifu. Hii mara zote huitwa “Uainishi,” inahusika na jinsi ambavyo mpangilio umeonekana katika Agano la kale ili kuwasaidia wakristo kuelewa mazingira yao ya sasa katika Kristo.nKwa mfano nmna kondoo alivyobeba dhambi au dhambi ilivyokuwa ikitolewa kwa kumchukua mnyama asiye na ila hii iliwalishia jinsi Yesu kama dhabihu alivyo wafaa waumini (Tazama [Isaya. 53:7](#), Historia [Yohana 1:29](#)).

Ulinganifu na matumizi. Wakati mwengine waandishi wa Agano jipywa walioanisha matukio ya kale na ya sasa na kuchukua kanuni za Agano la kale na kuzileta katika kipindi cha sasa. Mifano ya [Marko 2:25–26](#) na [1 Kor 10:6–10](#) zimekwisha kutajwa.

Mwandishi anapotumia ulinganisfu hatoi ufasiri wa kusudi la awali katika Agano la kale lakini ieleweki kwamba Uwianishaji unaheshimu sana kusudi la kwanza. Kwa mfano, katika [Mat 21:42](#), Yesu anatumia [Zaburi 118:22–23](#) (Kuhusu “Jiwe walilolikataa waashi”) kueleza jinsi ambavyo wayahudi walivyomkataa. Japo wengi wanaelewa kwamba huu ni unabii wa masihi

Pointi anayoieleza Yesu ni kwamba viongozi wa wayahudi waliomkataa ni (kwa kulinganisha) wamepotoka na kuanguka ([Mat. 21:41](#)) Kama nguvu kubwa ya Ulimwengu inayoonekama kuwa ndogo kama Israeli (soma maelezo [Zaburi. 118:22–23](#)).

Kuelewa matmizi ya uoanishaji kwa namna hii itatusaidia tunapokabiliana na ugumu katika sura za Agano jipya. Katika [1 Kor 9:9](#) na [1 Tim 5:18](#), Paulo anaeleza mambo ya sheria za Agano la kale ([Kumb. 25:4](#)) kuhusu kutokumfunga ng'ombe na anatumia kama kuhesabiwa haki kwa kuwalipa walio katika huduma. Agano la kale linashughulika na wanyama wanaofanya kazi lakini mtazamo wa Paulo ni “kwa jinsi gani tunapaswa kuwajali wale wanaotuhudumia kwa Neno” ni kama mjadala. Katika [Wagalatia 4:21–31](#), Paulo anatengeneza “Mfarakano” kutoka kwa saran a Hajiri katika kitabu cha Mwanza ili kuwashawishi wasomaji kuwakataa walimu wa uongo. Hakuna sababau ya kufikiri kwamba anatengeneza maana nyingine zaidi ya ile ya kitabu cha Mwanzo na wala hajadharau maana ya Agano la kale; bali anawapenda wale wanaofuata jumbe zake kwa kuwaona kuwa ni “Watoto wa Ahadi” (wamezaliwa kwa Roho na kuwa kama Isaka), na wale wanaofuata walimu wa uongo kuwa wamezaliwa kwa mwili” (Yaani., Ishmaeli).

Muendelezo wa mambo yajayo. Wazo la “mambo yajayo” katika Agano la kale inashughulika na mambo yajayo kipindi ambacho Masihi atashughulikia watu wake kwa kuleta Nuru kwa mataifa; nafasi ya Agano jipya ni kwamba kipindi hiki kimeanza kipindi cha kufufuka na kupaa kwa Yesu. Hizi ni sura tofauti zinazodhahirisha hadithi ya kazi ya Mungu katika ulimwengu lakini zinakataa muendelezo kwa sababu ni mungu yuleyule anaye waokoa watu kwa njia ile ile (cf. [Rum. 4:1–8](#)), anayewaokowa mataifa waaminio katika mti wa mizeituni ya watu wake ([Rum. 11:17](#)), na anayeirejesha sura ya Mungu ndani yao. Hivyo waumini wayahudi na watakatifu wanashiriki Baraka za Israeli (Mfano., [1 Pet. 2:9–10](#), tukirejea [Kut. 19:5–6](#) na sura zingine). Kwa hiyo amri kumi zinatekeleza maadili kwa Wakristo ([Rum. 13:8–10](#)). “haki ya Mngu” ile ile— utauwa wa mungu na uaminifu wa kutunza ahadi zake—Sherehe za Agano la kale zinarejea kwa Mngu katika kumleta Kristo ([Rum. 1:17](#)).

Hitimisho la mambo yajayo. Kundi inahusiana na iliyopita na inarejea katika katika mabadiliko ya ukombozi. Kwa mfano, waaminifu wa Mungu hawana sababau ya kufuata sheria ya vyakula ambavyo kusudilake ilikuwa ni kuwatofautisha Waisraeli na wat wa mataifa ([Walawi. 20:24–26](#); cf. [Mdo 10:9–23](#)). Mitazamo mingine ya Agano la Sinai haina nguvu kwa watu wa Mungu kama vile matoleo ya dhabihu na hata serikali ya ukasisi iliyowekwa Yerusalemu.

Maendeleo. [Zaburi 72:17](#) haibadili ahadi ya Baraka kwa mataifa ya [Mwanzo 22:18](#) bali inaendeleza hali ya kuboresha mtazamo. Kwa njia ile ile, [Isaya 52:13–53:12](#) wengi wameeleza maisha ya Yesu kama maisha ya kukataliwa na kunyanyaswa ikifuatiwa wa Uthibitisho na Ushindi. [Isaya 53:10](#) inaeleza, kifo si mwisho wa huduma ya masihi na ufufuo haujaelezwa pale ; (japo kwa sasa inaonesha muingiliano). [1 Kor 15:3–4](#) inasema, “Kristo alikuwa kwa ajili ya dhambi zetu kama yanenavyo maandiko” (Yumkini inarejea [Isa. 53:10](#)), na “akafufuka siku ya tatu kama yanenavyo maandiko” (inaendelezaa, au inachanganua, [Isaya. 53:10](#)). Mtazamo uliopo katika mifano hii ni kwamba habari inashabiana, na Mungu anaweza kuweka mambo mapya na mitazamo mipya kwenye mlolongo(katika swala la [Zaburi. 72:17](#), kwa kutoa katika miungu kwa kuweka Agano la Daudi; katika swala la [1 Kor. 15:4](#), kwa kumfufua Yesu kutoka wafu).

“Uelewa kamili.” Wakristo wamelitumia neno la Kilatini *sensus plenior* (“Uelewa kamili”) kwa namna ambayo Agano jipya linakuwa na maana kubwa zaidi ya ile maana iliyokusudiwa katika Agano la kale. Kuna kila sababu ya kuruhusu aina hiyo ya mazingira pale mtu anapowaza kwamba Mungu hupanga matkio na ndiye aliyevuvia maandiko na watafasiri wake. Hata hivyo ni vyema kuwa makini: kwa mitazamo mingi swala la osensus plenior limepotosha uelewa wa matumizi ya sura mabalimbali za Agano la kale (Tazama mijadala ya [Mat. 2:15/Hos. 11:1](#) chini; tazama [Zaburi. 16:9–11](#)). Kuna mifano ambayo katika agano jipya imefanyika: e.g., katika [Yohana 1:1–5](#), Yohana anaelezea “Neno” kama nafsi ya Mungu yenye nguvu katika uumbaji anarejea katika [Mwanzo 1:1–2:3](#) kwa kuona kitu Fulani ambacho Musa hakukisema. Hata hivyo [Zaburi 33:4–9](#) inaeleza hii haiku nje ya mwanzo (Tazama [Mwanzo. 1:26](#) Kwa ajili ya Utatu). Mtu anaweza kusema kwamba Musa anasema kama angeletewa injili ya Yohana, “sawa sikuwahi kufikiri namna hiyo na sasa unakuja unasema hivyo naanza kuona ulikoipata nanimeipenda”: ile ni kusema kwamba hakudhani maana ya kwanza imeharibiwa. Ni nyembambe hatahivyo kuwakilisha *sensus plenior* inayoleta maana halisi ya mwanzo.

[Mat 2:15](#) imechukuliwa kama jambo la *sensus plenior* kwa sababu ya inasema ipindi familia takatifu ilipokaa Misri (baadae ikarudi Palestina) hii ilikuwa ni kutimiza maneno ya [Hosea 11:1](#), “Kutoka misri nalimwita mwanangu.” Je Mathayo ameona maana ya masihi katika Hosea ambayo hakuna mtu amewahi kuiona? Yamkini hapana: ni dhahiri kwamba mathayo aliona katika hoseamhitasari wa mambo ya Kutoka yaliyokuwa na neno “Mwana.” (manabii wengi wanaihitimisha kutoka kwamba ilikuwa ni njia ya waisraeli kuwajibika kwa Bwana: cf. [Amosi 3:1–2](#).) Mja ya kusudi la Mathayo ni kwamba Yesu alijonesha mwenyewe kuwa ni masihi wa kweli (Ududi unaowakilisha Israeli) kwamba Israeli waliitwa kuwa hivyo na kutenda kwa uaminifu (Kwa kulinganisha na Israeli). Katika wazo la Mwana wa Mungu wazo kuu la Mathayo angalia rejea katika [Zaburi 2:7](#). Kwa hiyo Yesu alitimiza miunganikano yote ya kitabu cha kutoka ikiwa na maana ya kwamba ye ye ndiye msemwaji na mkamilishaji.

Uungu wa Kristo. Waandishi wa Agano jipya hulitumia Agano la kale kuwa ni la Yesu ambalo hapo awali lilihusika na Yahwe Mungu wa Israeli. Mfano, [Waebrania 1:10–12](#) Inamwelezea Yesu kwa kutumia [Zaburi 102:25–27](#), inayohusu umilele wa Mungu. Hii si kwasababu kwamba zaburi ni za Masihi lakini ni kwasababu waandishi wa Agano jipya Yesu kristo ni Yahwe aliyeavaa mwili (cf. [Yohana 1:1–14](#)). Kwa hiyo agano jipya hutumia maneno kwa maana ileile ya asili—yanamwelezea Bwana—na kutambua kwamba maelezo yake yanamuhusu Yesu na kwamba si mdogo kuliko Mungu baba.

Katika mambo yote haya Waandishi ya agano jipya wanajiona kwamba ni warithi na wafasiri sahihi wa Agano la kale.


Utatu

Mafundisho ya Biblia juu ya Utatu yamelalia katika thibitisho muhimu wa aina nne:

1. Kuna mmoja na Mungu mmoja wa kweli aliye hai.
2. Mungu huyu wa milele yuko katika nafsi tatu—Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho mtakatifu.
3. Nafsi hizi tatu zinafanana katika sifa na kila moja ina sifa ya uungu.
4. Kwa kuwa kila nafsi ni Mungu kamili nafsi hizi hazifanani.

Tofauti baina ya baba, Mwana na Roho Mtakatifu zinaonekana kulingana na jinsi zinavyoshabiana na katika jukumu ambalo kila nafsi inafanya katika kusudi lao moja.

Umoja wa asili na utofauti wa nafsi hizi za tatu unelezwa vizuri katika mchoro huu.



Mungu ni Mungu mmoja: Monotheism

Hakuna cha ziada katika theologia ya Biblia zaidi ya monotheism (Imani ya Biblia kwamba kuna Mungu mmoja tu): “Sikia, Ee Israeli: Bwana Mungu wetu Bwana ndiye mmoja” ([Kumb. 6:4](#)). Mstari huu unajulikana kama [Shema](#) kiebrania (tangu mwanzoni mwa tendo wa mstari huu inamaanisha “Sikia” au “Sikiliza”), ni moja ya mistari ya msingi na inayojulikana katika Agano la kale. Mungu anakataa polytheism (imani za Miungu mingi) na anataka ibaada ya kipekee: “Mimi ni Bwana wala hakuna mwingine zaidi yangu mimi hapa Mungu” ([Isaya. 45:5](#); cf. [Kumb. 4:35, 39](#); [1 Wafalme 8:60](#); [Isa. 40:18; 46:9](#)). Agano jipya linathibitisha Uungu wa Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, kama tutakavyoona, lakini haiondoki kutoka katika Monotheism ya Agano la kale kama tutakavyoona, haitoki katika monotheism ([Yohana 17:3](#); [1 Kor. 8:4–6](#); [1 Tim. 2:5](#));

[Yak 2:19](#)). Yesu ananukuu [*Shema*](#) katika mjadala na viongozi wa wayahudi([Mark 12:29](#)), na Paulo anaendelea kufundisha kwamba kuna Mungu mmoja akitambua Yesu ni mwanadamu mpatanishi kati ya Mungu na mwanadamu ([1 Tim. 2:5](#)).

Mahusiano ya Monotheism

Kwa kuwa kuna Mungu mmoja, sanamu ya aina yoyote ni uovu, ujinga, si sahihi na ni hatari. Ibada ya kuabudu”miungu” mingine ni kuiba utukufu anaostahili Mungu wa kweli katika ibada. Miungu yaweza kuwa katika namna mbalimbali. Miungu si ile iliyofinyangwa na watu tu bali ni chochote kile kinacholiningishwa na Mungu ili kuchukua nafasi ya ukuhani. Kulingana na Yesu mali inaweza ikawa ni miungu: “Huwezi kutumikia mali na Mungu” ([Mathayo. 6:24](#)). Ulafi, Uroho, na uchafu vyawenza kuwa ni ishara ya miungu ([Waefeso. 5:5](#); [Kol. 3:5](#)). Sanamu ni upuuzi, uongo na hatari—na inaweza kuingiza hata shighuli za kipepo ([1 Kor. 10:19–20](#)).

Kwa kuwa kuna Mungu mmoja yeye peke yake ndiye anapaswa kuwa ni nia mama ya waaminio. Yeye pekee anahitaji kuabutiwa na utii. Amri kuu inayofuatana na [*Shema*](#) ni mahusiano mazuri ya monotheism: “Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote na kwa nguvu zako zote” ([Kumb. 6:5](#)). Mungu mmoja wa kweli anastahili yote tuliyonayo na tulivyo. Anastahili upendo wa dhati ndani ya moyo kwa sababu hakuna cha kulinganishwa nae.

Mungu ni wa nafsi Tatu: Umoja wa utatu wa Mungu

Kama asili ya Mungu ilivyooneshwani katika, maandiko, huyu Mungu mmoja ameonekana kuwa katika nafsi tatu. Hizi nafsi tatu zina sifa moja za asili lakini ni tofauti katika majukumu na mahusiano. Kanuni iliyo katika utatu wa moyo wa tatu wa Mungu ni *Umoja na utofauti*, sifa hizi wala hazichanganyani. Chochote cha Muhimu na kweli kwa Mungu ni kweli kwa Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Wako sawa katika asili lakini tofauti katika utendaji.

Mapokeo ya utatu yametambulikana kabisa katika Agano jipya, ambapo Mungu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu wameonekana wakikamilisha ukombozi. Lakini wakati Agano jipya linatupa picha safi ya Utatu kuna vidokezo katika Agano la kale ambavyo vinaendela kuwepo na vitakuja. Mwanzoni mwa Biblia, Roho wa Mungu “likuwa katulia katika uso wa maji” wakati wa uumbaji ([Mwanzo. 1:2](#)) na sehemu zingine kaelezwa kama mwanadamu, akiwa na sifa za Mungu, lakini tofauti na Yahweh ([Isaya. 48:16; 61:1; 63:10](#)). Watafasiri wengine wanadhani kwamba wingi wa Mungu unaonekana katika neno la kiebrania linalomweleza Mungu, *Elohim*, ambalo ni wingi (japo kuna wengine wanapingana kwamba hii ni muhimu; neno limetumika kwa tendo lenye maana ya umoja katika Agano la kale na wengi wanakubaliana). Katika nyongeza matumizi ya wingi wa vijina Mungu anapojisema mwenyewe hujitamuka katika nafsi zote Tatu: “Mngu akasema, ‘na tumfanye mtu kwa mfano wetu’” ([Mwanzo. 1:26](#); cf. [Mwanzo. 3:22; 11:7](#); [Isaya. 6:8](#)). Wingi wa Mungu pia unaonekana kuoneshwani wakati malaika wa Bwana alipoonekana katika Agano la kale kama mwakilishi wa Yahweh, na wakati mwingine sifa za malaika hazikutofautiana kabisa na sifa za Mungu mwenyewe (cf. [Mwanzo. 16:7, 10–11, 13; 18:1–33](#); [Kutoka. 3:1–4:31; 32:20–22](#); [Hesabu. 22:35, 38](#); [Waamuzi. 2:1–2; 6:11–18](#)). Pia kuna sura katika Agano la kale zinazoita nafsi mbili Mungu au Bwana

“Kiti chako cha Enzi Mungu ni cha milele na milele, fimbo ya ufalme wako ni fimbo ya adili, umeipenda haki umeichukia dhuluma, kwa hiyo Mungu wako, amekupaka mafuta mafuta ya furaha kuliko wenzako” ([Zaburi. 45:6–7](#)). Daudi ansema, “Neno la Bwana kwa Bwana wangu, uketi mkono wangu wa kuume, hata niwafanyapo adui zako kuwa chini ya miguu yako”” ([Zaburi. 110:1](#)). Mungu aliyejukweka juu ya wenzio ([Zaburi. 45:6](#)) na Bwana wa [Zaburi 110:1](#) wanatambuliwa kama Kristo katika Agano jipyä ([Waebrania. 1:8, 13](#)). Kristo mwenyewe anajisema [Zaburi 110:1](#) mwenyewe ([Mathayo. 22:41–46](#)). Sura zingine hutoa maelezo ya kiungu katika sura za Kristo tofauti kutoka kwa Yahweh ([Methali. 8:22–31; 30:4](#); [Daniel. 7:13–14](#)).

Agano la kale linautazama wingi wa Mungu na kuuona katika picha kamili ya Utatu katika Agano jipyä ambapo uungu na utofauti wa naffsi ya Baba, Mwana na Roho mtakatifu hutenda kazi pamoja katika umoja na usawa kamili (katika ungu wa Kristo na Roho mtakatifu, ([Nafsi ya Kristo](#)). Nafikiri picha safi ya utofauti huu ni ubatizo wa Yesu, ambapo mwana anapakwa mafuta kwa ajili ya hduma yake na roho mtakatifu anashuka kama njiwa na baba anasema kutoka mbinguni kwamba, “Huyu ni mwanangu mpendwa niliyependezwa naye” ([Math. 3:13–17](#)). Nafsi zote za utatu zipo na zinafanya kitu tofauti tofauti.

Waandishi wa Agano jipyä wanafanya wimbo wa utatu wanapoandika juu ya kazi ya Mungu. Maombi ya Baraka na maelezo ya Karama ndani ya mwili wa Kristo ni utatu katika asili: “Neema ya Bwana wetu Yesu kristo, na upendo wa Mungu na ushirika wa Roho Mtakatifu ukae nanyi” ([2 Kor. 13:14](#)); “Basi panatofauti ya karama bali Roho ni yeze Yule, tena panatofauti ya huduma na Bwana ni yeze Yule, kisha kunatofauti za kutenda kazi bali Mungu ni yeze Yule azitendae kazi zote katika wote” ([1 Kor. 12:4–6](#)). Nafsi za utatu zimeungwanishwa katika kanuni ya ubatizo [Mathayo 28:19–20](#), “Mkiwabatiza katika (ndani ya) jina la Baba na la Mwana na la Roho mtakatifu.” Kuna sura nyingi zinazoonesha Utatu, au angalau wingi asili ya Mungu (e.g., [Yohana 14:16, 26; 16:13–15; 20:21–22](#); [Rum. 8:9; 15:16, 30](#); [2 Kor. 1:21–22](#); [Gal. 4:4–6](#); [Waef. 2:18; 4:4–6](#); [1 Pet. 1:1–2](#); [1 Yohana 4:2, 13–14](#); [Yuda 20–21](#)).

Utofauti katika majukumu pia unaonekana katika shhuda za biblia kuhusiana na uhusiano wa Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Usawa wa maandiko ni kwamba Baba hupanga, huelekeza, na kuagiza; mwana alitumwa na Baba na atawajibika katika mamlaka ya Baba na mtii katika mapenzi ya Baba; na wote wawili Baba na Mwana huelekeza na kumuagiza roho Mtakatifu anayetimiza mapenzi ya wote wawili. Sasa katika hili tunaweza kuona usawa kinafsi nahata sifa. Baba amefanya kwa njia ya Mwana ([Yohana 1:3](#); [1 Kor. 8:6](#); [Kol. 1:16](#); [Waebrania. 1:2](#)), na Baba alipanga ukombozi na kumtuma Mwana duniani ([Yohana 3:16](#); [Rum. 8:29](#); [Gal. 4:4](#); [Efeso. 1:3–5](#)). Mwana alimtii baba na akakamilisha ukombozi kwa ajili yetu ([Yohana 4:34; 5:19; 6:38](#); [Waebrania. 10:5–7](#); cf. [Mathayo. 26:64](#); [Mdo2:33](#); [1 Kor. 15:28](#); [Waeb. 1:3](#)). Baba hakuja kufa kwa ajili ya dhambi zetu wala roho mtakatifu hakufa kwa ajili ya dhmabi zetu bali hili lilikuwa ni jukumu la Mwana. Baba na Mwana walimtuma Roho mtakatifu katika njia mpya ya pentekoste ([John 14:26; 15:26; 16:7](#)). Mahusiano haya yamekuwepo milele ([Rum. 8:29](#); [Efeso. 1:4](#); [Ufunuo. 13:8](#)), na wanajenga usawa endelevu na utofauti ktika mahusiano tofauti ya mwanadamu.

Ndani ya Mungu kuna vyote viwili umoja na utofauti: Umoja bila kufanana, tofauti bila migawanyiko. Kanisa la kwanza liliuona uwiano wa utatu huu wazi kabisa. Kwa mfano, tamko la the Athanasi (c. a.d. 500) linasema:

“Tunamwabudu Mungu mmoja aliye katika utatu na utatu katika umoja; tunamtofautisha katika nafsi, lakini hatumgawi..... Nafsi zote tatu ni za milele na zinafanana ili kwamba Tunauabudu umoja wote katika utatu na utatu katika umoja.”

Umoja huu na utofauti huu uko katika siri kubwa ya utatu. Umoja bila utofauti ni fumbo lililo katika akili endelevu lakini ulimwengu unaonesha tofauti mabalimbali za kanuni hii ya umoja na utofauti.

Mahusiano halisi ya Utatu

1. Mafundisho ya utatu yanafanya mafunuo yasiyo na mwisho ya Mungu mweza kama alivyojulikana katika: “Hakuna mtu aliye mwona Mungu; Mungu Mwana Pekee, aliye katika kifua cha baba huyu ndiye aliyemfunua” ([Yohana 1:18](#)). Hakuna mtu anyeweza kumwona Mungu na akaishi ([Kutoka. 33:20](#); [1 Tim. 6:16](#)), lakini Mungu mwana alifanya udhihirisho wa Mungu katika mwili.
2. Utatu unadhihirisha mateso. Ukombozi wa mwanadamu mwenye dhambi unakamilishwa kwa njia ya tofauti na umoja wa uungu: “Basi si zaidi damu yake Kristoambaye kamba kwa Roho wa milele alijitoa nafsi yake kwa Mungukuwa sadaka isiyo na mawaa itawasafisha dhamiri zenu na matendo machafu mpate kumwabudu Mungu aliye hai” ([Waembrania. 9:14](#)).
3. Kwa sababu Mungu ni utatu ye ye ni wa milele na mahusiano katika ye ye katika utegemezi wote tangu uumbaji. Mungu hajawahi kupungukiwa wala kutumikiwa kwa mikono ya wanadamu au kuwa muhitaji ye ye ndiye humpatia mwanadamu uzima, pumzi na kila kitu” ([Acts 17:25](#)). Utu huwa kweli ndani ya mahusiano yanayotambulika, na uhalisi wa mahusiano unaweza kudumu pale mmoja anakuwa na kitu au mtu anapokuwa hana mtu wa kuwa na mahusiano naye; ikiwa Mungu hakuwa na wingi katika ye ye mwenyewe asingekuwa na mahusiano hadi pale alipoanza kuumba na ndipo angetegemea uumbaji wake kwa ajili ya utu wake. Katika nafsi za tatu kumekuwa na mahusiano mazuri kabisa. Mungu ni, kutoka katika misimamo yake, jamii kamili,f. Nje ya wingi wa Utatu yumkini umilele wa Mungu wa vilivyoumbwa au mahusiano ya umilele wa nafsi ambao umekuwepo ungekataliwa.
4. Mafundisho ya utatu ni zaidi ya uelewa wa mwanadamu na uwezo wa mwanadamu. Hata hivyo ni muhimu kuelewa asili ya Mungu na umuhimu wa historia ya wokovu ambao katika hilo Mungu anaonekana akitenda katika utatu. Ukristo wa Kibiblia unajengwa au kuanguka kuititia mafundisho haya ya Utatu.

Jinsi ya kusoma,kutafasiri na kuyatumia Maandiko

Tafasiri kwa mtu ambaye ni mlei

Lengo

Katika **2 Timotheo 3:15-17**, lengo la kusoma maandiko ni kujengwa kwa ajili ya kila kazi iliyo njema . Katika kufanya hili tunapaswa kuyaangaliamaaandiko kwa kusudi la kusikia kutoka kwa Mungu ili kukuza mahusiano yangu na Mungu katika Yesu Kristo.

Kwa hiyo lengo ni kumuona Yesu katika neno lake Kwangu, “*ambayo yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu kwa imani iliyo katika Kristo Yesu*” *Mstari wa 15*

Unapokuwa unasoma maandiko maandiko nayo hukusoma wewe, yanakuuliza na kuyajua mawazo yako (Waebriania. 4:12) – na kmwongoza mtu sit u katika kweli na kanuni. Maandiko yote hutupeleka katika kifo cha Yesu na kufufuka kwake, Katika msamaha wa Mungu na hivyo kukufabya uwe na uhusiano mzuri na Mungu kwa njia ya Kristo.

Yachunguze maandiko kwa shauku kubwa ya kujengwa uwe kama Mungu anavyokukusudia na ufanye kile ulichoitiwa kufanya.

- Usiliache Neno kama Yakobo “*Shika sana lichonacho*”
- Pambana mpaka upate na uone kuwa ni asali na dhahabu katika roho yako.

Maswali sita muhimu mfasiri anapaswa kujiuliza:

1. Ni wapi Biblia inazungumzia na kueleza katika Historia za nyakati za Biblia?

Kila kifungu cha Biblia kinapaswa kutafasiriwa katika nuru ya hadithi kubwa ya ukombozi wa Mungu na urejesho. Usiangalie Biblia kama Hadithi Fulani zilizoandikwa kwa ajili ya masimulizi; bali itazame kwa mtazamo wa maelezo ya Mungu mwenyewe. Biblia inahadithi moja, Hadithi ya Baba/Mungu ikimwokoa mwanadamu na krejesha kile kilichopotea pale katika Bustani.

- 1) Wapi mstari huu unalingana au kendana katika hadithi hii kubwa?

Katika nyakati ni wapi hadithi hii inaendana juu ya, “*Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake kwa Kristo*” **2 Wakorintho. 5:19**? Je ilikuwa kabla ya wazee wetu -Abraham, Isaka na Yakobo? Je ilikuwa kabla ya sheria za Mungu au ni baada ya sheria? Je ilikuwa ni katika Injili lakini kabla ya ukamilifu wa Roho katika kanisa la Agano jipya?

- 2) Jiulize mwenyewe, “Ni Agano gani lilikuwa na nguvu kipindi inaandikwa”?

Je hili ni Agano lililopita la kweli (au ahadi) au jipya lililotimia, jinsi utakavofanya maamuzi katika kutafasiri itasababisha jambo muhimu katika kutafasiri kwako kwa maandiko.

2. Ni nini wasikilizaji wa kwanza waliskia?

Bila kujiuliza swali hili utaishia katika kuweka mawazo siyo na kuweka Kiroho, “Ni kwajinsi gani hawa waliosikia kwanza walilipokea au walielewa”? Ili kujibu swali hili ni lazima usome sura nzima ili uielewe asili yake. Kuna aina mbili za sura katika maandiko.

Uhakiki wa waliyomo:

Mtafasiri anapaswa kuwa na ufahamu kwamba Maandiko yamehusisha namna mbalimbali za uandishi na hivyo mkarimani anapaswa kuwa makini namna ya kutafasiri. Kwanza jiulize, “Ni aina gani ya Uandishi Je nikitabu au ni mstari”?

Je ni simulizi? Vitabu vingi katika Biblia ni masimulizi. Masimulizi ni hadithi au michezo iliyosimuliwa. Vitabu hivi ni pamoja na Mwanzo, Kutoka , mambo ya walawi, Hesabu, 1st & 2nd Samweli, 1st & 2nd Wafalme, Matendo, na vingine.

Je nivitabu vya Hekima? Vitabu kama Ayubu, zaburi, Methali, maombolezo, Muhubiri, na wimbo ulio bora ni vitabu tunavyoooviita “Vitabu vya Hekima”. Vitabu hivi ni tofauti na vile vya masimulizi kwa namna ya kwamba vimejawa na lugha za Mashairi, au vina, mafumbo au maneno yaliyojirudiarudia kusisitiza.

Je ni vitabu vya Kinabii? Manabii walitekeleza Agano la Mungu kwa Waisraeli kwa maombi , “Kwanini Mungu anafanya haya na nini kitakuwa kama matokeo tukitii. Aina hii ya uandishi ina namna yake kama vile “ Maono, Utabiri” uliopekee sana kwa manabii.

Injili nne: haya ni maisha ya hadharani ya Yesu yaliyovuviwa na Roho Mtakatifu, Ujumbe na dhabihu.

Kila kitabu kiliandikwa na mtunzi tofauti lakini vyote vinaeleza habari moja inayofanana ya maisha ya Yesu, mafundsho, Kifo, kuzikwa, Kufufuka na kupaa mbinguni. Mfafanuzi wa neno anapaswa kufahamu waliokuwa wamekusudiwa kupokea neno hili na kusudi la kuutoa ujumbe huo kwao ili aweze kufasiri kwa usahihi Injili anayoisoma.

Mfano: Luka hakuwa shahidi wa huduma ya Yesu. Alikuwa kama mtoa habari akikusanya habari toka kwa walio ona na kuziandika na aliandika habari zake ili aweze kuzipelekwa kwa rafiki yake Theofilo.

Hata hivyo, Yohana aliyekuwa shahidi wa maisha ya Yesu na mafundisho anatueleza kwa nini aliandika Injili yake. Katika Yohana 20:31 anasema, “*Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo Mwana wa Mungu na kwa kuamini mwe na Uzima kwa Jina lake*”. Hii ndiyo maana tunaiita injili ya Yohana ni Injili ya kuamini. Yohana aliandika Injili yake kwa

wasiokuwa wayahudi hata hivyo Mathayo naye aliandika kwa Wayahudi akiwahimiza kwamba Yesu ndiye masihi aliyekuwa anasubiliwa, mwana wa Daudi aliyahidiwa na Kusudi la kitabu cha Mathayo ni kwamba “Imetimia”.

Je ni mfano? Mfano ni ni aina ya uandishi wa pekee. Ni hadihi za duniani zikiwa na maana ya mbinguni. Maelezo ya mifano mara nyingi huwa hatuyachukulii sana. Hutumia vielelezo, picha, na lugha nzuri sana. Ikiwa msomaji atakamilisha kwa kusema mfano huu ni kweli atakuwa ameriharibu neno la Mungu maana yake.

Kwa mfano, Katika Luka sura ya 8 ni mfano wa Yesu kuhusu mpanzi na mbegu. Mfano huu unamaanisha sana lakini siyo ndiyo iwe kweli. katika Luka 8:19, Yesu anasema, “*Mbegu ni Neno la Mungu*”. Unapaswa kujua kwamba kitendo cha mkulima kuweka mbegu katika udongo ni sawa na Jinsi ambavyo Mungu anaweka neno lake ndani ya mioyo yetu. Hiyo ni lugha ya mfano au alama..

Je ni kitabu cha utabiri? Hiki ni kama kitabu cha ufunuo ambacho kimejaa Alama na aina hii inahitaji ufahamu ili kuelewa maana yake iliyokusudiwa. Ina tumia sura za majoka, Malaika, mapepo, Vita na Dubu aliye na vichwa saba. Hivyo inatakiwa uwe makini katika kufasiri.

Je ni Nyaraka? Nyaraka ni barua zilizoandikwa kwa mtu au kanisa. Barua kutoka kwa Paulo, Petro, Yakobo na Yuda ni barua za kitume zilizoandikiwa watu halisi na makanisa halisi lakini ziliandikwa chini ya uongozi na uvuvio wa Roho mtakatifu. Hivyo, Uhalisi wa yaliyomo inabidi usome sura yote kwa makini, ukiyaangalia maneno, Sentensi na aya zinazoendelea na ukiifuata sura nzima. Uhalisi huonesha sura nzima kwa kuonesha lengo zima la kitabu.

Mfano: Tazama **Luka 17:5** ambapo wanafunzi walimwambia Yesu, “*Ongeza imani yetu*”.

Sura itakuonesha kwamba hili si swala la kuongezewa imani tu lakini pia kinyume chake – ni maelezo ya wasiwasi. Kama hautasoma “*Bwana ongeza Imani yetu*” Katika usomaji wa jujuu unaweza kukosa maana yake haswa. Fahamu pia uhalisi wa maandiko hufuatana katika kitabu kizima. Jiulize, “Ni nini asili ya kusudi la kitabu”? Lengo ni kufahamu lengo la mwandishi wa Kitabu.

Mfano: Kila mara unapoona “Kwa hiyo” katika maandishi ya Paulo unapaswa kukufuatilia sura zinazofuata ili upate kufahamu hili neno Kwa hiyo linamaanisha nini. Kwa kufanya haya utagundua neno Kwa hiyo liko pale kwa makusudi!

Warumi 12:1 Inaanza, “*Kwa hiyo, Ninawasihi ndugu zangu...*” Hapa, Kwa hiyo ya Paulo inaeleza neema ya Mungu iliyo katika warumi **3-11**. Paulo anazungumza hayo yote kwa sababu ya yale aliyyoyafanya kwa ajili yetu katika Kristo, kwahiyto tujitoe maisha yetu kwake kama dhabihu takatifu katika huduma na utukufu wake.

Mazingira ya Historia

Ni nini mazingira ya historia ya sura. Yanaweza kuwa yanajieleza yenewe au yanajitafasiri yenewe kulingana na mila na destri ya mahali? Hii inategenmea ufahamu wa msomaji juu ya mila na desturi ya mahali, mizimu, maisha ya familia, maadili au mambo ya jamii kulingana na wakati na majira kipindi kitabu kinaandikwa. Jiulize, “Ni kwajinsi gani wasomaji wa kwanza walipokea ujumbe huu na nini ulikuwa mtazamo wao , mwandishi alikusudia wasikie nini?

Mfano mzuri ni pale Paulo alipowaandikia warumi kwamba “*Yakobo nimempenda na Esau namchukia*” (**Warumi 9:13**). **Inamaanisha nini?** Si kwamba Mungu anamchukia Esau? Paulo alipowaandikia wasomaji wake maneno haya walielewa hasa waliporejea katika kitabu cha Malaki 1:21. Wayahudi wa Rumi aliokuwa anawaandikia walikuwa wanayafahamu maandiko na habari za Yakobo na Esau. Na ndiyo maana msomaji wa Biblia anahitaji kuwa na misaada ya vitabu vingine ili kuelewa maandiko anayoyasoma:

- **Biblia ya kujifunzia**
- **Kamusi ya Biblia au Encyclopedia**
- **Komentari ya Biblia (mambo haya na misaada hii inapatikana katika mtandao)**

3. Andiko hili linahusiana vipi na tukio la Yesu?

Jiulize, “Andiko hili linamtaja vipi Yesu - neno hai la Mungu”? Yesu anatueleza kuyaangalia na kuyachnguza maandiko ilitujue yanamtaja kwa namna gani katika kila sura. Alisema katika **Yohana 5:39**, “*Hamjasoma maandiko yote haya yaninishuhudia mimi*”. Soma pia mafundisho ya Yesu katika **Luka 24:25-27**.

Kwa hiyo kila andiko linatakiwa lifasiliwe kwa kumwangalia Kristo.Hii inamaanisha kwamba kila unaposoma andiko msomaji anapaswa kusoma na aone katika msitari je hilo adiko lililopita linamtajaje Yesu au kanisa.

Hii ndiyo maana ya **Waebrania 1:1-2**, “*Mungu ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi za sehemu nyingi mwisho wa siku hizi amesema nasi katika mwana aliyweweka kuwa mrithi wa vyote tena kwa yeye aliufanya ulimwengu.*”

4. Ni kwa jinsi gani Biblia yote inavyojieleza katika kila sehemu?

Msomaji anatakiwa kuiacha Biblia yote ijieleze. Hii ni kusema kwamba habari yote kubwa ya Biblia inatakiwa sisi itutawale na sisi tuielewe angalau kwa udogo tu..

Mfano: Katika kitabu cha kutoka 20 Musa alipokea Amri kumi. Tunahitaji Agano jipy la Yesu katika mahubiri yake ya Mlimani ili yaweze kuitafasiri Biblia na mafundisho ya Rabi. Paulo katika Wagalatia yatueleze makusudi ya Sheria. Na hivyo Agano jipy likamilishe Agano la kale.

5. Ni kipi sasa napaswa kukifanya katika Sura hii kilishosemwa na maandiko?

Maandiko hayapaswi kusomwa tu ili kuwa na ufahamu binafsi. Kwa kuwa maandiko yote yanamweleza Yesu hivyo tunasoma ili tupate kumwabudu, kumtumikia, na kummwinua yeye. Tunapaswa kujiuliza, “Andiko hili linanihusu vipi”?

Msomaji anapaswa ajiliulize maswali manne katika maisha yake:

- **Nifanye nini?**
- **Niwe je? (Kwa kutambua wewe ni nani katika Kristo)**
- **Nienende vipi?**
- **Nitazameje?**

Hapa kuna maswali mengine unayoweza kujiuliza ili ksaidia katika utendaji wako wa kweli ya Neno:

- **Liandike neno la Mungu katika maneno yako ili uweze kulitenda katika maisha yako.**
- **Kuwa kwangu katika Kristo kunahusianaje na kulielewa Neno?**
- **Kinahitajika nini kwangu ikiwa nitalitenda Neno kama linavyosema?**
- **Ni kwajinsi gani naweza kufanya kile Mungu kaniambia nifanye kwa wengine pia?**
- **Ni hatua gani nifanye kulingana na hili?**

6. Mungu anawekaje kweli zake kwetu?

1. Anasema nasi kwa njia ya Neno lake lililovuviva- Maandiko matakatifu -**2 Timotheo 3:16, 17**

2. Mungu anasema nasi kwa njia ya Roho wake - Tazama **Yohana 14-15**

Tunapaswa kuushukuru umoja wa Roho na Neno – Hatuwezi kuielewa kweli nje na Roho wake ambaye ndiye Roho wa kweli. Ni Roho mtakatifu ambaye anaweza kulifunua neno lake aliloliandika . Kwa maombi unapaswa umombe awe ndiye mwalimu wako.

3. Mungu anasema nasi kwa njia ya Roho wake kupitia watakatifu wake.

Hizi ni baadhi ya njia ambazo Roho mtakatifu huweka kweli yake ndani yetu:

- 1) Roho mtakatifu hutupatia mwangaza wa uelewa.
- 2) Roho mtakatifu hulifunua Neno lake (Alilolivuvia)
- 3) Roho mtakatifu atatuelekeza jinsi ya kukaa na umoja wa walio amini. (Matendo 15)
- 4) Roho matakatifu amelipatia kanisa karama ya Neema kwa njia ya Yule anayesema nae.

Roho mtakatifu husema kweli yake kwetu kwa njia ya karama mbalimbali za walioamini - Wachungaji, Walimu, wainjilisti na Manabii.

UBATIZO WA MAJI- Historia na Maana yake

Asili ya ubatizo wa maji :

Masomo ya Historia yanaonesha uwepo wa ubatizo wa maji nyakati za Agano la kale. Wayunani walipotaka kushirikiana na Israeli na ikiwezekana wawe wayahudi (Si kwa rangi, lakini kidini), walitakiwa wapiti hatua tatu: Kutahiriwa, kutoa dhabihu za wanyama na kubatizwa kwa maji. Mfano wa kwanza wa ubatizo ulikuwa ni kuzamishwa kwa mwongofu wa kwanza wa kiyunani. THili lilifanyika katika bwawa lililokuwa katika mahakama ya hekalu la wayunani.

Hivyo ubatizo wa maji uliotajwa katika agano jipya ni mada yetu ya kujifunza.

Ubatizo huu:

- Ulianzipwa na Baba (Yohana. 1:6, 33)
- Umeagizwa na Mwana (Mt. 28:19)
- Umethibitishwa na Roho (Mt. 3:16; Mdo 2:38b)
- Umeelekezwa na Mitume (Mdo 10:48)
- Ulifanywa na kanisa la Kwanza (Mdo 2:41; 8:12; 9:18)

Maana na aina ya Ubatizo wa Maji

Neno la Kiingeleza ‘Baptize’ linatokana na neno ‘Baptizo’ (kwa kiyunani) ambalo ni matokeo ya chanzo cha neno “bapto”. Kiyunani -Bapto inamaanisha “kuchovya” (Lk. 16:24; Yh. 13:26; Uf. 19:13) Inabeba wazo la kuchovya kitu ndani ya kimiminika halafu baadae unakitoa nje.

- Matumizi ya kihistoria – Tendo “Baptizo” Linaweza kuangaliwa toka Mwanzo, katika Lugha ya Kiyunani miaka ya K.K. 5. Linamwendelezo wa kihistoria katika Lugha ya kiyunani hadi karne ya kwanza nay a pili B. K. kila mahali neno hili halijabadilika maana yake ya - “Kuchovya”, “kuzamia”, ‘kuzamia ndani ya’, au “Kuzamisha”. Mf. Kati ya miaka ya 500 na 400 K.K.- Tabibu; kati ya miaka ya 200 na 100 K.K..- 2 Wafalme 5:14 (Septuagint); Kati ya 100 K.K. na B.K. 100- Strabo; Karne ya kwanza B.K.- Yoseph; kati ya kjarne ya kwanza na ya pili.- Plutarch
- Jambo la ufundii- ‘Bapto’ na ‘Baptizo’ hayajatumika katika wakati wa kutendewa. Hii inamanisha kwamba maji hayajasemwa kwamba ubatiuzwe ndani ya mtu Fulani, bali mtu Fulani abatizwe ndani ya maji. Inabeba maana ya “Kuzika katika ardhi.”
- Uthibitishpo wa Kibiblia-Kuna uzamishwaji uliofanywa na Yohana (Yohana. 3:23); Ubatizo wa Yesu (Marko. 1:9-10); na ubatizo wa mkushi wa Ethiopia (Mdo 8:38-39)

- Uthbitisho mwingine wa ubatizo kuwa ni kuzamisha unapatikana katika kitabu cha **The Didache**: Hiki ni kitabu cha kwanza cha huduma ya Kikristo kilichoandikwa kati ya miaka 100 – 100 B. K. kinachotrofautisha kati ya “kunyunyizia” kiyunani ni ekxeo, na “Kuzamisha” ni (baptizo). Mwanahistoria wa kanisa Philip Schaff, Mwana uamsho Martin Luther, na John Calvin wote wanaeleza kwamba kuzamisha ulikuwa ni utaratibu wa kanisa la kwanza. Yoseph (Myahudi mwanahistoria wa karne ya kwanza) alimwita yohana mbatizaji kuwa ni ‘Yohana Mchovyeshaji’. Ubatizo wa kwanza kwa ajili ya hao watu wa mataifa walioojiunga na imani ya wayahudi ilikuwa ni kuzamishwa. Ni vyema kujua kwamba kuna neno jingine la kiyunani linalotumika

“Kunyunyizia” Ni tendo la kiyunani, “prosraineo. Halikuwa hadi miaka ya B.K.1311 kwambva kanisa la Roma katika baraza la Ravenna likafanya ‘Kunyunyizia’ sawa na ‘kuzamisha’ kama njia ubatizo wa mbadala. Miaka ya 1644 kanisa la England likafanya kunyunyizia kama njia ya ubatizo kwa kupiga kura ya bunge.

Umuhimu wa Ubatizo wa Maji

Kuna misimamo miwili ya Ukristo mikubwa: Kundo moja linaamini kwamba ubatizo ni muhimu sana na unaweza kuweka uzima ndani ya mtenda dhambi (Ubatizo wa kuhuiosha), hali kundi jingine lina amini kwamba hakuna chochote kinachotokea katika ubatizo wa maji – bali yamesimama tu kama alama. Lakini hata hivyo misimamo yote hii miwili inapaswa kuepukwa.

Ubatizo si jambo la ajabu; lakini pia siu jambo ambalo halina maana. Muumini wa kweli anapokuwa amebatizwa ni swala muhimu sana la kiroho katika kuikiri imani yake katika Kristo. Toba na imani yake imemfanya awe ni kiumbe kipyta, na ubatizo wa maji ni tangazo la hadharani la kuwa ndani ya “Kristo.”

- Ubatizo wa maji ni kujitambulisha kwa Bwana Yesu Kristo (Rum. 6:3-4; 1 Kor. 15:1-5; Ef. 1:13; 1 Petro. 2:24) Katika Ubatizo, Mkristo anakiri ikmani yake katika kristo na kazi yake msalabani. Kwa wazi anatangaza Imani yake katika Injili. Kwa hasa ‘anajitambulisha’ na ‘kujiungamanisha’ na kifo, kuzikwa na kufufuka kwa Yesu Kristo. Anatangaza kwamba Yesu kristo alikufa kwa ajili yake, akazikwa na kufufuka kwa ajili yake na hivyo nay eye anajihesabu kuwa amekufa na kuzikwa na kufufuka na Yesu.
- Ni kumvaa Yesu Kristo (Wagal. 3:27) Katika Ubatizo Mkristo aamvaa Kristo. Kwa njia ya tendo hili anatangaza kwamba yeeye ni mali ya yesu na kwamba tangu sasa “si yeeye anayeishi bali ni Kristo”. Kama vile sare zinavyoonbesha kwamba wanafunzi hawa wanatokea wapi hata ubatizo uko kwa njia hiyo unatangaza kwamba muumini ni mali ya Yesu. Ni ushuhuda wa wazi kwamba Mtu aliye batizwa sasa ni Mkristo.
- Ni maelezo ya kusamehewa dhambi (Mdo 2:38) katika ubatizo wakristo wanaonesha ukweli wan je kwamba amepokea msamaha wa dhambi. Hii sehemu ya maandiko inasema: Tubuni mkabatizwe ‘kwa’ ajili ya msamaha wa dhambi ... Hii haimanishi kwamba tunapokea msamaha ikiwa na pale tunapobatizwa. Neno “kwa” katika kiyunani ni Kihusishi)inamanisha hapa: ‘*kwa*

ajili ya', au '*kwa sababu ya*'. Mstari unasema: "Tubu na ubatizwe kwa ajili ya kuwa na upikeaji wa msamaha wa dhambi". Msamaha hauji kwa njia ya ubatizo. Unapatikana kwa njia ya Yesu (Lk. 24:47; Mdo 5:31; Mdo 10:43; Waefeso. 1:7) na damu yake (Mt. 26:26; Waebrania. 9:22; 1 Jn. 1:7).

- Ni ushuhuda wa Utambuzi wa Mungu (1 Pet. 3:21) katika ubatizo Mkristo anashuhudia kwamba amepokea kutambuliwa kwema na Mungu. Sisi ni maadui wa Mungu kwa sababu ya dhambi zetu. Lakini kwa njia ya mahusiano yetu na Mungu tumekwisha kupatanishwa na sasa tuko na amani na Mungu (Rum. 5:1; 2 Kor. 5:18-19). Miyo yetu tayari imekwisha kunyunyiziwa damu ya yesu ili tuwe safi kutoka katika hatia zetu na sasa tunaweza kuja kwa ujasiri mbele za uwepo wa Mungu (Waeb. 10:19-22). Kumbuka: Sehemu ya andiko hili inaeleza ubatizo kuwa ni jawabu, mwitikio, auhimizo lautambuliwaji mwema mbele za Mungu.
- Ni lango la kuingia katika maisha ya hadharani kama mfuasi wa Kristo (Mdo 2:40-42; Rum. 6:4) katika ubatizo, wakristo kwa kwa uwazi anatangaza mwisho wa maisha yake ya kale – maagizo ya kale. Njia za kale za ulimwengu zinakuwa zimezikwa au kuzamishwa katika maji na sasa ameibuka upya katika mfumo wa serikali ya Mungu. Na hivyo sasa anaungana na ushirika wa kanisa, watu wa Mungu. Katika nyakati hizo ubatizo wa wayahudi katika jina la Yesu ilimanisah ni kupoteza uyahudi na ushirika wa taifa lake, kisiasa na haki zake na faida zake.

Biblia inawaagiza wale wote wanaomwamini Bwana Yesu wabatizwe katika jina la Baba, Bwana na Roho Mtakatifu (Mt. 28:19; Mk. 16:16; Mdo 2:38; 8:12, 37; 10:47-48; 16:33-34). kumbuka: hakuna ubatizo kabla ya kuokoka unoonekana katika Agano jipya.

Kweli hii inaweza kuonekana kwa ukweli kwamba watu mara zote wanaufanya ubatizo baada ya kuokoka siyo kabla ya kuokoka. (Mdo 8:12; 9:17-18; 10:47-48). Mara zote Mungu hutenda kazi ndani kwanza halafu baadae anakuja nje. Anambadilisha mtu baada ya kuwa amembadilisha moyo wake kwanza. mfano imani (ndani) na matendo (nje) Tunaambiwa kuamini katika miyo yetu na kukiri kwa vinywa vyetu (Nje) (Rum. 10:10) Mwanadamu anaangalia mwonekano (Nje) lakini Mungu anaangalia moyo (Ndani) (1 Sam. 16:7) katika Biblia katika Biblia Ibada zinatokana na uhalisia wa ndani. Mfano. Abraham aliamini kwanza. Alitahiriwa baada ya miaka 25.(Waeb. 11:8; Acts 7:2-4; Linganisha Mwanzo. 12:1-3 Na Mwanzo. 17:9-19; Linganisha Rum. 4:1-4 & 10,11)

- Kwa nini sasa watoto wasistahili kubatizwa? Kwanza hakuna uthibitisho wa biblia unaousiana na Swalka hilo. Katika swala zima la ubatizo haioneshi kwamba motto anaweza kushiriki. Hata Didache hakikuruhusu ubatizo wa watoto wadogo. Maisha ya Kikristo ni pale mtu anapowajibika kwa Mungu. Hakuna nafasi ya uwakala. Mtoto hawezu kubatizwa na mtu mwagine anayeaminu ubatizo kama yeye. Kwa mfano – Wokovu: Siwezi kuokoka kwa ajili ya mwagine' nguvu ya Roho Mtakatifu: Siwezi kupokea upako kwa ajili ya mtu mwagine; utakatifu: Siwezi kuwa mtakatifu kwa ajili ya mtu mwagine; Hukumu: Siwezi kuwajibika kwa ajili ya mtu mwagine. Yesu aliamuru wanafunzi wake wabatizwe, mwanafunzi ni mfuasi, mtu

anayejifunza na anafundishika. Mwanafunzi ana Bwana wake. Mtoto hawezi kuwa ni mwanafunzi! Hata kipindi kile watu walipokuja kwa Yohana Mbatizaji aliwaamuru watu wote watubu kwanza. Wale waliotubu ndiyo walio batizwa . (Mt.3:8, 11; Mk. 1:5; Lk.3:8-14; Mdo 13:24).

Maswali ya kawaida yaliyoibuliwa kutetea Ubatizo wa watoto

“Biblia inasema “Wote wa nyumbani mwako” kubatizwa. Je katika nyumba hii hapakuwa na watoto?”

Tunapaswa kuelewa kwamba swala si kwamba kulikuwako na watoto katika nyumba hii. Yawezekana walikuwepo. Lakini somo linalohusiana na watu wa nyumbani mwako haijalishi kuna watoto au hawakuwepo bali wale tu waliookoka ndiyo wale waliobatizwa. Kornelio: Mdo 10:44, 47, 48; Bwana jela wa Philipi: Mdo 16:33-34; Krispo: Mdo 18:8; Stephanas: 1 Kor. 1:16 na 16:15; Lidia: Mdo 16:15 (katika swala hili haitaji kwamba ni wale tu walioamini ndiyo walibatizwa, lakini pia hii haihalalishi kwamba watoto walibatizwa kwa sababu Neno la kiyunani linalomaanisha wa “nyumbani mwako” linaweza kumanisha kuwa ni wale waliokuwa katika nyumba ya Lidia wafanyakazi, watenda kazi aliokuwa kawaajili kwa ajili ya kuuza nguo - 16:14).

“Je yesu hakuwazuia wanafunzi wake wasiwazuie watoto kuja kwake? Je hakusema kwamba watoto wasizuiliwe kuja kwake kwakuwa ufalme wa Mungu ni wao? (Mt.19:13)”

Ndiyo. Kumbuka watopto hawa walikuwa wanaletwa kwake ili aweze kuwabariki na siyo kuwabatiza. Haya mawili ni tofauti kabisa. Kumbatiza mtu ni kumtambulisha katika kazi za msalaba kubariki ni kutafuta faida za Mungu kwa ajili ya mtu huyo.

“Je kutahiriwa ni mbadala wa ubatizo katika Agano jipy?”

Hapana. Kutahiliwa na kubatizwa makusudi yake ni tofauti kabisa. Kutahiriwa ilikuwa ni kwa ajili ya Israeli? Wazao wa Ibrahim; ilikuwa ni alama ya mtu kuwa na ushirika na taifa la Bwana. Ilikuwa si kwa aili ya waumini wote

Na ndiyo maana Naamani na Yule aliyetubu hawakuambiwa watahiriwe. (Tazama 2nd Wafalme 5) Ubatizo, kwa upande mwingine ni kwa ajili ya kila aliye amini; ni ishara ya mahusiano binafsi na Bwana. Kutahiriwa ilikuwa kwa ajili ya wanaume tu, ubatizo ni wa ajili ya wote, jinsia zote. Kutahiriwa kulifanyika siku ya nane hali ubatizo unafanyika mara tu mtu anapoweka maisha yake kwa Mungu. Ikiwa ubatizo uliingia kuwa niamba ya kutahiriwa haitaleta maana kwani wayahudi katika kanissa la karne ya kwanza walihitaji watu wa mataifa watahiriwe pia (Mdo 15:1-2). Hakika wayahudi wa Kikristo hawakuona kama ubatizo uko kwa niaba ya kutahiriwa.

“1 Kor. 7:14 je haitetei ubatizo wa watoto kwa sababu inasema kwamba watoto wa walio amini tayari hao ni watakatifu?”

Sura nzima (mst 12-16) nio jawabu la Paulo kwa ndoa mchanganyiko ambapo mmoja wa wanandoa ni muumini. Hali ilikuwa kwamba baadhi ya wababa na wamama amba walikuwa tayari wamekwisha kuoana kabla ya kuokoka walikuwa wamechanganyikiwa kama ndoa zao zilikuwa na kibali mbele za Mungu maana mmoja wao hakuwa ameokoka. Walikuwa katika kitendawili kwamba waachane au wafanyaje. Swala lilikuwa ni kwamba tufanye nini juu ya hawa watoto? Paulo akajibu akawaambia kwamba ndoa hizo mchanganyiko zinakubalika na Mungu kama aliyeamini ataishi maisha ya Ki Mungu kwa ajili ya Mwenzie ili kwamba na mwenzi wake apate fursa ya kuyatoa maisha yake kwa ajili ya wokovu. Na kwa kawaida ni kwamba ikiwa wazazi wanakubalika na Mungu basi ni halali kwamba wazae watoto. Kwa hiyo Paulo alipozungumza juu ya watoto kuwa watakatifu naq mwenzi asiyeokoka kutakaswa anachomaanisha ni kwamba uwepo wa aliye amini katika nyumba unaiweka ile familia kuwa katika wingu la utakatifu ambalo lityapelekea asiye amini apate fursa ya kupokea wokovu. Hamanishi kwamba wanakuwa wameokoka.

- **Nini kile Biblia inasema kuhusu watoto**

Hatupaswi kuogopa kwamba watoto wasioamini wanapokufa kabla ya kuisikia Injili kwamba watapotea milele. Mungu ni mwenye haki, wa rehema na anapenda watoto wote, hajjalishi wamezaliwa katrika nyumba za kikristo au hapana (Mt.18:2-3; 19:14). Hawezi kuwawayibisha hadi pale watakapoweza kutambua mema na mabaya (Kumb. 1:39; Is. 7:15-16). Jukumu la mzazi ni kuwalea watoto katika kumcha Mungu (Waefeso. 6:4) na kuwaongoza katika Njia iwafaayo (Methali.22:6).

- **Ni kwa jinsi gani ubatizo wa watoto ulianza kanisani:**

Mapokeo haya yalianzishwa na I renios (karne ya pili B.K.), yakapiungwa na Tetulia na baadae yakaaza kufanyika miaka ya karne ya 5. Huu ubatizo wa watoto ulianza kama matokeo ya mafundisho ya uongo ya sakaramenti nkatika kanisa la Roma. Mababa wa kanisa walipoanza kufundisha kwamba ubatizo unampatia mtu kuokoka au neema ya siri. “ Ubatizo wa uhuisho” “ ubatizo wa maji unaondoa dhambi). Pia kulikuwa na sababu za kisiasa. Kanisa la Roma lilitaka kila mtu aingie katika mifumo yao kwa kumfanya kila mtu kuwa ni Mkristo tangu anapozaliwa, kanisa likahakikisha kwamba watu wanakuwa chini ya kanisa na uongozi wa kanisa la Roma.

Wakati wa Ubatizo wa maji

Katika Biblia tunaona kwamba wale waliosikia na kuikubali Injili walibatizwa “haraka”. Hapakuwa na kucheleweshwa (Matendo 2:41; 8:12; 8:36-38; 16:31-34). Swala lilikuwa ni kwa Paulo tu ambaye alibatizwa baada ya siku tatu na hili haikuwa ni kosa lake (Mdo 9:18).

Baadhi ya maswali kuhusiana na Ubatizo wa maji

- Muunganiko kati ya Ubatizo na Wokovu

Wokovu limekuwa ni wazo la kuokoka na Jehanamu. Na hivyo inaleta shida sana wanapofundisha kwamba ubatizo ni sehemu pia ya wokovu. Lakini tunapaswa kuelewa kwamba wokovu unahatua tatu. Na hatua zote znatakiwa kupitiwa ili mtu hakika na kweli awe ameokoka. Kuna wokovu wa mambo a nyuma-kuokoka kutoka katika dhambi, wokovu wakati uliopo – ukombozi kutoka katika nguvu za dhambi na wokovu kwa yajayo – ukombozi kutoka katika uwepo wa dhambi. Mtu anapotubu nha kuamini anafanyika kuwa muumini. Lakini swala la wokovu linakuwa halijaisha, hatua yab pili ni kubatizwa kwa maji na baada ya tendo hili anapaswa kuendelea katika imani ya Kikristo. Pia swala la wokovu linapasw kuendelea katika maisha yake na baada ya Yesu kuja kututwaa ndipo sasa tutao koka kikamilifu.

- Je tunapaswa kubatizwa kwa kanuni ya Tritarian?

Kipi ni sahihi – Kubatizwa katika Jina la yesu; au katika Jina La Baba, Na la Mwana Na la Roho Mtakatifu? Mt. 28:19, 20 inasema tunapaswa kubatizwa katika Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu'. Sababu ya kanuni ya Tritarian kutokutajwa katika kitabu cha Mtendo kwa sababu mkazo ulikuwa katika tofauti kati ya Ubatizo wa Yohana au Ubatizo wa kiyahudi na ubatizo ambao yesu alikuwa kauleta. Hata hivyo haijalishi tutumie kanuni ipi tunashuhudia Injili ya yesu Kristo na hatuna haja ya kuhalalisha hilo.

- Kwa nini yesu alibatizwa?

“*Kutimiza haki yote*” (Mt. 3:15). Kwa mameni mengine, yesu alibatizwa kama tendo la nje kwa ajili ya utii kwa ajili ya wito wake wa Kimasihi. Alitaka kufanya kila kitu ambachokilikuwa kikimpendeza Mungu. Kwa hali hii akawa ni mfano wa kutuonesha sisi jinsi nasi tunavyotakiwa kuishi maisha yanayompendeza Mungu.

- Je tunapaswa kubatizwa “kwa ajili ya waliokufa”??

(1 Kor. 15:29) Hapana. Hili halikuwa ni tendo la kitume. Paulo hakusema “ kwa nini tubatizwe kwa ajili waliokufa... ” lakini kwa nini wanabatizwa kwa ajili ya wafu” sura hii inahusika na ufufuko. Paulo alikwa anajaribu kuthibitisha kweli ya ufufuko kwa wayahudi wale ambao hawakuamini. Ili kuendeleza wazo lake la kwamba hakika kuna ufufuko akaamua kueleza kupitia wayahudi. Kwa kuchukua ubatizo wa wafu walikuwa wameonesha kuwa walikuwa na hofu ya ufufuko japo hawakuwa wanakubali. Hapa Paulo alichukua tamaduni zilizokuwepo kwa ajili ya faida yake na hakuwa anaandika kama sheria kewa Wakristo.

Usalama wa Muumini Je Muumini Anaweza Kupoteza Wokovu Wake Wa Neema?

Kila Mkristo anawasiwasi na Wokovu wake katika Kristo. Mashaka yamekuwa yakiwaingia watu wapya na wachanga, kama mwizi usiku na kuondoa Uhakika wao wa wokovu. Kunakuwa na mnong'ono katika sikio ukitoka kwa adui na kutuambia kwamba tumepotea. Anasema, "unawezaje kujiita Mkristo na kufanya kile ulichokifanya?" Pia kunasauti nyingi kutoka madhabahuni zikiwaambia waumini kwamba kutokutii kunaweza kukutenga na Kristo na upendo wake.

Je muumini anaweza kupoteza wokovu wake kwa njia ya wasiwasi, dhambi au kutokutii kwa hiari ? Je twaweza "Kuanguka kutoka katika Neema?" Inawezekana kuokoka milele halafu ukapoteza zawadi hii ya thamani kwa matendo, yale tuliyoyafanya au kutokuyafanya?

Jambo Lenyewe Hasa

Kwanza tunapouliza Swali, "Je Mkristo anaweza kupoteza wokovu wake?" Tunapaswa kujiuliza swali lililombee yetu ambalo ni la maana sana ambalo ni, "*ni kwa jinsi gani nilipokea wokovu wangu mara ya Kwanza?*" Je msamaha ulikuja kwangu kwa sababu ya kile nilichokifanya au msamaha ni matokeo ya kile Yesu alichokifanya kwa ajili yangu? Je kuokoka nui juhudhi zangu au ni kazi ya Yake? Ninapaswa kuangalia kama kuokoka ni kwa neema au kwa matendo au ni yote mawili. Jinsi nitakavyojibu maswali haya ndipo nitakapokuwa nimepata jawabu la ninaamini au siamini kwamba naweza kupoteza wokovu wangu.

Nilikuwa na Wokovu, lakini Nimeupoteza

Madhehebu mengi makubwa yanafundisha kwamba muumini anaweza kupoteza wokovu kwa sabau ya dhambi ambazo hazijatubiwa au kuungamwa.. Mjadala huu ulianza zamani kabisa karne ya 17. John Calvin Na James Arminius walikuwa na mitazamo tofauti. Calvin alifundiosha "Usalama wa milele wa Muumini," ambapo Arminius alisema "hapana." Kwenye swala la usalama wa milele. Madhehebu yametofautiana sana kutokana na mawazo ya watu hawa wawili.

Calvin anasema, "NINAO SIWEZI KUUPOTEZA !

Arminius anasema, NINAO, LAKINI NAWEZA KUUPOTEZA!

Kwa hiyo, Ukweli uko wapi?

Kitendawili

Lugha zinaweza kuchanganya, kwa mfano wazo la "kuokolewa." Neno nhili linamaanisha , Kunusurika, ukombozi, kuokoka. Ni kwa jinsi gani naweza kuokolewa "kwa muda" au kuokolewa kwa "sehemu"? Ni kama kusema ulinusurika kupigwa risasi au ukapona kutoka

katika kukanyagwa na gari. Ikiwa kama ulipigwa risasi basi haukunusurika. Kama gari lilikanyaga au hata kama ni sehemu ndogo tu ujue haukupona na hilo gari. Kuokoka kwa moja kwa sehemu au kwa muda mfupi si “kuokoka” kabisa. Kiukweli kuokolewa kutoka katika nini? Katika Biblia tumeokolewa kutoka katika “ghadhabu” kwa njia ya kristo. Au hatujaokolewa au tumeokolewa kutoka katika ghadhabu ya Mungu.

Milele au Kitambo

Tafakari juu ya neno *Milele* katika maandiko. Linamanisha” maisha ya vizazi, au kutoka kizazi hadi kizazi.” Msamaha anaotupatia yesu umerudiwa sana ukiitwa “Uzima wa milele.” Tazama **Yohana 3:16; Yohana 3:36; Warumi 6:23; Waebrania 7:25; 1st Yohana 5:11-12** Sasa ni kwa jinsi gani tena wokovu uwe wa milele na bado uwe wa muda kitambo? Wokovu ambaos yesu ametuahidi unaelezwa kama, “*name nawapa uzima wa milele wala hawatapotea kamwe wala hakuna mtu atakayewapokonya kutoka katika mkono wangu.*” **Yohana 10:28**

Kumbuka, ikiwa kamwe huwezi kupotea inawezekanaje ukawahi kupotea? Na kama msamaha ni wa milele (milele) kwa nini isiwe milele au kitambo tu?

Zawadi Na Mshahara

Maandiko yanaeleza kwamba wokovu ni kama “zawadi.” Neno la Mungu linalo sema “Neema” ndani yake limebeba kitu kinaitwa zawadi. Neema mara zote ni zawadi na si mshahara. Kiukweli msahara na zawadi ni maneno mawili yanayopishana. Msahara ni malipo unayopata kutokana na kazi uliyofanya na zawadi hauifanyii kazi inatolewa bure na ndiyo maana inaitwa zawadi.

Wokovu ni zawadi ambayo unapaswa kuipokea na wala si kitu ambacho unakifanyia kazi ili ukipate. Inapokea zawadi. Si kustahili ulikokufanyia kazi bali ni rehema ambayo Mungu huachilia. Wokovu hauanzi katika maisha ya Mtu bali katika upendo wa Mungu.

Wazo la kupoteza wokovu linaaamisha kwamba ulipata wokovu kwa sababu ya tabia nzuri na unaweza kupoteza wokovu ukifanya tabia mbaya. Hiki si kile maandiko yanatufundisha.

Wokovu wa Neema

Hebu tuchukue muda kidogo tuliangalie neno hili wokovu wa Neema na matumizi yake.

Kwanza mwanadamu anakabiliana na mambo mawili katika uwepo wa Mungu mtakatifu:

- Kwa kuzaliwa sisi ni wenye dhambi – wana wa Adamu tumezaliwa katika dhambi (**Warumi 5:12, 19**). Asili yetu ni dhambi, ubinafsi na hatuvezi kumpendeza Mungu. Tazama **Warumi 8:8**.
- Tumeamua kuwa wenye dhambi (**Warumi 3:10-23**). Kwa hiyo sisi ni wenye hatia ya uovu dhidi ya sheria ya Mungu na upendo wake.

Kuta na vizuizi

Kwa sabu ya hivi vizuizi vilivyopo katikati yetu na Mungu mtakatifu, tunahitaji mambo mawili:

- *Ukombozi* kutoka katika hali tuliyomo – Kujitawala sisi na wala si Mungu kututawala
- *Msamaha* Kwa kile tulichokifanya – dhambi

Kile Mungu anachgokitoa Neema ya Wokovu ni kwamba ameshaangusha vizuizi vyote vilivyokuwa vinatutenga naye. Mwanadamu amesimamisha kuta mbazo hawezi kuziangusha. Mungu anbidi aanze na tayari ameanza kwa kumleta mwana wake afe kwa ajili yetu. Hatuwezi kujibadili namna tulivyo ndani na wala hatuwezi kurudi nyuma na kufanya yale ambayo tuliyakosea huko nyumba. Mwanadamu anahitaji haki lakini anahitaji rehema! Neema ya Mungu katika Kristo ni hiyo Rehema. Kuna Mtu alifafanua neno Neema kama UKUU WA MUNGU KWA GHARAMA ZA KRISTO: na kwa Kiingereza ni:

G-God's -Mungu

R-riches - Utajiri

A-at-kwa

C-Christ's -Kristo

E-Expense -Gharama

“Yaani Utajiri wa Mungu kwa Gharama ya Kristo”

Ukuu wa Mungu tumepewa msalabani kwa njia ya Wwana wake pekee Yesu. Maandiko yanasema hivi, “*Kristo alikufa kwa ajili yetu tulipokuwa tungali wenyе dhambi.*” Hiyo ni zawadi ya Wokovu wa Neema.

Taswira Ya Maneno Manne

Agani jipya linatupa taswira ya “maneno manne” yanayoonesha zawadi ya Mungu ya Neema kwa wenyе dhambi. Taswira ya maneno haya manne inatuonesha upendo wa Mungu katika kutusamehe milele na kutuweka katika sawa na Yeye Milele.

Kuhesabiwa Haki= Warumi 3:24 inasema, “*wanahesabiwa haki bure kwa Neema yake kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu.*” Neno *Kuhesabiwa haki* linamanisha kutangaza kuwa “hauna hatia”, “Hushtakiwi” au “Mwenye haki”. Paulo anasema ndicho kile Mungu ambaye ni hakimu wa dunia mwenye haki alichotufanyia. Ametutangaza kuwa hatuna hatia. Alikamilishaje hilo zoezi? Haikuwa ni rahisi. Mungu alibaki njia panda. Kama Mungu mtakatifu anapaswa kuiadhibu dhambi. Na kama Mungu wa Upendo anatamani kuwasamehe wenyе dhambi. Anachukia dhyambi na anawapenda watenda dhambi. Anawezaje kubaki mtakatifu na aendelee kuapenda watenda dhambi? *Kuhesabiwa haki* lilikuwa ni jawabu la Mungu.

Tendo la Neema. Yumkini kielelerzo cha jinsi Mungu alivyotuhesabia haki kinaweza kutusaidia kuona nini msalaba wa yesu ulichofanya kwa ajili yetu. Tuchukulie mimi ni baba yako. Lakini pia kazi yangu ni hakimu wa Wilaya. Na wewe ni motto wangiu mwasi. Unaniibia simu na wakati unaendesha gari lako ukiwa umelewa unajikuta unamgonga mtoto na kumuua. Na unaletwa mahakamani kwangu kushtakiwa. Ushahidi wote umekamilika na unashtakiwa kwa mashtaka mengi tu ya kujunja sheria. Ni jukumu langu kama hakimu kukuhukumu – wewe motto wangu kabisa. Kwa jili ya faida ya kielelezo unakuta hukumu ni kubwa tuseme hivyo. Unashitakiwa kuuawa. Ninabaki njia panda! Kama baba yako wa upendo naamua kukusamehe na kuachilia rehema juu yako, na kama hakimu natakiwa nifuate sheria na kuhukumu mvunja sheria. Nini jawabu la hili ? kama hakimu naamua kushuka kutoka kwenye kiti change na kuja kwako nasimama pembeni yako na ninajihukumu mimi mwenyewe kwa niaba yako niutoe uhai wangu nife kama ambavyo ungetakiwa ufe. Sheria inakuwa imekamilishwa na wewe unahesabiwa haki. Na unatangazwa kuwa mwenye haki, hunahatia. Ninachukua nafasi yako na adhabu—mtu asiye na hatia kwa aliye na hatia. Kuna mtu alisema kuhesabiwa haki inamanisha “kuwa kama mabavyo nilikuwa sijatenda dhambi”. Ni upenbdo mkubwa sana huo. Cha ajabu sana hicho ndicho Mungu alifanya, Mungu mwenye haki, akachukua hatia yetu. Yesu (Mungu katika mwili, **Yohana 1:14, 18; Waebrania 1:3**) alikufa kwa niaba yetu. **Warumi 5:8** inasema, “...*Kristo akafa kwa ajili yetu.*” Sasa Mungu anawaona watenda dhambi kana kwamba hawajatenda dhambi— au
wamehesabiwa haki. Tumesamehewa na hakimu wa Ulimwengu. Milele!

Kumbuka Mungu ametutangaza kuwa hatuna hatia. Ni tendo la upendo wake. Anatuona kuwa hatuna kosa hali anajua kuwa tunamakosa! Haki ya Yesu imewekwa katika akaunti zetu ambazo hazikuwa na kitu na Mungu anatuona sisi sote katika Kristo. Tumesamehewa bila kustahili ndani yetu. Hatuna chas kufanya tena. Ni Neema safi. Tuimestahilishwa na kutangazwa kuwa hatuna hatia na haya yote ni kwasabu ya kifo cha Yesu mwokozi wetu. Huo ni mtazamo mmoja wa jinsi gani Mungu aliondoa vizuizi. Yeye *alituhesabia haki* sisi katika Kristo. Tumesamehewa milele na si kuachiliwa tu.

Kukombolewa=Neno linguine la taswira lililotumiwa katika Agano jipya ni hili “Kukombolewa.” **Yesu ametukomboa na kutusamehe pia.. Warumi 3:24** Pia inasema, “Wamehesabiwa haki bure kwa neema yake kwa njia ya ukombozi ulio katiuka Kristo Yesu.” Hata kama kuhesabiwa haki inatupa picha ya kizimbani lakini kukombolewa inatupa picha ya soko la watumwa. Inaonesha mwenye dhambi ni mtumwa wa dhambi na mtumwa wa shetani. Yesu Kristo alikuja kulipa gharama kwa ajili ya uhuru wetu. Yesu alitumia taswira hii ya neno aliposema, “*Kwa maana mwana wa Adamu naye hakuja kutumikiwa bali kutumika na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi*” (**Marko 10:45**). Hili neno la Kiyunani la Fidia linamaanisha kuwa gharama zimelipwa kwa mmiliki wa watumwa ili mfungwa anunuliwe. Gharama iliyotumika kutununua kututoa katika utumwa huu ilikuwa ni damu nzuri ya Yesu. Hili lilikuwa ni wazo la Petro alipoandika, “*nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo kwa fedha au dhahabu mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kutoka kwa*

baba zenu. Bali kwa damu yaa thamani kama ya mwana kondoo asiye na ila asiye na waa yaani Kristo” (**1 Petro 1:18, 19**). Ukombozi umekwisha kununuliwa kwa ajili yetu. Uhuru wetu kutoka ktika vifungo vya dhambi umekwisha lipwa kwa damu ya yesu Kristo. Tumetangazwa kuwa hatuna hatia mbele ya sheria ya mungu na kuwekwa huru mbali na utumwa. Hatupaswi kuuzwa tena, kwani sisi si watumwa tena bali wana tumefanywa wana katika familia ya Mungu (**Warumi 8:15**). Tumewekwa huru na kuachiliwa milele! Biblia inatuambia kwamba kuna mambo angalau matano yanayohusu ukombolewaji wetu:

- Ilimgharimu Mungu atoe uhai wa mwana wake (**1 Petro 1:18, 19**)
- Ilitukia, kihistoria katika msalaba (**Wafeeso 1:7**)
- Ni milele na si kitambo (**Waebrania 9:12**)
- Ilitolewa kwa ulimwengu mzima (**1 Timotheo 2:3-6**)
- Inapaswa istahili kwa njia ya imani katika kazi ya yesu Kristo pale msalabani (**Warumi 3:26, 28**)
- **Upatanisho**= Tatu, Neema ya Mungu iokoayo imetazamwa kama a *Upatanisho* kwa ajili ya dhambi. **Warumi 3:25** inaonesha kielelezo cha tatu cha Paulo kwa kile kilichotokea pale msalabani. “*Amabye Mungu amekwisha kumweka awe upatanisho kwa njia ya imani ...*”

Hili wazo la kufanya mapatano ni neno la kikuhanu linaloonesha kilichotokea pale kuhani alipotoa dhabihu ya mnyama kwa Mungu ili kuondoa shutuma ya dhambi. Ilikuwa inaonesha siku ya Yom Kippur- siku ya mateso pale kuhani wa wayahudi kwa mwaka siku moja alitoa mwanakondoo siye na ila kama dhabihu kwa ajili ya dhambi za watu. Neno hili upatanisho linaonesha pasaka pale Misri ambapo damu iliwekwa katika miimo ya milango ya nyumba za Israeli na malaika wa mauti “alipita” juu ya yao. Pasaka ni kivuli kilichotimizwa katika msalaba wa kristo ambapo damu ya Masihi iliwekwa katika msalaba kama dhabihu kwa dhambi zote.

Wazo kuu la Upatanisho ni kwamba dhambihu ya damu isiyo na hatia ya yesu huondoa dhamira ya mashtaka yetu na kuondosha ghadhabu ya Mungu iliyokuwa dhidi yetu. Kupatanisha ni “kufunika juu” na kukwepesha ni kuondoa au kung’oa. Haya yote mawili yesu aliyafanya kwa ajili yetu. **1st Wakorintho 5:7** inasema, “*Kwa maana pasaka wetu amekwisha kutolewa kuwa sadaka yaani Kristo.*” Yohana Mbatizaji alisema, “*Tazama mwanakondoo wa Mungu aichukuae dhambi ya ulimwengu.*”(**Yohana 1:29**)

Faida za “Upatanisho” wa Kristo

Kwanza kabisa – Milele Mungu ameshatusafisha na unajisi wote. Dhambi zetu zimekwisha na kuondolewa milele. Tazama **Wakol. 2:14** amabapo dhabihu hii huondoa dhamira za dhambi zote wakati wote.

Jambo la pili, Hii inamanisha kwamba Mungu hana hasira na sisi tena! Ghadhabu yake kwetu sisi tuliookolewa imekwisha KUONDOLEWA! Yesu alichukua ghadhabu ya Mungu pale msalabani. Kwa hiyo Mkristo anapotenda dhambi (na wote tunatenda dhambi) hapaswi kuogopa ghadhabu ya Mungu. Upendo wa Mungu kwetu katika Kristo hauna masharti. Hata maonyo ya Mungu kwa watenda dhambi si adhabu bali ni kazi ya upendo ili kutufundisha tyuenende kwa imani.

Upatanisho unasema, “Mungu mashanishafisha na ananipenda milele.”

Maridhiano= katika **Warumi 5:10, 11**, Paulo anatumia picha nyingine mara nyingi tu. Ni neno la kifamilia *maridhiano*. Neno hili lilioneshwa kwetu na bwana wetu yesu Kristo katika mfano wa mwana mpotevu (**Luka 15:11-32**). Huyu mwanae aliporudi nyumbani kwa baba yake na hawa wawili wakakumbatiana baada ya mwana kuungama ile ilikuwa ni picha ya kupatana au kuritdhia.. Kupatanishwa na Mungu ni kurejeshwa kwa baba yetu wa mbinguni kwani vizuizi vyote vimeondolewa. Kwa sabu dhambi, hatia na ghadhabu imeondolewa sasa tunaamani na Mungu milele. Mungu ni Baba na sisi ni wana wake na ushirika umerejeshwa.

Kuliunganisha pambo hili pamoja

Paulo amekuwa akituonesha picha . Inaitwa *Tumeokolewa kwa Neema*. Picha hii ni kama fumbo kubwa. Tunapoanza kuviunganisha vipande vyake sasa tunaanza kuiona sasa kwa ujumla. Kumbuka huu ni mwendelezo:

Upatanisho: Mungu ametusafisha na kuondoa hatia zote.

Kuhesabiwa haki: Mungu ametutangaza kuwa hatuna hatia na tumesamehewa.

Ukombozi: Mungu katuweka huru mbali na mauti.

Maridhiano: kama matokeo tumeridhiana na Mungu na kurejeshwa katika ushirika.

Paulo anasema katika **Wakolosai 1:22**, “*katika mwili wa nyama yake kwa kufa kwake ili awalete ninyi mbele zake watakatifu wasio na mawaa wala lawama.*” Haya ni matokeo ya Wokovu wa neema. Tuna msamaha, uhuru na kusafishwa ili aweze kutuleta kwake “. . . Mtakatifu na. . . zaidi ya maonyo.” Haya yote yanamanisha Mungu kaisha tukubali kwa njia ya Kristo. Dhambi si tatizo tena. Vizuizi vyote vimeondolewa. Haijalishi ni dhambi gani umefanya hakuna kitu kinaweza kukuzuia kwa Mungu. Neema yake ni kuu kuliko dhambi zetu zote.

Maandiko nane yenye kusumbua:

Kuna sura nane tu katika Agano jipya zinazoonesha kama inawezekana “*kuanguka katika Neema.* ” . Tutaiangalia kila moja tuone wazo lililofundishwa hapo.

Yohana 15: 5,6 “ *mtu aipokaa ndani yangu hutupwa nje kama tawi akaaye ndani yangu name ndani yake huyo huzaa sana maana pasipo mimi ninyi hamwezi lolote. Mtu sipokaa ndani yangu hutupowa nje kama tawi na kunyauka watu huyakusanya na kuyatupa motoni na kuteketea*”

1. Mistari ni mifano na ni alama. Hatupaswi kujenga theologia zetu katika mifano.
2. Swala analolizungumzia Yesu hapa ni kuzaa matunda (haki), siyo wokovu au kutokutii. Swala ni “ukkaji” wetu katika kristo amabo ni ushirika wetu na Kristo na si uhusiano wetu na Krsito (Wokovu).
3. Yeye anayekaa huzaa matunda kadri maisha ya kristo yanapoendelea katika masiha yake. Hatufai katika mazao ya kiroho kama hatutakaa katika Kristo. Hii mifano ya mizizi, matunda,mzabizu na matawi ni swala letu la kuwa na ushirika wa karibu na Kristo kitu kitakachopelekea maisha yetu yawe ya maana na yanayostahili na si “yasiyostahili.”

Wagalatia 5:4 “*Mmetengwa na kristo ninyi mtakao kuhesabiwa haki kwa sheria mmeanguka nakutoka katika hali ya Neema.* ”

1. Sentensi hii inapaswa kusomwa katika “mazingira” ya kitabu kizima na kusudi la Wagalatia ambalo Mtume Paulo anajaribu kuilinda “Wokovu wa Neema” dhidi ya wale waumini wa kiyahudi kutoka Yerusalem waliokuja Galatia wakihubiri “injili tofauti.” tazama **Wagalatia 1:6**.
2. Hawa walimu wa uongo (wayahudishi) walikuwa wanchanganya sheria na Neema; wakiliambia kanisa kwamba wanaume wanapaswa kutahiriwa wanapaswa kuzingatia sheria za kiyahudi (Mishna) na siku kuu. Walikuwa wakiongeza sheria hizi kwenye msalaba wa Kristo kama matendo yaokoayo.
3. Paulo alifundisha neema tu katika swala la wokovu. Aliita mafundisho yao kuwa ni “Injili tofauti”. Ilikuwa ni Injili tofauti kwasababu iliongeza matendo kwenye kazi kamili ya kristo. Tazama **Wagalatia 2:20, 21**.
4. Paulo anawathibitishia wagalatia kwamba dhambi zetuna mambo yetu ya dini ni hoja tena lakini Neema ya Mungu tuliyopewa kwa njia ya mauti, kufufuka na kupaa kwa Christo inatosha ktupatia wokovu bila kuongeza chochote. Kuongeza juhudzi za mwanadamu ni “kukosea kanuni ya Neema ya wokovu.”

Waebria 6: 4-6

“...*ikiwa watashindwa...*” *hiki kipande kinaleta swal la je Mkristo anaweza kupoteza wokovu wake kwa njia ya kutokutii.*

1. Ikiwa inafundisha kupoteza wokovu inafundisha pia kwamba muumini anayeweza kupoteza wokovu hawezi kuurejesha tena. Amefanya dhambi inayompelekea “mauti” **Ist** ***Yohana 5*** Ikiwa inafundisha kwamba unaweza kuokoka na dhambi inaondoa Neema ya

Mungu ujue pia inafundisha kabisa kuwa Uasi – hauwezi kukurejesha tena katika wokovu. Sidhani kwamba haya ndiyo mafundisho ya hapa.

2. Mwandishi wa waebrania anaeleza kwamba wale walio katika **Waeb. 5:12-14** ni kama wale “wanapaswa kuwa walimu” ni kwamba wam, eokoka lakini ni wachanga. Wanapaswa kukua katika imani. Halafu katika sura inayofuata katika **6:1-6** anawaeleza watu wale wale kwamba wakomae. Na halafu anawaeleza kama:

“Kwa maana hao waliokwisha kupewa Nuru...

Na kukionja kipaswa cha mbinguni,

Nakufanywa washirika wa Roho Mtakatifu,

Na kulionja neno zuri la Mungu,

Na nguvu za zamani zijazo”

Maelezo haya yote ni malezo ya muumini aliye katika Kristo. Mwandishi anasema kwamba “Kama” ilikuwa inawezekana kwa waumini hawa kuanguka kutoka katika imani (kumkana Yesu) sasa haiwezekani kuwarejesha katika wokovu tena. Kwa nini? Kwa maana hakuna jina chini ya mbingu tulilopewa tunaloweza kuokolewa kwalo B (**Matendo 4:12**) Kristo inabidi arudi na kufanya wokovu tena! Kwa hiyo kama ilikuwa inawezekana kuokoka halafu ukapotea huwezi kuokoka tena!

3. Yumkini, sehemu hii (Mistari 4-6) ni ya “kufikirika” ya mtu anayetaka kueleza kwamba Kristo ni njia pekee ya wokovu na kumwacha ni kupotea milele. Tazama **1st Yohana 2:19** nadhani ni amelezo ya kimawazo na si kitu halisi. Maana inahali ya “vipi ikiwa ”. na kwa hiyo kiukweli ni kwamba sura hii inaonesha kwamba Mtu akiokoka kweli hawezi kupotea tena.

2nd Petro 2:20-22 “...Mbwa kurudia matapishi yake.”

1. Maneno haya yalizungumzwa kwa nani? Tazama 2:1= Walimu wa uongo, waliomkataa bwana wao aliyewanunua kwa damu ya thamani (Tazama **1st Petro 1:18,19**)
2. Petro anazungumza na wale ambao walikuwa tayari wameshaingia katika wokovu katika Kristo, wameiacha kweli na kurudia hali yao ya zamani.
3. Hii si hali ya kawaida ni kama maelefu ya washirika walioomba na kuongozwa “sala ya kumpokea Yesu” lakini ndani yao hakukuwa na toba ya kweli na kuzaliwa tena mara ya pili. Hawa sasa “wanaanguka” bila kuwa wameokolewa.

Yakobo 5:19, 20 “...Ataiokoa nafsi yake na kifo ...”

Kuna njia nyingi tunazoweza kuzitumia kuuelewa mstari huu:

1. Ikiwa Mkristo ataiacha kweli mrudishe uokoe nafsi yake asije akafa dhambini na kwenda jehanamu. Ikiwa hii ndiyo maana basi mstari unafundisha upotofu.

2. Ikiwa Mkristo atatenda dhambi, mrejeshe na uokoe nafsi yake kutoka katika “mauti” ya ushirika uliopotea hapa duniani. Hili wazo linapunguza neno “Kifo” na kulifanya kuwa sawa na giza au kupotoka.
3. “*Okoa nafsi yake*” inaweza kuwa na wazo lenye maana ya “uokoe utu wake” kutoka mauti. Inaweza sasa kutafasiriwa kwamba “ okoa maisha yake kutoka kenyé matokeo ya mauti ya dhambi.” Hii inaweza kuwa ni maana inayokubalika tukilinganisha na vifungu vingine ili kuelewa zaidi kama **Yakobo 4:8** na **Wagalatia 6:1,2**

Ufunuo 3:5 ...na sitalifuta jina lake kutoka katika kitabu cha uzima”

1. Mazingira yako katika yale makanisa saba ya ufunuo
2. Kanisa la Sardi lilikuwa na aina mbili za watu katika ushirika wajke, waliookoka na ambao bado hawajaokoka. Anawaambia waliookoka kwamba wokovu wao uko salama na kwasababu wanastahili majina yao milele yako katika kitabu cha uzima. Haya maelezo hayamanishi kwamba Mungu anafuta majina ya wale wanaofanya dhambi isiyosameheka.

Wazo la Mwisho

Wale waliookolewa milele kutoka katika ghadhabu ya Mungu wanaelezwa na Yesu , Paulo na Petro kwamba “wamezaliwa mara ya pili.” Unapokuwa umezaliwa kutoka juu “kuzaliwa kiroho” huwezi kutokuzaliwa tena. Unapofanywa Mwana katika familia ya Mungu milele huwezi kuondolewa tena. Kile neema inachokitoa hakiwezi kuondolewa. Mungu anachotaka kutoka kwetu ni kumtumainia. Anatuambia tuishi kwa imani. Na ndiyo maana anatupatia imani kama zawadi ya Neema yake. Haijalishji imani yako ni imara au dhaifu haiwezi kuathiri kukubaliwa kwako na Mungu. Imani ni mkono mtupu na ni chombo tukitumiacho kupokea zawadi ya bure ya Mungu.

Mila Na Injili

Utangulizi: Kila jamii ina mila zake mbalimbali. Kiukweli mila na desturi huonekana mara zote kuwa ni sawa. Historia inaonesha kwamba Ukweli halisi wa injili ya Yesu Kristo unapoingia katika Mila na tamaduni Fulani kila kitu hubadilika. Nuru hupenyeza katika giza na dini nyngi na mila na desturi nyngi ni mipangilio ya wanadamu. Maamuzi yetu ya Kikristo yako katika sehemu mibili: Tunapaswa kuamu7a kukataa hizo mila na desturi ambazo ni mambo ya wanadamu yaliyofanywa iili kuipinga Injili na jambo la pili, tunapaswa kuzikubali mila kama hizo kwamba zinatoka katika Injili na hisyo zinafaa.

Pia, Mila nyngi na tamaduni nyngi ni kama ziko katikati kwa maana ya kwamba si mila mbaya kwani zimekuwa zikifundihwa na wazee wetu toka kizazi hadi kizazi.

Maana:Mila ni nini? Neno la kiyunani lililotumika katika agano jipya linaitwa “*paradosia*” Ni muunganikano wa maneno mawili - *para*=juu ya au zaidi ya & na aneno la kiyunani - *dokeo*=kutoa. Kwa hiyo “*Kujitoa kwa*” Hii ndiyo maana ya msingi inayoeleza maan ya neon Mila. Ni mawazo, mienendo, imani, hadithi na tabioa za kitamaduni ambapo0p kundi “*Hujitoa kwa*.” Wanashikilia kuwa ni kweli kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Ni mila za wanadamu, baadhi ni zakikabila, zingine ni za kitamaduni (kabila nyngi zinafanya utamadamu wa kufanana), zingine niza kidini; baadhi niza kiovu na zingine za kipepo.

Mfano: katika Yohana 13 ni hadithi ya Yesu akiwaosha miguu wanafunzi wake. Haikumaisha kwamba iwe desturi bali ilikuwa ni kielelezo cha utumishi. Hata hivyo sasa kuna makundi ya kikristo ambayo yamejenga mafundisho, mfuno wa maisha na kuwa sehemu ya mfuno wao wa desturi ya maisha katika kuishi. Mji wa Kentucky kuna “Wabatisti wanqaooshana miguu.” Wamefanya swala la kuoshana miguu kama sehemu yao ya ibada ya kila siku.

Kukaa kiutamaduni au Kuishi kulingana na Utamaduni

Changamoto kwa mwanatheologia yoyote wa biblia au mwanafunzi ni kule kujua nini maana ya “*Kuishi kiutamaduni*” na nini maana ya “*Kishi kulingana na Utamaduni*.” Kwa kuafnya hivyo anaweza kuondoa mila zisizofaa katika kanisa na kuhifadhi takmaduni za kimungu zinazolibariki kanisa.

Tazama Marko 7:1-15 & Mathayo 15: 1-20

Marko na Yohana zinaonesha matukio katika maisha ya yesu ambapo anakutana na mila za dini za Kiyahudi ambazo ziliikuwa zimeiziba kweli. Mafarisayo walishikilia mila zao (tafasiri) juu ya amri za Musa. Walizingatia sana sheria za Musa kuliko kata sheria za Mungu. Katika **Marko 7:13** Yesu akawaambia, “*Huku mkilitangua Neno la Mungu kwa mapokeo yenu mliyopokeana tena mwafanya mambo mengiu yaliyo sawa sawa na hayo.*” Waliyafanya, na tunaendelea kuyafanya! Yesu alikataa mapokeo kama hayo na tunapaswa kufanya vivyo hivyo. Tunapaswa kujua ni mambo yapi yamekaa kiutamaduni na yapi ni ya kweli ya milele. Tunapaswa kuelewa mambo ya kuishi kulingana na Neno la Mungu katika kizazi au utamaduni wowote.

Swali: Ni mila gani kanisa limezipokea ambazo tumezishikilia kuliko hata Injili. Ni Mila gani ambvazo “Tumeziongeza” kwenye injili ambazo zimebadili habari njema na kuleta habari mbaya zilizotengezezwu na wanadamu? Tunapoangalia kwa makini sana kuhusiana na swala mila na desturi na hata zile za mila za kimadhehebu tunapaswa kuwa kama Yesu tuchague kipi tuhifadhi.

Kuna maadhi ya mila zinaweza kuisaidia injili kusambaa na zingine zikasababisha Injili kutokuenea.

Mchanganuo utakaopelekea kuijua thamani katika Utamaduni au mila:

Mchanganuo #1-Mila hizi zilitoka wapi? Chanzo chake ni nini?

maelezo: hii ilikuwa ni njia ya yesu na mitume kuhusiana na mila. Yesu alianza mafundisho yake ya mapokeo ya mila kwa kusema, “*Mmeshasikia imesemwa kwamba ...laini mimi nawaambia ...*”

Yesu kama neon lililo hai la Mungu alijua tofauti ya Mila zinazofaa na mila zilizotengenezwa na wanadamu zinazoharibu kweli au zinazoongeza mambo Fulani katika kweli.

Mfano wa Kristo Kuhusiana na Mila:

1. Aliitenda sheria ya Mungu- Hakuna aliymshitaki kwa kuivunja sheria ya Musa.
Yesu aliheshimu kwakujua kwamba zimetoka kwa Mungu kwa ajili ya Musa.
2. Alipinga na kukataa sheria za kiyahudi Mishnah (Sheria 613 za Talmudic za Rabbis)
Yesu hakukubaliana na tafasiri za Kirabi za kiyahudi kuhusiana na sheria , na mara zote alikiuka sheria zao ili apate kuwfundisha ukweli.
3. Yesu alitupatia agano jipya ili kukamilisha agano la kale na kututengenezea mila mpya ili kanisa lake liweze kuishi kwazo.

Mfano wa Paulo Kuhusiana na Mila:

1. Paulo alikuwa ni rabi aliyeelimika na amesoma sheria . Tazama **Wagalatia 1:14**
“name niliendelea katika dini ya kiyahudi kuliko wengi walio hirimu zangu katika kabilia yangu nikajitahidi sana katika kuyashika mapokeo ya baba zangu.”
Kama myahudi aliyejitoa kikamilifu kuitunza sheria na mapokeo ya watu wake.
2. Paulo ilibidi atathmini mapokeo ya utoto wake kwa nuru ya Injili na akaanza kuzikataa mila hizo kulingana na Injili.
Hakutaka kuwatwika watu wa mataifa mila za kutahiriwa, vyakula na hata sherehe n.k. ambazo zilikuwa ni kawaida ya wayahudi .Tazama **Wakol. 2:16-23**
2. Paulo alifuata mfano wa Kristo katika kuweka mapokeo mapya yaliyokuwa yamejengwa katika Injili. Mafundisho na mila zake zikawa ni desturi za kanisa.
“*Basi ndugu simameni imara mkayashike mapokeo mliyofundishwa ama kwa maneno ama kwa waraka wetu.*” **2st Wathesalonike2:15;** *halafu tena anasema,*
“*...Jitengeni nafsi zenu na kila ndugu aendaye bila utaratibu wala si kwa kufuata mapokeo mliyoyapokea kwetu.*” **2st Wathesalonike 3:6**

Muhitasari wa mchanganuo #1- Injili inapohubiriwa kwa ufasaha na mtu akaiishi inaleta mapokeo mazuri sana yanayopelekea injili ienee. Pia itaweka wazi mapokeo ya uongo na yasiyofaa yanayoizua Injili. Sisi leo tunapaswa kufanya kama Wakristo na kile mitume walifanya – Kukataa mapokeo ambayo yanaizuia Injili na tushkilie mapokeo yanakayoifanya Injili ienee.

Mchanganuo #2- Mila inatoka kwa Mungu au imefanywa na wanadamu ?Paulo analieleza kanisa la Korinto “*Mmeyashika yale mapokeo vilevile kama vile nilivyowatolea.*” **1st Kor. 11:2**

Maelezo: Paulo alifka Koritaho na akaokoa wengi wakamfuata Kristo na akaanza kuwa fundisha Injili (mafundisho) na maelekeoz mengi (mapokeo). Baadhi ya yale mapokeo ilikuwa ni kuitunza Meza ya Bwana. Kutunza meza ya bwana ni mapokeo ya Kikristo. Yesu

aliwafundisha wanafunzi wake kukutana na kula kaqma njia ya kumkumbuka na mauti yake pale msalabani.

Kanisa la kwanza lilikuwa na mapokeo mengi mazuri na liliyapata kutoka kwa Yesu na mitume wake. Mapokeo haya yalikuwa ni maelekezo kuhusiana na mambo mengi kama chakula, sikukuu, wazee, sera za kanisa na tabia mbalimbali ndani ya kanisa. Mitume walikuwa wamekwisha kusimika destri zinazoitwa “**KUISHI KULINGANA**” katika vizazi vyote. Waliyaondoa na kuyakataa mapokeo yaliyoitwa “**KUKAA KIUTAMADUNI**”.

UTENDAJI:

Kila kizazi cha mkristo kina paswa kuhifadhi mapokeo yake. Tumekuwa tukifanya mfumo wa mila kuwa ndiyo mfumo wa kuishi? Huu ni upotofu mkubwa. Wayahudi walifanya hivyo na kujikuta wamemkosa masihi kwa sababu ya mapokeo yao.

Vielelezo: kanisa katika Koritnho lilishatkiwa kwa dhamira mbaya kwakuwa likosea meza ya Bwana. Badala ya kutumia meza ya bwana kumkumbuka Kristo na dhabihu yake aliyoifanya pale msalabani waliivuruga na kuifanya sherehe ya kula kunywa na kulewa.mapokeo yakabadilishwa maana na utendaji wake.

Wingi wa Sura za 1st Koritnho 11 zinahusika na kuwarekebisha kutoka katrika kuachga mitazamo ya mitume na kuingozsa matumizi yao mabaya.

Historia ya pasaka katika kanisa la Agano jipy

Tunapoangalia mabadiliko ya pasaka ya wayahudi tunaweza kuona ni kwajinsi gani mila zilibadilisha lengo na kuleta kitu kingine kabisa nje nay ale makusudio ilivyokuwa imeanzishwa.

Kuitunza pasaka lilikuwa ni agizo la Mungu alilopewa Musa ili kukumbuka jinsi Mungu alivyowakomboa taifa la Israeli kutoka Misri utumwani. Waisraeli waliambiwa waweke damu katika milango ili malaika wa mauti apate kuiona damu “na kuipita nyumba hiyo.” Wamisri ambao hawakuwa na damu hawakupona hata kidogo watoto wao wa kwanza walikufa na hata motto wa farao.

Hii pasaka ikawa ni mila ya Wayahudi na ikawa inasherekewa katika nyumba za wayahudi. Ilisherehekewa katika chakula na waliweka aina mbalimbali za vyakula vyenye sura mbalimbali zilizowapelekea kumkumbuka Mungu wao aliyeaokoa kutoka katika nchi ya Misri. Ilikuwa ni aina hii ya chakula am,bayo yesu alikuwa pamoja na wanafunzi wake usiku ule aliosalitiwa na Yuda.

Mila iliyobadili

Yesu aliitunza pasaka lakini pia aliibadili milele. Aliondoa yaliyopita na kuweka yaliyopo na yatakayokuja. Aliwaabia wanafunzi wake kwamba ile pasaka ya zamani ilikuwa ni kivuli cha pasaka ya Mungu msalabani wakati damu ya mwanakondoo wa Mungu haitamwagwa tena katika milango, BALI KATIKA MSALABA WA MTI. Damu yake ita, mfanya Mungu apite asiiangalie dhambi tena. Kw ahiyo Yesu akabadili mapokeo ya Agano la kale na kuweka mapokeo ya Agano jipy. Akafanya “kumbukumbu mpya” na si kukumbuka tena pasaka ya Agano la kale bali tukumbuke dhabihu yake aliyoifanya kwa ajili ya dhambi za ulimwengu mzima.

Meza ya bwana ilipaswa kusherekewa kama kumbukumbu ya kifo cha Kristo na kufufuka kwake. Haikuwa na maana zaidi ya hiyo. Ilikuwa ni kumbukumbu ya Krsto na msalaba wake kwa niaba yetu. Baadae kanisa la Rumi likafanya chakula hiki kuwa katika neema iokoayo.

Kwakufanya hivyo mapookeo haya yakabadilishwa kwa maana ya Neema na hivyo mafundisho haya yakaongezwa katika Injili! Baadae hii ilifanyika kuwa ni mila iliyoharibika! **Utendaji:** Kila kizazi kinapaswa kutathmini historia ya mapookeo yake, angalia mapookeo yake, asili yake na faida zake. Mara zote utakuta kwamba mkazo uko kinyume na maandiko.

Ushauri wa Paulo kuhusiana na wanawake kuwa na nywele ndefu

Paulo anakuja na hoja kama za wanaume kuwa na nywele nzedu kama vile wanawake walivyo na swala la wanawake kufunika vichwa vyao wakati wa maombi . Desturi hizi zinamasharti lakini zinaweza kutufundisha kanuni za milele tunazopipata katika Injili.

Kanuni za milele za Paulo=Amri ya mungu kwa wanawake na wanaume ni kwamba mwanaume ni kichwa cha mwanamke na kunapaswa kuwa na utofauti na mna wanavyopaswa kuva na kuishi.

Kielelezo: kabilia la wamasai katika Africa mashariki lina mila zisizo za kawaida kwa vijana wa kiume kufuga nywele ndefu na hasa wanapotoka katika rika la uja kwenda utu uzima. Wanawake muda wote wanywele fupi. Nywele ndefu za hawa vija amba wanaitwa wamorani huwa ni alama yao ya utu uzima. Anap[okuwa amefikia utu uzima anakata nywele zake, na wazo kuui la hapo ni kwamba sasa ni mwanaume na si mwanamke!

Utendaji: Mungu ahwezi kuidhinisha kwamba mwanamke na mwaume wavae sawa kana kwamba wanajinsia moja. Hatupswi hata kubadilishiwa viungo vya uzazi, kubadilishana mavazi au kufanana.

Muhitasari wa Mchanganuo #2

Tunapaswa kujiuliza kwa haya mapookeo. Je mila hii inaeneza na kuishuhudia Injili. Ukikuta kwamba haifanyi hivyo basi hiyo ni ya wanadamu na inapaswa kukataliwa. Haya yalikuwa ni mafundiosho ya Yesu alipokutana na mila hizi katika kipindi chake. Wayahudi walikuwa wamechukua amri kumi na kuongeza Amri zingine 613 kwenye Amri za Mungu zile kumi! Mila zao0 zilikuwa katikati yao na Masihi wa Mungu.

Mchanganuo #3- Nini hamasihohililopo nyuma ya Mila na Desturi?

Maelezo: mapookeo ya Mungu mara zote hutuelekeza kwa Kristo na Injili. Mapookeo ya Mungu humpa Mungu utukufu! Hamasisho nyuma ya mila na desturi linakuwa ni zuri, safi8 na si la kibinagsi. Na hii inaeleza kwa nini Yesu alikataa kujionesha nje maana ni swala aliloniona kwa waandishi na mafarisayo. Walipenda sana kuonekana kwa watu wakifanya desturi za dini zao (mapookeo).

Haya ndiyo mazingira ya Mathayo **Mathayo 15** na **Marko 7**. Wayahudi waliwasumbua sana wanafunzi wa Yesu kwa sababu walikuwa hawanawi mikono kabla hawajala. Ni Yesu alivyokabiliana nao ni kuwakemea, “*Mwaikataa Amri ya Mungu mpate kuyashika mapookeo yenu.*”**Marko 7:9**

Utendaji: Mapookeo yoyote ya kidini yanayokutukuza wewe au yanayokufanya u8onekane kuwa wewe ni mtu wa dini sana mbele ya macho ya Mungu hayasitahili katika injili na yanapaswa

kukataliwa. Kwa nini iwe hivyo? Kwa sababu mwili (neon la Paulo katika kueleza dhambiz eu za asili) unaweza kuwa ni uovu au wa kidini. Mwili unaonekana kuwa ni mbaya au mzuri. Na haya yote yanaweza kuwa katika mwili wa mwanadamu kwa matendo mabaya na naweza kuva vazi la dini kama vile mafarisayo lakini bado akamuwa mwana wa Mungu! Ni huu mwili wa mafarisayo ambapo walijitahidi sana kumfikia Mungu kwa njia ya matendo. Haya ndiyo yaliyokuwa maisha ya rabi Sauli anayetuambia kwamba kabla hajamjua Kristo alikuwa ni “nasmi niliendelea katika diuni ya kiyahudi kuliko wengi walio hirimu zangu katika kabilia yangu nikijitahidi sana katika kuyashika mapokeo ya baba zanguu.” **Wagal 1:14**

Kielelezo: katika barua ya Paulo kwa Wakolosai anawahukumu wale ambao wanatafuta kutumia mapokeo kupata kibali kwa Mungu. Katika **Wakolosai 2:16-23** Anajalibu kuorozesha matendo mengi ya wale wanaotumia dini zao za mwzi, ibada za malaika, sherehe na sabato kama njia ya kuhesabiwa haki katika mwili mbele za Mungu.

Mila hizi zote zilishindwa vipimo hivi. Mila zetu za Kikristo zinapaswa kutohuna na Injili na kumtukuza Kristo.

Swali: Ni mapokeo gani siku hizi zinatumika katika kupata kibali kwa Mungu zaidi ya kumwamini Mungu kwa zawadi yake ya wokovu katika Kristo? Kila dini leo hii zinamapokeo ya wanadamu yanayobadili na kuharibu na kuikana Injili. Ni jukumu la muhubiri wa Injilki kuliona tatizo hili kulisahihisha na kuifanya injili ilishughulikie.

Muhitasari wa mchanganuo #3-Kila kinachoitwa mapokeo ya Kikristo kinapaswa kutathminiwa na kuangaliwa chanzo chake na hamasa yake. Ikiwa yatakuwa yaharibu neema, na kuweka matendo au kukataa upekee wa kujitosheleza katika msalaba – tunapaswa kukataa.

Mchanganuo #4- Je mapokeo au mila inahamasisha, inalinda na kuitetea kweli ya Injili?

Maelezo; Kuna baadhi ya mapokeo katika kanisa yanayoonekana kana kwamba ni ukristo laini ukiyaangalia kwa makini utakuwa yanachembe nyingi sana za upagani.

Mfano: Ubatizo wa watoto; Kumwabudu Mariamu, mafundisho ya pagatori, mafundisho ya Baraka na laana, siku hizi inaitwa “Injili ya mafanikio”na mapokeo mengi ambayo wanadamu wajifanyia ambayo hayaendani na maandiko.

Kielelezo: Mtazamow a tarehe 25 decemba kama Siku ya kuzaliwa Kristo inapaswa kujadiliwa, kupewa changamoto au hata kupingwa. Asili yake iko katika sikukuu za kipagani za Saturnalia, (the winter solstice), juma la kulewa, kubaka, kuandamana na haya yopte yalifanyika tarehe 25 Decemba. Ilikwenda hadi mwishoni mwa karne ya 4 kwamba Yohana wa Chrysostom akatangaza kuwa tarehe 25 itakuwa ni siku ya kuzaliwa Kristo. Siku kuu hizi mbili ziliunganishwa na kanisa la Rumi kuwavutia wapagani waingie kanisan! Kwa miaka kadhaa waumini wa Othodox walijua kwamba hii ni kweli na wakakataa kabisa kutenda haya. Katika

marekani Puritani alikataa kuwa Krismas si ya watu wasioamini” na pia ilizuiliwa katika miji mingi ya England kwa miaka mingi.

Utendaji: Ingekuwa ni mafanikio makubwa sana ikiwa leo hii Wakristo wangekataa ibada za wapani? Ingetokea nini kama wazee katika dini kubwa wanetumia vigezo ambavyo Yesu alivitumia katika Uyahudi? Vipi ikiwa viongozi wa makanisa wangeliweza kuhoji kuhusiana na Krismas? Kwa Kuuliza tu CHANZO CHAKE, HAMASA YAKE, NA UENEZAJI AKE WA INJILI au hata utendaji wa yenye kama yenye – Krismas kama tunavyoifahamu leo isingefaulu huu mtihani! Kama wachungaji wa kimarekani wangempinga Santa Claus as fable, na kumtanga Rudolph kama Muungu, na kuwaaambia watoto wetu wasijishughulishe asingefaulu njama zake. Alithubutu kutokuikataa Kristmas!

Kwakuwa wazi kabiusa, haitatokea kabisa. Biashara ya Kimarekani ina nguvu sana. Krismas imekuwa ni wkti wa Biashara mzuri sana kwa wale wanaofanya biashara wakati huu. Kitu cha kukumbuka kuhusiana na Krismas ni kwamba mapokeo ya Krimas katika Marekani yalianza kama swala la Kristo kuzaliwa au kuja kututembelea. Siyo leo! Yesu hakutukaribisha alipozaliwa. Matukio ya wale mamajusi leo hii hayapo na wala hayaruhusiwi katika serikali, maeneo ya wazi au mahali popote na jamii zetu. “Salamu za vipindi” zimeondoa “Heri ya krismas” katika ulimwengu wa Wamarekani. Yawezekana kanisa limeshap[oteza Krismas kabisa.

Muhitasari wa Mchanganu #4 Kila kiongozi wa kanisa, Askofu, na hata mchungaji anapaswa kuyahoji mapokeo ya utamaduni wake au dhehebu lake kwa nuru ya mwanga huu wa mchanganuo wa Biblia. Muhimu kuliko zote ni hii kanuni – mapokeo yetu yanahamasisha, kulindfa na kuieneza injili ya yesu Kristo? Ikiwa hapana basi azikatae hizo mila? Je anachangamoto ya kimaandiko ya kuipa changamoto mila hiyo?

Mifano ya tamaduni za kiafrika amabzo ziko kinyume na Injili ni hizi:

1. Kudumishga uchawi au kuunganisha uchawi na Imani ya Kikristo.
2. Kuomba mababu waliokwisha kufa
3. Kutunza na kutumia hirizi katika majumba
4. Utamaduni wa wanaume kutotaka kuwaelimisha wanawake au kuwashudumia kwa utu.
5. Wake wengi
6. Tohara ya wanawake
7. Mifumo ya kipendekoste kama vile kuomba kiroho na ambo mengine ambayo yanapaswa kupimwa katika maandiko.
8. Chochote na yote yaliyokuja katika kanisa la kiafrica kwa njia ya mafundisho ya kidini, kama vile utume na namna ya kumtii Kristo.

Hitimisho:

- Hebu tukumbuke kwamba mapokeo au mila siyo Injili lakini yanaweza kuisaidia Injili.

- Usifanye kama walivyofanya wayahudi – Itathimini mila kwa kuipima na “Sheria.” Mapokeo yanaitumikia Injili na si kitu kingine.
- Kubali changamoto ya kufanya kama Yesu na Mitume walivyofanya – Tumia miongozo hii kwa kila mapokeo katika kanisa au jamii yoyote.

Baraka, Laana na Injli ya Neema

Utangulizi:

Mfundihso yaliyozoleka kabisa ya madhehebu na ya Kikristo na Wachungaji wa Kikristo ni yale mafundisho ya agano la kale ya Baraka na Laana. Japo kuwa mafundisho haya yako katika agano la kale lakini ni kivuli cha kile kilichotimizwa na kazi ya Kristo pale msalabani. Yesu Kristo alifanmyika laana kwa ajili yetu pale msalabani na matokeo yake ni kwamba hakuna Baraka nje yake yeye na hakuna laana tena kwetu kutoka kwake. Kwa sababu kuna halki kubwa ya kutokuelewa maandiko haya yafuatayo ni maelezo yanayoonesha ukweli wa kweli hizi za Biblia.

Tii, Utii

Kile kilicho katika wazo la laana na Baraka ni swala la kutii na kutokutii. Katika “Agano la Kale” liko karibu sana na neno “Kusikia”. Kutii ni mwitikio sahihi wa kukubali sauti, mwito au neno la Mungu. Katika wazo la Agano la kale ni kwamba waweza kusikia sauti ya Mungu au Neno La Mungu na usitii kile anachokikusudia. Mungu anaposema unategemea “Kusikia” au kutii. Hii inaeleza kwa nini neno Kutii katika Kiyunani kwenye agano jipya linamaanisha, “Kusikia kwa hali ya juu.” Kwa hiyo kusikia Neno la Mungu ni kutii neno la Mungu . Pia katika Agano la Kale hakuna neno kutokutii bali kunaneno “Kukaidi” au “Kuasi” ndiyo yametumika.

Tumaini na Utii

Katika Agano la Kale Kutii kabisa kumeunganishwa na unyenyekevu wetu na tumaini lisilo na masharti la agizo la Mungu. Huu muungsnikano wa Kutumaini na kutii ulianzia katika bustani ya Edeni. Hapo tunaona Adamu akiishi katika matumaini kamili katika Mungu katika kumpatia mahitaji yake yote. Adamu aliishi kwa furaha na baba yake akintumainia Mungu na kumpenda Mungu. Tunamwona kwa unyenyekevu akumfurahia Mungu. Adamu na Eva waliona kiwango kikubwa cha ukuu wa Mungu katika kumpenda kwake na kuhusika. Tumaini hili kamili lilionekana katika utii wao kwa yale ambayo Mungu aliwaomba wafanye. Kabvla hawajaanguka mahusiano yako ya mwanzo kutumaini na kutii kwao ilikuwa ni kielelezo kikubwa katika mkaisha ya mwanadamu.

Hili ni somo kwetu sote. Kutokutumaini ni mlango wa kutokutii. Nyoka alipokuja kwa Eva lengo lake ilikuwa ni kuleta kutokutumaini ukuu wa Mungu. Silaha yake ilikuwa ni mashaka. Anataka tuwe na mashaka na kupoteza matumanini ya kwamba Mungu ni nani. Shetani mara zote anataka tusitumaini ukuu wa Mungu, huruma ya Mungu au shauku zake juu yetu. Tafakari juu ya hili. Adui akikupata na kukufanya usitumainie ukuu wa Baba ujue utajaribiwa usiwe na matumaini na usitii. Kwa Nini? Kwa sababu kama Mungu hana Nguvu zote kwa hiyo hawezi katuongoza. Hawezi kubadili hali ya michanganyiko iliyo katika maisha yetu. Shetani mara zote anajaribu kututoa katika kumtumaini Mungu. Kama hutatumainia huruma yake, utaanza kumchakachua kwa kuingilia nguvu zake. Na mwisho Shetani ataanza kutujaribu kuwa na mashaka juu ya shauku za Mungu alizo nazo kwa ajili yetu. Adui anatuambia kwamba Baba alishatuacha, na

kabisa hashughuliki na mambo ya mwanadamu. Hana shauku wala makusudi kwa ajili yetu. Tunapoanza kuamini uongo huu tunakuwa hatumtumaini Mungu kutawala maisha yetu. Anachotuachia ni ule uchakachuaji kwa kutumia utii wetu kama silaha ya kumwendesha yeye kwa namna Fulani.

Imani na utii

Katika maandiko wazo la kumtumaini Mungu ni pana na limetazamwa kama “kuamini” Mungu. Imani na utii yanahusiana kwa ukaribu sana. Mfano mzuri wa kuamini unaoleta utii ni ule wa Ibrahim katika mwanzo 15. Ibrahim ana miaka 99 na mke wake Sara ni tasa. Mungu anamwambia Ibrahim kwamba Uzao wake utakuwa mwingi kama nyota za angani. Ibrahimku aliposikia maneno ya Mungu maandiko yanasema, “*Akamwamini Bwana naye akamhesabia jambo hili kuwa haki.*” (**Mwanzo. 15:6**) Paulo ananukuu mstari huu katika Warumi **Warumi 4:3** kuonesha kwamba kumwamini Mungu kumedhihirishwa na utii. Pointi ya Paulo ni kwamba utii wa Ibrahim ulitokana na imani yake (tumaini) katika Mungu.

Tunaposoma kwa makini kitabu cha Yakobo tunaelewa kwamba tumaini la kweli/ imani katika mungu huleta matendo mema. Imani hizi/matendo haya ni utii wa imani, tazama **Yakobo 2:26**. Imani katika Mungu inaleta utii safi.

Utii bila Imani

Tunachojifunza kutoka katika hili ni kwamba utii wowote tunaoutoa kwa Munguambao hautokani na Mungu wetu tunayemtumainia ni uovu. Unakuwa umejaa, ubinafsi, majivuno na kujitawala. Kwa huzuni kabisa Wakristo wengi wameendelea kutoa utii wa uongo kwa Mungu unaotokana narocho ya udini usio muheshimu Baba yetu wa Mbinguni. Kiukweli utii unaotokana na kutokutumaini umetengenezwa na dini za hapa duniani. Kutii ili umfrahirishwa Mungu, ili kupata kitu kizuri kutoka kwa Mungu au kumchakachua Mungu hakuwezi kuleta ushirika na Mungu.

Kutokutumaini na Utii usio kweli

1. Hofu kama Msukumo:

Kutii kwingi kwa Mungu kunatokana na kumwogopa Mungu. Inaonekana Mungu kama ni Gaidi aliye na shauku ya kutuadhibu na hawezo kutusamehe. Wale wanaotii kwa sababu ya hofu ya jehanamu au hukumu zingine kamwe hawajauona uso wa Mungu katika Uso wa Yesu Bwana wetu aliyeteseka. Tunapotumika kwa hofu ya kuhukumiwa, kunaonesha kutokuamini msalaba wa Kristo unaotufanya tuwe “sawa” katika macho ya Mungu.

2. Wajibu kama Msukumo:

Mtume Yohana Anawaelezea watu wanaodhani maagizo ya Mungu ni kama mzigo wa kutunza. Katika **1st Yohana 5:3**, anasema Amri za Kristo si “kitu cha kuhuzunisha” au mzigo mzito. Hizi dini zote tulizoijihararishia zinaangalia sana na kukuwekea alama nyingi juu ya siku zako zilizoenda vizuri na siku zako ambazo hazikwenda vizuri wakidhani utii ni wajibu au mzigo tunaopaswa kuubeba au kufanya kila wakati. Yohana nasema kwa kuwa tumekwisha kuona upendo wa Mungu katika Kristo amri zake si mzigo tunaopaswa kuubeba bali ni fursa ya kuonesha furaha yetu katika kumtumikia yeye. Utii unaotokana na Yeye kweli kabisa ni Utii wa Agano jipy.

3. Kushitakiwa Moyoni & Aibu kama msukumo:

Kustakiwa mopyoni na kuona haya ni kama ndugu. Vyote viwili ni vibaya! Unaposhitakiwa moyoni na ukashindwa kutekeleza kunaleta aibu. Kuona aibu ni kushatkiwa moyoni kunakofanya uharibifu. Kuna wakristo wengi sana mabyo wamekufa tayari ambayo utii wao ni kwasababu ya kushtakiwa moyoni na wamesukumwa kufanya kwa sababu wanahisi wameharibu upendo na Rehema za Mungu. Utii wao ni majuto, matabiko na umejawa na kujutia. Wanajua kwamba laana ya Mungu iko karibu tu kuwafikia.

4. Uchakachuaji kama msukumo:

Kuna waumini wachache wanaokiri kwamba wamejaribu kumchakachua Mungu lakini wako wengi sana wanamchakachua Mungu mara kwa mara. Kutokutuaini kwao ni kama mchezo uliochezwa kama hivi - "Mungu, Kama nitafanya hivi, umestahili na unatakiwa ufanye hivi." Naweza kumfanya Mungu anitumikie kwa kutii sheria Fulani Fulani alizoziweka. Kwa mfano; Wachakachuaji hutumia **Luka 6:38** kama sababu ya theologia ya Toa upate"". Wanafikiri kwamba wanaweza wakamfanya Mungu kama mashine ya bahati nasibu inayotekeliza kile wanachokitaka. Wanatoa (Utii) wakitegemea kupata zaidi ya kile walichotoa – zaidi ya mara mia. Wale anaojaribu uchakachuaji huu wanakwepana kabisa na maana ya mazingira ya kifungu cha Luka 6:38 ambayo ni kuwapenda adui zako, kuwaombea, na kuwafanya wengine kama wewe unavyopenda kufanya (**Luka 6:31**)

Bora kuliko dhabihu

Kwa mfano, Mungu alimwambia mfalme sauli baada ya kushindwa kutii kwa kutoa dhabihu za dini yake kama kitu kitakachosimama kwa niamba yake katika kutii sauti ya Mungu, "Je Bwana huzipenda sadaka za kuteketezwa na dhabihu sawa sawa na kuitii sauti ya Bwan? Angalia kutii ni bora kuliko dhabihu, na kusikia kuliko mafuta ya beberu. Kwani kuasi ni kama dhambi ya uchawi na ukaidi ni kama ukafiri nha vinyago kwa kuwa umelikataa Neno la Bwana ye ye naye amekukataa wewe nawe usiwe mfalme .

"1st Samwel 15:22-23.

Watu wa dini humpatia Mungu aina Fulani ya utii unaotokana na aibu, kuishtakiwa moyoni, wajibu, woga au uchakachuaji. Waislamu wa siku hizi ni mfano mzuri. Tafasiri ya sheria zao za kiiislamu (Sharia) zinawaambia kwamba kwa kupigana Jihadi wanaweza kumshawishi Allah awapatie Baraka ya wanawake wanawali katika paradiso. Wapigana Jihadi kwa ujinga kabisa huwa wanaamini Mungu anaweza kununuliwa kwa juhudzi za mwanadamu.

Wakristo wengi wamekuwa wakifanya kitu kile kile tunapofikiri kwamba tunaweza kupata Baraka kutoka kwa Mungu kwa kutoa zaka. Kile kinachoitwa "Injili ya mafanikio" inawaeleza mamilioni kwamba Mungu hukaa katika dhabihu zetu (Kutii bila kutumainia). Inasema kwa kutoa pesa unaweza kumpa Mungu rushwa ili akupatie pesa zaidi. Unaweza kutoa ili upate. Upande mwingine wa mafundisho haya ya uongo ni kwamba kama hautatoa au "hautapanda mbegu ya fedha" mlaji (laana) atakuja katika nyumba yako. Kwa hiyo utii ni uchakachuaji wa kuapata Baraka na kuepuka laana.

Baraka na laana.

Unaweza kuwa unataka kunikumbusha kwamba Agano la kale linatufundisha kwamba tuamini katika Baraka na laana. Mara nyingi tunaichukua **Mwanzo 12:3**, “*Nitawabariki wale watakaokubariki na kuwalaani wale watakao kulaani*,” kufundisha kwamba Mungu atawabariki wenzetu wale wanaoibariki Israeli sasa na kwamba Pia Mungu ataachilia laana juu ya wale wanaoilaani Isareli ya sasa. Sura nyingine ya Agano la kale inayotumiwa kufundisha Baraka na laana katika kanisa la leo ni **Malaki1 3:10, 11**. Tunaelezwa kwamba (na watu kadhaa) kwamba kutoa zaka inaleta Baraka za Mungu kwetu na kwamba kukataa kutoa zaka ni kumleta mlaji (laana) katika mafanikio yetu (Mazao). Je tunapaswa kuendelea kuamini kwamba hili bado ni neno la Mungu kwetu? Sidhani.

Ufunuo Endelevu

Wale wote wanaofundisha kwamba laana huja tu kwa wale wanaoshindwa kutii, wanapata theology zao kutoka katika Agano la kale na si Agano jipya. Na tatizo lao ni kushindwa kuelewa mahusiano yaliyopo kati ya Agano jipya na lile la kale. Wasomi wengi waliokomaa wanaeleza wazo la ufunuo

endelevu katika maandiko. Hii inamanisha kwamba Musa alijua zaidi sifa za Mungu, makusudi na mapenzi yake zaidi ya aliye tangulia Ibrahimu. Abrahamu hakuna na sheria, Mungu alikuwa na shria. Baadae manabii wa Israeli walipewa ufunuo wa Kusudi la Mungu kwa ajili ya Israeli zaidi ya kile alichokijua Musa. Walikuwa wakiruydia rudia shauku ya Mungu ya kumtuma Masihi atakayewaokoa wanadamu. Walijua zaidi ya Musa. Hata hivyo Yesu anajua zaidi ya Musa kuhusu Mungu kwa sababu ni mkuu kuliko Musa. Ni mkuu kuliko Manabii kwasababu alitimiza sheria na manabii. Yesu Kristo ni Ufunuo kamili na hatima ya ufunuo wa Mungu. Katika Yeye kuna utimilifu wa Mungu.

Laana katika Agano la Kale

Hii inatusaidia kujua ni kwa nini Baraka na Laana zimefundishwa katika Agao la kale zaidi ya Agano jipya..

Katika maelezo ya Agao la kale Mungu anatenda kusudi lake kwa ajili ya kuokoa na kurejesha kile kilichopotea katika bustani ya Edeni. Laana inakuja juu ya mwanadamu aliyetenda kosa kwa uasi wa Adamu. Kutokutii kunaleta ghadhabu ya Mungu na mara zote inaitwa “Laana.” Mungu anapofanya Agano na Ibrahimu anaanza kuonesha utii lakini anatahadharisha laana(kukosa kibali) kwa wale wanaoshindwa kutii. Halafu Mungu anampatia Musa sheria zake na anazikuza. Kiwango cha waisraeliu kilipimwa kwa sheria. Sheria ilijaa ahadi ili kuwabariki wale watakao tiina kuwalaani wale wasiotii. Baraka na laana hizi kanuni zake zinalenga zaidi kjwa watu wa agano la kale walioishi kipindi hicho cha historia chini ya sheria.

Laana katika Agano Jipya

Mtume Paulo anapokea ufunuo zaidi anapoendelea kufafanua kile kilichotokea kipindi cha kusulubiwa Yes- Masihi wa Mungu.

Yesu ni mwanakondoo wa Mungu ambaye kwa kifo chake na kumwaga damu yake kulisafisha dhambi ya ulimwengu (**Waefeso 1:7**). Akiliandikia kanisa la Wagalatia, Paulo anasema katika **Wagalatia 3:1-13** kwamba, sisi, watu wapya wa Mungu hatuko chini ya sheria na hukumu zake.

Anatuita wana wa kweli wa Ibrahimu kwa sababu tunaokolewa kwa imani katika dhambihu ya Kristo na hatuokolewi kwa matendo ya sheria (**Wagal. 3:7**). Tumebarikiwa pamoja na Ibrahimu, Muumini (**Gal. 3:9**). Halafu kwa ujasiri anatangaza kwamba tuko huru mbali na laana ya sheria: “*Kwa maana wale wote walio wa matendo ya Sheria wako chini ya laana. Maana imeandikwa amelaniwa kila mtu asiyedumu katika yote yaliyoandikwa katika kitabu cha torati ayafanye. Ni dhahiri ya kwamba hakuna mtu asiyehesabiwa haki mbele za Mungu katika sheria kwa sababu mwenye haki ataishi kwa imani. Na torati haikuja kwa imani bali ayatendaye hayo ataishi katika hayo. Kristo alitukomboa katika laana ya Torati kwa kuwa alifanya laana kwa ajili yetu maana imeandikwa amelaniwa kila mtu aangikwaye juu ya mti. Ili kwamba Baraka yta Ibrahimu iwafikilie mataifa katika Yesu Kristo tupate kupokea ahadi ya Roho kwa njia ya Imani.*”

Ni tangazo la furaha sana “*Kristo alifanyika laana kwa ajili yetu.*” Kumbuka laana inaondolewa kwa wale wanaomwamini Yesu kwa kazi aliyoifanya. Kwa sababu tuko “ndani ya Kristo” laana zetu, kutokutii na dhambi ziko msalabani na Yesu na tumewekwa huru na na sheria na laana. Hakuna laana kwa waumini, ni Baraka tu.

Hatutunzi alama ztulizofanikiwa

Hii inamanisha kwamba kwa waumini walio katika Kristo Mungu haangalii “kupata” (deni) liliwekwa kwa Yesu mabegani na kupelekwa msalabani. Ile barua ya kufaulu au kutofaulu kwako imajaana imeshalipiwa yote kabisa. Sasa hebu tafakari hii ni ngumu sana kuweka “alamza kupata au kutokupata” na mtu ambaye ambaye hatunzi kufaulu au kutokufaulu kwake! Kwa hiyo kila utii ninaoufanya kwa Mungu unaotokana na msukumo wakumfurahisha, kupata kitu kutoka kwake au kumfanya anipende zaidi ni ujinga na haufai. Utii wowote usiozingatia dhabihu kamili ya Yesu kristo kiukweli utaleta roho ya udini ambayo kamwe haiwezi kujenga ushirika na Mungu.

Ndani ya Kristo au Chini ya Sheria

Kwa hiyo tuko huru kuamua, tunaweza kuwa huru katika Kristo au kuwa katika vifungo vya sheria. Uamuzi ni wetu. Wale wakristo wanaoishi katika kushtakiwa dhamira zao, aibu au vifunga wanakuwa bado “hawajaamini” katika utii unaotokana na imani juu ya kazi aliyoikamilisha Yesu. Wanaishi kama waisraeli wa Agano la kale wanaohukumiwa na sheria. Wagalatia inatuambia kwamba kama tutatoa utii kwa Mungu ulio na msukumo wowote ili tupate kibali cha Mungu basi utii huo unaharibu neema.

Fikiri hivi – Sheria zote za agano la Kale zilitokana na kutokumtumaini Mungu, upendo wake na rehema zake zake. Hiyo imedhihirishwa na na amri kuu nay a kwanza ya Waisraeli katika

Kumbukumbu la torati 6:4, 5 “*Sikia, eee’ Israeli: Bwana Mungu wetyu, Bwana ni mmoja.*

Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote kwa Roho yako yote na nguvu zako zote.”

Huu ndiyo msukumo sahihi wa kumtii Mungu. Tunampenda kwasbabu tunampenda, tunamtumainia na tunataka kumpendeza.

Kipi unachagua – Sheria au Neema? Kristo au Musa? Baraka au laana? Huwezi kuwa na yote.

Watu waliogeuzwa

Kitu pekee kinachowabadilisha watu ni mtazamo wa mabadiliko katika msalaba wa Kristo. Kutunza amri kumi hakumbadilishi mtu, wanaweza kutulia kwa muida lakini haiwezi kuwabadilisha.

Upendo wa mungu ulipofunuliwa na kupokelewa ndipo ulipowabadili watu. Tunapokamatwa na Neema ya ajabu ya Kristo ndipo sasa tunaanza kuwatumika na kutii pamoja na kutumainia.

Ni kwa jinsi gani Mungu anatubariki?

Kwa kuwa hakuna laana kwa walio katika Kristo, sasa upande wa Baraka katika utii inakuwaje? Kwakuwa siwezi kutii ili kupata Baraka zaidi sasa Baraka zinakujaje kwetu? Hebu fikiri hivi – Kwa kuwa Mungu anabariki utii kamili hakuna hata mmoja wetu aliye haki. (**Warumi 3:10**)kile tunachoweza kumpatia Baba ni utii wa kawaida tu. Ambao unaweza kumkwaza motto wa Mungu yejote aliye na shauku ya kumpendeza Mungu. Mungu anamwana wake aliye mtoa utii kamili na kwamba katika mwana wake huyo wa pekee Yesu kristo. Alimpatia Mungu utii kamili kwani mara zote alimpendeza Baba . Kristo ndani yetu ndiye anaweza kutoa utii kupitia sisi.

Kile Mungu anataka hutupatia

Muumini anayetaka kumpendeza Mungu anapaswa kujua na kumtumaini kweli kwamba kile Mungu anachotuamuru kufanya alishatangulia kukifanya na kutupatia nguvu ya kukifanya ndani yetu na kutitia sisi.

Imenakiliwa katika Mathayo 12 kwamba yesu alikuwa katika sinagogi na akmwona mtu aliyejwa na mkono mlemavu. Akamwamuru mtu Yule “*Nyoosha mkono wako!*” (**Matt. 12:13**) Yesu alikuwa anamwambia yule mtu afanye kitu ambacho kwake yeeye kilikuwa ni kigumu kukifanya. Hata hivyo Yule mtu alitumaini lile neno la Kristo na akanyoosha mkono wake na mara ukaponywa. Kile Mungu anachokiamuru mara zote hutupatia na nguvu ya kukifanya. Maandiko tena yanatupa kwamba mwanaume ameagizwa kumpenda mke wake kama Kristo alivyolipenda kanisa. Hii ni moja ya maagizo ambayo ni magumu kuyafanya. Hakuna mwanaume anayeweza kumpenda mke wake kama Kristo anavyoweza kumpenda. Na ndiyo maana tumekaliwa na upendo wa Yesu ulioenea katika miyo yetu kwa niia ya roho wake Mtakatifu (**Warumi 5:5**).Kile Mungu anakitaka pia hutupatia uwezo wa kukifanya kwa neema yake. Mungu hawezi kutuambia kufanya kitu ambachop hawezi kutupatia nguvu ya kukifanya.

Yeye ni Baraka

Mwisho, Muumini aliyekomaa amesha tambua kwamba Kristo peke yake ni bora kuliko zawadi zingine zote, Baraka au vibali. Yeye ananifaa kuyliko hata vile atakavyo nifanyia. Baraka yangu kuu ni kwamba nipate kuishi katika ushirika na baba yangu wa mbinguni na kupata furaha yake kwa kuwa mshirika wake ili niweze kuleta ufalme wa Mwana wake mpendwa.

Utii wa Imani

Warumi 1: 5 & 16:26

*“... Yesu Kristo Bwana wetu ambaye katika Yeye tulipokea Neema na utume ili mataifa wote wapate kujitiisha kwa imani kwa ajili ya Jina lake. **Warumi 1:4-5***

*“Ikadhihirishwa wakati huu kwa maandiko ya manabii ikajulikana na mataifa yote kama alivyoamuru Mungu wa milele ili waitii Imani;” **Warumi. 16:26***

Utangulizi:

Maandiko yanadhihirisha ufunuo endelevu kuhusiana na mapenzi ya Mungu juu ya Utii. Kadri tunavyoendelea na wakati wa Mungu akifunua mapenzi yake kwetu tunaona aina ya utii unaomtukuza Mungu na dhabihu ya mwana wake kwa ajili ya kutotii kwetu.

Agano la kale

Utii katika Agano la kale umezingatia misingi ya hofu. Ni utii ili kuepuka ghadhabu ya Mungu na maonyo yake.

Kuna tatizo hapa; utii unaotoka katika kisima cha maji ya hofu au majukumu ambayo unayafanya kwa sababu ya hofu ikiisha hofu nayo unaacha. Hofu ni hisia lakini haiwezi kubadili moyo. Hofu inapokuwa imeondoka hofu inaoneskana.

Kielelezo: Ni kama utii wa motto mdogo unaofanywa kwa woga ili asije akamatika na kupigwa. Lakini anapokuwa mbali na wazazi motto anakosea kama kawaida. Hajaumiliki utii bado bali amemiliki hofu ya kuadhibiwa .

Jambo la pili, kumcha bwana kunaleta kushtakiwa kwa dhamira njema kunapotokea tumekosea. Katika Israeli hii dhamira siyo swala la mtu binafsi bali ilikuwa jamii nzima ilikuwa ikifikia taifa zama. Waliposhtakiwa mioyo yao ndipo walipoitwa “Watu wasio na utii.” Matokeo ilikuwa na jamii njema yenye maadili zaidi kipindi cha Musa. Lakini mikiki ya jamii huwa ni utii wa polisi.

Mwisho Paulo anasema katika wagalatia kwamba Mungu aliwapatia Israeli Sheria si kwa ajili ya kuwaokoa bali kwa ajili ya kuwatengeneza, lakini zaidi ilikuwa kwa ajili ya kuwaongoza kwenye kiwango cha juu kwa ajili ya utii wa imani katika kazi kamili ya Yesu kristo msalabani. (Tazama **Wagalatia 3**). Anasema unapaswa kukutana na Musa kabla ya kukutana na Yesu! Kiwango cha juu ya sheria ya Musa kitaonesha dhambi yenu na kuwaonesheni uhitaji wa mwokozi .

Agano Jipyä

Yesu anakuja na kuweka sura mpya kwa waisraeli wa Mungu. Anawatambulisha kwa baba mbinbguni. Baba yake ni baba katika Luka 15 anapoelezea habari za mwana mpotevu. Yesu anasisitiza utii na anaeleza utii kwa njia ya makombo ya nguruwe. Anajifunua kwa njia ya utii na mahusiano yake na Mungu maana alikuwa akitafuta kumpendeza Baba na kumpatia utukufu. Inaonesha utii wa imani na tumaini katika moyo wa Baba kwa upendo.

Nini hasa kinachowabdalisha watu na kuwafanya wamtii Mungu?

1. Je sheria na kanuni zinaweza kuleta utii?

Sidhani. Kiukweli tunaona kinyume. Unaweza kuweka tangazo katika shamba lako linalosema, “*Usitembee katika majani.*”

Nini kityatoka? Kitakachofanyika kila motto katika namna yake atajaribu kutembea juu ya nyasi ulizozua! Sheria inaweza kupunguza kasi lakini haiwezi kumbadilisha mtu. Sheria inaonesha ubinafsi wetu na dhambi zetu za asili lakini haiwezi kutubadilisha.

2. Je Neema ya Mungu + matendo inaweza kuleta utii?

Sidhani. Ni asili ya mwanadamu kutokuitegemea neema au upendo wa Mungu kana kwamba haitoshi. Tunajaribu kuongeza vitu kwenye msalaba wa Kristo. Kawaida yetu si kutoshelezwa na neema ya Mungu lakini kuongeza sheria na amambo mengine ya maadili tunahisi kwamba hiyo itakuwa ni uthibitisho wa kusudi jema. Wazo hili likuju mapema kabisa kabla ya kanisa la kwanza katika matendo 15. Paulo na Barnaba pamoja na ndiugu wengine walienda katika kanisa la Yerusalem kujadili swala hili la neema + matendo (utii). Baada ya mjadala mkubwa wa wazee wa Yerusalem waliandika barua kwa waumini wa mataifa inasema kwamba, “*hatupaswi kuwabebesha mizigo ninyi watu wa mataifa mbayo hata sisi wenyewe hatuwezi kuibeba.*”

(*Tazama Matendo 15:19-29*)

Hii ndiyo ilikuwa hatima yao kuhusiana na kumtumikia Mungu ili kupata kibali kwaq Mungu: “ikiwa utaongeza kitu chochote cha kwako ili kujipatia kibali kwa Mungu utakuwa unaiharibu neema ya Mungu.”

Kwa nini hili ni kweli?

1. Ni watii tu ndiyo wanaweza kumpendeza Mungu. Miaka ya 1990 hapama marekani vuguvugu la watu lilitokea likajulikana kama

Watunza Ahadi. Wakristo wengi wa kiume walihudhulia kongamano hili. Lilikuwa ni vuguvugu zuri lakini kwa namna Fulani walilikosea. Kwa nini? Kwa sababu tunaweka ahadi kwa Mungu kwamba hatuwezi kuiacha neema yake. Kufanya ahadi kwa Mungu ni jambo la ajabu kwa sababu tabia yake anahitaji utauwa na utii siyo tu ubabaishaji na ahadi ya utii. Ni Yesu peke yake aliyeweza kumpatia Mungu dhabihu kamili ya utii. Waembrania inatuambia kwamba Kristo alijaribiwa, akapimwa na kuteswa lakini bado alikuwa mtii katika m,ateso yake. (**Waembrania. 4:8**) kazi yetu siyo kumrukoo yeye au kumuiga bali kumwamini. Kazi yetu siyo kumuiga Kristo lakini kutumainia utii wake kamili kwa niamba yetu.

2. Uchakachuaji wa Kikristo

Kua aina nyingi za utii zinazotafuta kutawala au kumchakachua Mungu. Wazo ni kwamba tunawenza kutawala uungu kwa tabia zetu zinazojaribu kushughulika kwa ajili ya kupata kibali chake. Kwa hiyo kwa kutii watu wengine wanadhani kwamba wanaweza kubalansi Baraka na laana kutyoka kwa Mungu. Wanadhani kwamba Mungu anaubao unaoonesha kiwango cha kiasi gani mtu ajitahidi na kwamba wako malaika wamewekwa ambao kazi yao ni kutuma vema tunapo jitahidi.

Injili (habari njema) huwezi kupata vema kwa Mungu maana hatunzi kumbukumbu za vema! Msalaba wa Kristo ndiyo ubao wa alama wa Mungu. Msalaba unatulilia - “Deni limelipwa!”² **Kor. 5:21** inasema-“*Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye.*” Unaona hilo? Katika kristo tumeshatangazwa “wenye haki” kwasbabu haki ya Kristo ndani yetu ni kwakuitogemea kazi kamili (utii kamili) ya Kristo. Mtu mmoja alisema “wawezaje kupata vema kwa Mungu asiye na tabia ya kusahisha watu?”

Haiwezekani; kwa nini tunaendelea kujaribu, kufanya na hata kuchakachua ?

Utii wa Imani

Kama vile kitabu kinavyomaliza katika Kitabu cha warumi kanisa linaanza na “*Utii wa Imani*” (**Rum. 1:5**) na kinaishia na “*Utii wa Imani*” (**Rum. 16:26**). Tafasiri nzuri ya neon hili ni “Utii unaotokana na kutumanini Neema ya Mungu katika Kristo Yesu.” Ni utii unatokana na furaha ya kutumainia na kupenda neema ya Mungu. Ni tuii ambao imani inatoa. Katika **Warumi 1:4** Paulo anasema kusudi zima la injili ni kuleta “*Utii wa Imani*” kwa mataifa yote. Utii huu ambao imani inatoa ni Injili ya Mungu kwa watu wote.

Injili hii ya kumtumainia Mungu iko kinyume na ile anayotengeneza mwanadamu. Dini inamaana ya kujitegemea mwenyewe, hali utii wa kweli si kupata kitu kutoka kwa Mungu bali uamini kwa kile Mungu alichokifanya katika Kristo. Juhudi yoyote ambayo haimtegemei Mungu hiyo ni uovu. Uovu ni nini? Kwa sbaabu ni utii ambao umejengwa katika UBINAFSI na hamasa binafsi. Utii wowote ambao haumwamini Mungu na wema wa Mungu, neema na rehema mara zote utatengeneza dini. Hgaitaleta ushirika na Mungu.

Maagizo na Kupatiwa mahitaji

Habari njema za injili ni kwamba Mungu anapoamuru utii wetu ujue tayari ameshafanya. Hawezi kutuambia tufanye hali ye ye ahajafanya kwanza.

Kwa mfano: Mungu anawaamuru waume wawapende wake zao kama vile kristo alivyolipenda kanisa akajitoa kwa ajili yake. Swali langu ni – Nani anaweza kuwa na upendo wa ajinsi hiyo? Siwezi! Kiukweli hata wewe huwezi. Bali kristo ndani yetu anaishi na kutupenda na anapenda kupidia sisi na hivyo tunaweza kuwapenda wake zetu.

Katika Injili ya luka tunaona mfano mzuri wa kutegemea/Imani. Yesu anaingia kwenye Sinagogi na alipokuwa akifundisha anamwona mtu ambaye anatatizo la mkono. Yesu akamwambia Yule mtu asimame na aje kwake (Mtu Yule akatii). Yesu anawaamuru “*Kumnyoosha mkkno na Yule mtu akafanya vivyo! Na mkono wake ukarudia hali yake na kupona*” (**Luka 6:10**) Angalia ile amri na utowaji wa ile huduma ya nguvu ili kitendeke kitu. Mkono wa Yule mtu ulikuwa umepinda hakuweza kuunyosha lakini alimtumaini Kristo na alifanya kulingana na vile alivyoambiwa kufanya nay eye akafuata na kutii.

Hivi ndiyo vile utii uliojaa neema huwabariki wale wanaotii na kumbariki Mungu. Tunamtii Mungu kwa kuwa tunamwabudu na kumtegemea. Sisi ni wana wa Mungu wenyewe shauku ya kumpendeza.

Oswald Chambers huita utii, “ukuu wangu kwa ajili ya ukuu wake na ubora wangu kwa ajili ya uutukufu wake. “Tunapotenda dhambi (tunaasi) hatuna adhabu au kuaibishwa lakini tunakimbia kwa baba tukidai msamaha wetu na kumtumainia Mungu kwa neema yake ili kutufunika kutokutii kwetu.

Kuishi katika Neema kunaleta ushirika na baba na kunageuza majukumu na kuwa furaha. Kila agizo haliwi ni mzigo bali ahadi ya Baraka na ushirika na Mungu wetu baba yetu.

“Utii hauna “makusudi” huu utakuwa si utii wa Agano jipya. ” *Dudley Hall*

NI KWA JINSI GANI WAWEZA KUTAMBUA, KUTUMIA NA KUENDELEZA KARAMA ZAKO ZA KIROHO

Marudio:

1. kila uumini aliyezaliwa tena anakarama moja au zaidi za kiroho.
2. Karama ya kiroho ni uwezesho wa Kristo unaoupokea kipindi unapompokea Yesu Kristo ili ufanye kazi za Kiroho katika maisha ya kanisa na dunia.
3. Karama za kiroho si "upendeleo" au uthibitishio wa kuwa kiroho; zinaweza kutumiwa vibaya, kimwili au kishetani kabisa.
4. Kwa hiyo ni vyema tukajawa na Kristo ili apate katuongoza na kutuwezesha katika huduma zetu.
5. KARAMA ZAKO NI HUDUMA YAKO. Unapaswa kuwa wakili mwema wa karama zako.
(1st Petro 4:10)

A. Wakili ni mtu anayepokea kutoka kwa Bwana wake na kutunza kwa uaminifu wakati Bwana wake hayupo. Na baadae anapaswa anatakiwa kutoa hesabu pindi Bwana wake atakaporudi.

B. Tazama **Ist Petro 4:10**, inatuambia kwamba Mungu ameweka "*neema za huduma mbalimbali*" katika mikono yetu; wewe na mimi ni watawala wa neema ya Mungu! Kweli kubwa sana hiyo! Karama zako kiukweli ni neema ya Mungu halisi uliyowekewa uilinde na kuwa wakili mwema! Mkazo wa hapa ni kwamba siku moja kila mkristo atatoa hesabu ya matumizi ya karama zake katika kiti cha hukumu cha Kristo.

I. KWA JINSI GANI NAWEZA KUTAMBUA KARAMA YANGU?

Maelezo: Wewe ni karama. "Utu wako mpya" katika Kristo umeborteshwa na karama yako. Karama yako inakuhamasisha na kutawala mwonekano wako. Ikiwa umekuwa mwaminifu kwa Yesu katika mwenendo wako wa kila siku ujue umekuwa ukifanyia kazi karama yako haijalishi unaijua karama yako au huijui! Wewe ni karama yako! Karama yako ni wewe kama Mkristo uliyejazwa na Roho unafurahi unapotenda katika huduma ya ufalme. Si mpaka ujue karama yako ni nini ndiyo uanze kuifanyia kazi. Wakristo wengi wamekuwa wakimtumikia Bwana kwa muda kadhaa sasa bila kujua kwamba wanauwezesho wa kiroho! Zifuatazo ni njia za muumini kutambua karama zake:

A. **Kwa jia ya Kupenmdelea kufanya vitu binafsi** – Inaonekana kwamba Mungu anapokuwa amewapa “karama” watoto wake huwa pia anatoa karama moja ya hamasa. Karama hii ndiyo inayokusukuma sana na kuonesha matumizi ya kila karama ambayo muumini anaweza kuwa nayo. Paulo anatupa mfano mzuri wa hili. Paulo alihamasishwa kuwa kama “mtume kwa matraifa” hii ndiyo ilikuwa huduma yake – huduma ya utume. Neno mtume linamaanisha “mtu aliye tumwa kupeleka ujume.” Karama hii leo tunaiita umishonari; ni mtu anayekwenda katika eneo jipya na kuanza kazi ya Mungu mahali pale kwa ajili ya Mungu. Karama ya utume (Umishonari) inatakiwa itofautishwe na ile ya mitume ambayo ilikuwa ni ya kipekee (Watu kumi na mbili) na walichaguliwa na Yesu pekee. Paulo alikuwa na karama zingine pia ; unabii, kufundisha, hata miujiza; lakini karama hizi alizitumia katika utume wake aliokuwa kapewa kwa ajili ya Mataifa.

Maswali ya kujiuliza mwenyewe:

1. Ni kipi kinachokusukuma kama Mkristo? Kama n motto wa Mungu kibinafsi unajisikia nini na unahamasika kufanya nini? Karama zako zinathibitika kwa njia ya shauku ya kiroho. Ni “Moto unaonyoosha tumbo lako.” Ni kipi kinachokupa raha unapotumika katika ufalm,e wa Mungu?
2. nakushauri ujifunze karama mbalimbali za Roho. Tenga muda wa kuomba na kufunga. Tafuta uongozi wa Mungu akuoneshe huduma yako.
3. Unapofanya hili, utajisikia kama unahamasika kufanya kitu Fulani sana. Hili ndilo jawabu lako!

Hebu tufanye hivi baada ya kujisomea kmuda mrefu, umeomba na kufunga unaanza kusikia kana kwamba unasukumwa kufundisha. Ni kwa jinsi gani unaweza kuipima shauku yako?

B. **Kutambulika hadharani** – Ikiwa shauku yako binafsi inaongozwa na Mungu karama yako itaanza kuonekana hadharani kanisani. Yaani watu wataiona karama yako na kuanza kutamani kuitumia. Kutabulikana kwa namna hii kuko kwa namna mbili

1. **Kanisa litaitumia**. Kwa mfano unaanza kuomba nafasi ya kufundisha kama masomo ya Biblia, au kuwa na kundi la kujifunza Biblia n.k. halafu unaanza kujisomea na kufundisha. Kama hutapokea ushirikiano kwa wale unaowafundisha sasa huo utakuwa usuhuhuda wa wazi kabisa kwamba haujapewa karama ya kufundisha. Kama umepewa kufundisha kanisa litafurahia karama hiyo. Watu wataitafuta karama hiyo ili waitumie.

Kumbuka hili: Baadhi ya karama za kufundisha inaweza ikawa si “kuhubiri/kufundisha. Unaweza ukawa na huduma hii lakini ikakusukuma kujifunza neno la Mungu, kufanya utafiti au kuandika vitabu. Walimu wengine hawawezi kuhubiri lakini wanafundisha vizuri sana.

2. Mungu ataibariki karama hivo. Unapoipata karama yako na aunaanza kuitumia kutakuwa na upako na Baraka kutoka kwa Mungu; na hasa kama utakuwa ni Mkristo ulijejiachia na kujawa na Kristo kabisa. Roho wa Mungu ataithibitisha karama yako. Kanisa litaihitaji karama yako na Mungu ataibariki na kuikuza unapokuwa unaitumia karama yako.

C. Kujisikia vizuri mwenyewe – Njia nyingine ya kutambua karama yako ni kwamba kutakuwa na furaha unapoitumia karama yako. Kama kufundisha ni karama yako utapenda kusoma Biblia. Maandalizi ya masomo yako yatakuwa ni furaha na si huzuni. Utajisikia kutosheleka juu ya kazi uliyofanya na moyoni utajisikia kwamba kweli nimeiwakilisha kweli ya Mungu.

D. Ukiri sahihi – Pia kama huduma yako itakuwa ni ya Mungu kutakuwa na ukiri sahihi kwa sauti ya Mungu. Huduma yako italeta utukufu kwa Mungu na si katika mambo ya mwili. **Mathayo 7:22, 23** inasema, "wengi wataniambia siku ile Bwana Bwana hatukufanya unabii kwa jina lako na kwa jina lako kutoa Pepona kwa jina lako kufanya miujiza mingi ndipo nitawaambia dhahiri sikuwajua ninyi kamwe ondokeni kwangu ninyi mtendao maovu".

1. Hapa, Yesu anasema wazi kwamba si kila karama inatoka kwa Mungu! Watu hawa wanweza kuwa wamefanya unabii, kutoa mapepo, na miujiza lakini Yesu hakuwajua. Walikuwa ni watu waliopotea na karama zao zilikuwa ni za shetani.

2. Ikiwa karama yako itakuwa ni ya Mungu basi itatumika kwa ajili ya utukufu wa Mungu. **katika I Kor. 12:3**, inasema kwamba hakuna mtu anayeweza kumwita Yesu bwana hadi pale atakapokua amefunuliwa na Roho Mtakatifu. Ikiwa huduma ya mtu ni ya Roho Mtakatifu mara zote atamruhusu Yesu na ukweli wake. Karama zake, zitakapotumika vema zitamtukuza Kristo na si yeye Mwenyewe.

E. Kwa tangazo la Kinabii - Katika **1st Timotheo 1:18** na **4:14** kunamaelezo yanayofurahisha sana. Inaonekana kwamba Paulo au mtu mwingine aliyekuwa katika mamlaka alisema neno la kinabii kwa Timotheo. Baadae wazee waliweka mikono kwa Timotheo ili kumweka wakfu kwa ajili ya huduma. Wakati mwingine Mtu anaweza kutambua karama yake kwa njia ya unabii. Yaani mtu anakwambia huduma yako itakuwa ni nini.

1. Kipindi Charles Haddon Spurgeon alipokuwa ni motto kama miaka kumi na mbili muhubiri alimtembelea nyumbani kwake akamwambia Charles kwamba atakuwa ni muhubiri mkubwa siku moja. Spurgeon hakusahau hili na jambo hili lilitimia.

2. George W. Truett, mchungaji maarufu wa Baptist Dallas, Texas alikuwa anasoma sheria na kamti ya kanisa siku moja ili mwambia George kwamba Mungu amemchagua kuwa mchungaji wao japo kuwa George Truett hakuna na shauku ya kuwa mchungaji. Alitii wito na akwa mtumishi wa Mungu mkubwa sana.

Aina hii ya uthibitisho hutokea mara chache sana na lazima uwe makini kutambua. Unaweza ukakutana na kila aina ya watu wanaopenda kuwekea watu mikono wakiwaambia mpokee karama! Kuwa makini! Uwe makini kuruhusu watu kukuwekea mikono labda hadi uwe unajua maisha yao ya kiroho na mamlaka yao.

F. Kuwekewa Mikono: katika kanisa la kwanza alama au ishara hii ilimanisha yafuatayo:

1. Tendo la kuwekwa wakfu = kutengwa kwa ajili ya Baraka au wakfu
2. Tendo la kuthibitishwa = Idhinisho – Tunafanya hili kwa watumishi vijana na mashemasi
3. Tendo la Mitume = Kumtenga kwa ajili ya majukumu, huduma au kazi **Mdo 13:2, 3**
4. Tendo la mawasiliano = kukabidhiana nguvu za kitume, kuwasiliana na Roho Mtakatifu

II. NI KWA JINSI GANI NAWEZA KUITENDEA KAZI KARAMA YANGU?

Maelezo: karama zote mara nyingine zimekosewa katika matumizi. Hii imedhihirishwa na kanisa la Korintho katika karne ya kwanza! Haitoshi tu kujuua kwamba karama yako ikoje. Kunatakiwa kuwe na njia sahihi ya namna ya kuitumia karama yako.

A. *Kunatakiwa kuwe na kukubaliwa kunako faa kwa karama yako.* – Paulo anatufundisha vitu vinnee katika **Warumi 12:3-6** kuhusu kuikubali karama yako.

1. Huaswi kujivuna kwa sababu ya karama yako. – Mstari wa 3
2. Kunapaswa kutokuwa na hali ya kutokutosheka katika karama yako. – Mtari wa 4-6
3. Mungu amepima imani ya kutosha ndani yako kuhusu karama yako. - Msatri 3
4. Mungu amekupatia Neema ya kutosha katika huduma yako. - Mstari 6

B. *Kunatakiwa kuwa na tathmini nzuri ya karama yako . - Warumi 12:3*

1. hakupaswi kuwa na mtazamo wa kuijinua.
2. hakupaswi kuwa na mtazamo wa kushushana hadhi.

Karama zote ni sawa katika maho ya Mungu. Kila mmoja wetu anakazi ya kufanya na huduma ya kutenda.

C. *Kunapaswa kuwa na matumizi mazuri ya karama yako.*

1. Tumeambiwa katika maandiko tusikatae karama zetu. **Ist Timotheo 4:14**

2. Tumkeambiwa tushirikiana katika karama, kuufanya moto uendelee kuwaka!! **II**

Timotheo 1:6

3. Tumeambiwa kuwatumikia wengine kupitia karama zetu. **Ist Petro 4:10**

a. Si uwakili wema tunaposhidwa kutumia karama zetu.

b. Ni dhambi kutokuwa wakili mwema!

c. Inapaswa kutumika wakati wote the time! (Tendo “kutumika” katika kiyunani ni wakati uliopo = tendo linaloendelea)

D. *Kunapaswa kuwepo na marekebisho sahihi ya karama zetu.* - **Waefeso 4:16** inasema kwamba kila karama ielekezwe kwa Yesu. Kwa hiyo kila wakati unapotumia karama yako nje na uongozi wa Bwana Yesu Mungu ataikataa kwasababu itakuwa imekuwa ni kwa ajili ya matendo ya mwili.

III. NAWEZAJE KUENDELEZA KARAMA YANGU?

Maelezo: Zitumie chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu! Kuna sababu mbili za kwa nini Wakristo wengi hawaendelezi huduma zao : 1) Kutokuzitumia 2) au Kuzitumia vibaya.

A. Wakristo wengine wanashindwa kuziendeleza karama zao kwasababu hawako tayari kuzitumia kwa ajili ya bwana katika hudma ili wengine wabarikiwe. Karama zilizoachwa hukauka kama mguu usiotumiwa katika mwili wa mwanadamu.

B. Wakristo wengine wameshindwa kuziendeleza kwasababu wanazitumia vibaya. Kama tutashindwa kumruhusu roho Mtakatifu kutuongoza katika huduma zetu zinaharibika kwa sababu ya kutumiwa vibaya au kutumiwa kwa misukumo binafsi.

Hitimisho:

Mtafute Bwana jito kwake mwambie akufunulie huduma yako fuata kile kinachokuhamasisha, rejeshwa kwa jia ya watu walio nje yako na maonyo binafsi.

Theologia ya Somo la Mateso Kutoka Kitabu cha Ayubu

Utangulizi:

Mtu anayeweza kusimama hapa na kuelezea kwa ufasaha kitu mateso ni mtu Yule ambaye bado hajawahi kuteseka.

Mungu alijaribu kuelezea katika kitabu cha Ayubu. Ushuhuda wa Ayubu umedumu kwa muda kwani Mungu aliuvuvia na kuuhifadhi.

Kitabu cha Ayubu kinatuambia kuna mateso makali ambayo hata huwezi kuyaelezea. Kile unachowea kufanya ni kuinamisha kichwa na kumwachia Mungu yeze ndiye aelezee.

Kuna mateso magumu ambayo mtu anaweza kuishia kusema “anafanya mambo yote vyema.”

Utangulizi wa Ayubu:

Ayubu hakujuwa utangulizi wa historia yake. Aliteseka hakumjua Mungu na Shetani alipambana na roho yake! Mateso yake yalikuwa **kulingana na mapenzi ya Mungu**. Mungu alipenda.

Utendaji: Kunanyakati ambapo mateso yako yanakuwa hayana sababu isipokuwa Mungu anakuwa kayaruhusu! Unajikuta umekamatika kati ya Mungu na shetani. Kuna vita isiyonekana inayoendelea na WEWE uko kwenye huo uwanja wa vita!

Ayubu= anatufundisha kwamba watakatifu wanapokuwa wakiteseka huwa hawajui sababu ni kwa nini – ila anachojuwa ndani kabisa ya nafsi yake ni kwamba yote ni sawa tu!

Utendaji: Ayubu hakumsikiliza mshitaki wake. Walijua walikuwa wamekosea.

Ayubu= marafiki zake waliingilia kile Mungu alichokuwa akifanya katika maisha yake Ayubu. **Salimu amri!** Hakuna anayepaswa kuingilia kile Mungu anachoamua kukifanya ndani ya mtakatifu wake. Mungu anaruhusu haya yote yaingie katika maisha ya mototo wake kwa ajili ya uzalishaji wa chakula kitakacholisha ulimwengu!

Utendaji: Usiingilie maonyo ya watakatifu wengine.

Ayubu= Mungu wa Biblia ni Mungu wa mateso. Pale lile kasha lililoficha maisha yetu linapoondolewa tunaona yote kuwa ni siri na aibu, na nyuma ya hili tunachokiona ni Mungu anayejali, anayehusika na anayetabika pamoja na sisi. Moyo wa Baba yetu wa mbinguni mara zote umeguswa sana na mateso ya ulimwengu. Marafiki wa Ayubu walimbeza na kumshutumu kwa sababu walikuwa hawamjui Mungu na jinsi anavyoshughulika na mateso ya mwanadamu. **Matumizi;** katikati ya mateso, ni Mungu tu asiyetubeza. Yeye mwenyewe aliumizwa na kudhihakiwa na Watu, mtu wa huzuni na mwenye masikitiko makali.

Somo: Mateso si kwa ajili ya kutukamilisha. Sisi sote tunawafahamu watu ambao mateso yao yamewafanya wawe wakali na wasiotaka kuteseka tena.

Utendaji; Mateso yanawakamilisha tu wale wanaokubali wito wa Mungu katika Kristo. Kukataa na kuteseka kunaweza kukugharimu.

Mateso ni Siri ya muda-

Kama Ayubu hatujui yaliyojili (kile Mungu alikuwa akifanya) Tunamwona Mungu hayupo kimwili lakini katika ulimwengu wa Roho yeze alikuwepo katikati ya mateso hayo.

Utendaji: Kulikuwa na watu watatu katika msalaba – mwizi mbaya, mwizi mvumilivu na Mwana wa Mungu,

Wote watatu waliteseka ma kusulubiswa. Wote waliteseka lakini kwa makusudi tofauti.

Ayubu=Aliteseka mateso ya mwili – Lakini Biblia inaeleza mateso machache na haiyakazii sana.

Utendaji: Mila na desturi zetu huona mateso kama laana. Tunapoona Baraka na kufarijija tunaona kama ni kibali cha Mungu. Si hivyo. Maandiko yanasema “*Kwa sababu anayeteseka katika mwili amekufa katika dhambi.*” Kwa maneno mengine – Mateso ya mwili ni safisho la Mungu.

Uwazi wa Agano Jipyka kuhusu Mateso:

“Kama Mtu akiteseka kama Mkristo ...” 1st Petro 4:16

Somo: Dunia inapomuona mtu anakubali kuteseka kama Mkristo huwa inashangaa sana inaona ni ujinga na hatimaye inakerwa!

Kielelezo: Watu kama Mchungaji Youcef Nadarkhani wa Iran yuko jela . Mwezi wa October 2009 alishitakiwa kwa uasi na serikali ya kiislamu ya Irani. Alikataa kuikana imani yake katika Kristo. Na Pia Mwaka 2016 Mchungaji Saad Abidini ameteseka katika magereza ya Irani kwa zaidi ya miaka miwili kwa ajili ya maandiko haya. Kitu pekee alichotakiwa kukifanya ni kukana imani yake katika Kristo na kukubali kuwa Mwislamu. Lakini alikataa.

Utendaji: Kuteseka kama Mkristo inamaanisha kwamba kunautofauti mkubwa kati yako na dunia. Ni zaidi ya kutofautiana kimtazamo wa kimaandiko. Dunia hujaribu kuchukua nafsi ya ukuu kwenye utu wako – Yesu Kristo. Na ndiyo maana hawaoni sababu.”*hata kama wataniua – bado nitamkuza Yesu*” Roho ya dunia ya upinga Kristo ina kuwaga na mtazamo huo wa kikuhanu – Inawapa kuchukia na kutuona kana kwamba ni wajinga na wehu!

Kielelezo: Dunia ilimsulubisha Kristo msalabani - “aliokoa wengine, ajiokoe mwenywewe?” Wanachukua Theologia yetu na kuibadili kidogo, wanaivuruga & kuighoshi

Utendaji: Kuteseka kama Mkristo ni kukosa jibu kwa ulimwengu na hila zake. Ulimwengu ulimgeuka Kristo kipindi cha kusulubiwa kwake kwa kubadili maneno yake kuwa ni kufuru na kejeli. Watakufanyia kitu kilekile. Hakujibu lolote na wewe pia usijibu!

“Kama mtu akiteseka kulingana na mapenzi ya Mungu” 1 Petro 4:19

Kuna mateso mengine niya makusudi,na mengine yanazuilika. Kuna mateso mengine ambayo hayaepukiki na hayo yanatoka kwa Mungu.

utendaji: Mateso ya Ayubu yalikuwa ni yamakusudi – Mungu alirushusu. Mateso ya Yesu yalikuwa ya makusudi – Mungu aliruhusu. Mateso yanaweza kuwa ni makubwa na yautukufu pale moyo wako hautamwacha Mungu. Mtu hawezi kuwa katika hatari kama atakuwa yuko sawa na mapenzi ya Mungu!

Kielelezo: kama kusingekuwa na usiku hakuna ambaye angeweza kushukuru uijio wa mchana. Hakuna usiku–hakuna nyota, au mwezi kumulika giza.

Utendaji; Giza lako mara zote ni “*giza la hazina ya Mungu*” Isaya 45:3

Mateso yaliyo katika mapenzi ya Mungu si kwa ajili ya kukufundisha au kukukamilisha bali na fursa ya Mungu kuwaonesha wengine kusudi lake katika maisha yetu kwa njia ya mateso yetu. Kwa njia ya mateso tunafanyika chakula cha kuilisha dunia.

Utendaji: mapenzi ya Mungu kwako ili uteseke hayajaelezwa sana bali ni matokeo ya utii. Haiwezekani kuishi katika utii endelevu na usiteseke. Watu ambao hawajateseka katika ulimwengu huu bado wao hawajafanyika chumvi! Wanaume na wanawake wa Mungu walio bora huteseka na shetani hutumia mateso yao kumdhiihaki Mungu.

Utendaji: Kamwe usipende kuteseka! Huo ni ugonjwa wa dini za giza kama wale mazelote huko Philipi ambao walikuwa wakijiangika misalabani. Zaidi sana chagua mapenzi ya Mungu hata kama yanaweza kumaanisha ni mateso au kifo. Iache iwe ni “*Kulingana na mapenzi ya Mungu.*”

Somo: Mateso ambayo yameelezwa kuwa ni upotevu au utoaji wa vitu kwa ajili ya Mungu – hayana maana. Paulo aliyeteseka alipoteza vitu vyote =anaona kama ni takataka akilinganisha na faida alizozipata kwa kumjua Kristo. (Wafilipi 3)

“Ushirika wa Mateso yake” Mateso 3:10

Ushirika wa kweli katika maana ya Wakristo inamaanisha kushiriki kwa pamoja. Tunashiriki mateso yake tu pale mateso yetu yanakuwa ni kwa ajili Yake. Kufia imani, kufa, kwa rafiki zako, baba yako au mama ni sehemu ya ushirika wa mateso yake pale kupoteza huko kunakuwa ni kwa ajili ya ushirika wako na Kristo.

Utendaji: Kuwa makini na wale wanaokuhurumia katika mateso yako lakini hawana huruma na Yesu aliye nyuma ya mateso hayo kabla na baada ya mateso.

Unapoteseka- juu hili- Mungu anataka jambo moja tu katika maisha yako – analeta watoto wengi katika utukufu! Huwa hajali itatugharimu nini bali anajali kile kilichomgharimu pale msalabani. Mateso yako kama mtoto wa mfalme ni kushiriki pamoja naye ye ye aliyeseka kwa ajili ya mambo yetu.

Mungu alishachukua wajibu wadhambi na uthibitisho wa hilo ni msalaba. Ni Mungu anayeteseka si mtu anayetawala juu kwa jeuri yake bila kustahili.

Utendaji; Ni baadhi yetu wanaojua mateso kwa ajili ya Yesu. Watu wengine huteseka kwa aliji ya mkumbo, jamaa, mataifa au undugu. Wale tu walio katika ushirika wa karibu na Kristo wanaweza kwa hiari yao kuteseka kwa ajili ya Kristo

Shauku Ya Kitume

Utangulizi:

Sasa nataka tufikiri kuhusu “shauku ya kitume.” Yawezekana likawa ni neno ambalo hulijui. Shauku na Kitume – unapoyaunganisha maneno haya pamoja hakika utakuwa na kitu ambacho kinaweza kuvunja au kugeuza Dunia.

Nini maana ya Shauku ya kitume? Ninaiona imeelezewa wazi katika maneno ya Paulo kwa kanisa la Rumi na yameandikwa katika **Warumi 15:15-21**

“Lakini ninawaandikia kwa ujasiri zaidi katika sehemu za waraka huu kana kwamba kuwakumbusha kwa neema ile niliyopewa na Mungu. Ili niwe muhudumu wa Kristo Yesu kati ya watu wa mataifa niifanye Injili ya Mungu kazi ya ukuhanikusudi mataifa wawe sadaka yenyе kibali ikiisha kutakaswa na roho mtakatifu. Basi ninasababu ya kuona fahari katika Kristo yesu mbele za Mungu. Maana sitathubutu kutaja Neno asilolitenda Kristo kwa kazi yangu mataifa wapate kutii kwa neno au kwa tendo. Kwa nguvu za ishara na maajabu katika nguvu za roho Mtakatifu hata ikawa tangu yerusalem na kando kando yake mpaka iliriko nimekwisha kuihubiri Injilki ya Kristo kwa utimilifu. Kadhalika nikijitahidi kuihubiri Injili nisihubiri hapo ambapo Jina La Kristo limekwisha kutajwa nisije nikajenga juu ya msingi wa Mtu mwingine. Bali kama ilivyoandikwa wale wasiohubiri habari zake wataona na wale wasiojasikia watafahamu.”

Neno “**Utume**” linamaanisha “**mtu aliyetumwa akiwa na ujumbe**.” Ilikuwa kama mfalme anapotuma mtu akiwa na ujumbe wa mfalme. Mtumwaji alikuwa na sifa mbili tofauti:

1. mamlaka (Kwa sababu anafanya kazi ya Mfalme, anazungumza maneno ya mfalme kwa sababu yuko kwa niaba ya mfalme.)
2. Kipaumbele (Kwa sababu mfalme amemtuma ni kazi iliyokuwa na kipaumbele. Alipaswa kwenda na kuwakilisha ujumbe.

Neno “**Shauku**”= linamanisha “pathos” katika Kiyunani. Anawakilisha ujumbe kwa umuhimu, hisia na akiwa ameguswa moyoni. Katika agano jipya neno shauku linaweza kumaanisha:

1. Kutabika na=tazama **Matendo 1:3** inayosema yesu alikuwa hai baada ya shauku (mateso)
2. Inaweza kueleza hisia zako kali = Tazama **matendo 14:15** “...watu wa shauku”
3. Inaweza kumanisha msukumo mkali = Tazama Wakol **3:5** ...Uasherati, Shauku, tama mbaya.

Kwa hiyo, Kutohana na mtazamo wa Ki Mungu, Shauku yako ndiyo inayokufanya uteseke na kujitoa kwa ajili ya hiyo.

Kwa hiyo naiona shauku ya kitume ikitoka katika moyo wa Kristo. Siwezi kuipata hadi nimempata yeye! Tunaweza kujiuliza, “Nini kilichokuwa ndani yake hadi kikapelekea ateseke?” Soma Kitabu na utaona kwamba yesu alikuwa na ulimwengu yakiwemo na mataifa yote ndani ya moyo wake. **Math 24:14**-inasema kwamba Injili ihubiriwe kwa mataifa yote.

Math 28:19... Kwa mataifa Yote

Matendo 1:8-hadi mwisho wan Nchi.

Mungu anataka mwana wakeaabudiwe katika kila Lugha ya taifa au kabil.. Tazama **Ufunuo 4:4** kama wenye uhai wane na wazee 24 wanavyo mwabudu mwana kondoo! Wanatoka katika kila taifa na kutoka katika kwa watakatifu wa Agano jipya na la kale .

Baadhi ya maswali tunayopaswa kujiuliza:

Je shauku ya kitume kwa ajili ya mafia ilikuwa kwa ajili ya mitume tu? hapani, Si kweli. Katika Historia yote ya kanisa wanaume na wanawake wameshakamatwa na shauku ya kuyaambia mataifa kwamba “*Mungu alikuwa katika kristo akiupatanisha ulimwengu*”

Ni kwa jinsi gani waweza kujuua kwamba umekwisha kupoteza shauku hii ya Kitume?

Inadhihirika pale ndoto zangu za kimya na maombi yangu ya faragha yanakuwa hayatazami jina la Yesu likiabudiwa katika kila taifa, lugha na kabil. Mara nyingi kila mara muda wetu wa faragha na Mungu humwambia kile unataka na unahitaji na unakuwa hausikilizi moyo wa Mungu kwa ajili ya mataifa.

Inadhihirika pale unapokuwa unaimba kuhusu mbingu lakini unaishi kana kwamba duniani ni nyumbani. Unakuwa wa dunia pale unapokuwa unatawaliwa na “vitu.”.

Moyo wa kitume unakuwa hauko ndani yangu ninapokuwa najali sana mambo ya michezo, midoli, kutembea tu na kuona watu na sishughuliki kwa ajili ya watu wamjue Mungu.

Ninajua pale ninapokuwa siisikii ninapokuwa nikifanya maamuzi hata kama ni yahatari na bila kujali kama Kristo atatukuzwa katika hayo.

Ni kwa jin si gani waweza kujuua kama Paulo kwamba unatabika kwa ajili ya mataifa wamsikie Yesu?

1. Unapopanga kuondoka lakini unakuwa unatamani kukaa.
2. Unapokuwa unajisikia vibaya kwamba Mungu hajakuita uondoke uache hata mji wako na kwenda kuyafuata mataifa kwa ajili yake.
3. Unapokuwa hauko tayari kuteseka na kujitoa kwa ajili ya kitu Fulani. Unakuwa huna huruma nacho.

Ni Kwa jinsi gani naweza kuwa na shauku ya ndani kabisa kwa ajili ya waliopotea na mataifa?

Kwanza-Huwezi kuwa unaweka oda kama ya pizza au kupiga namba 100. Kujali kile Mungu anachokijali inahitaji muda na utendaji wa kazi ndani yako na Roho wa Mungu afanye kazi ndani yako.

Jambo la pili, Unapaswa kumjua ukae karibu naye unaweza kusikia sauti yake na ukawa tayari kutii kile unachokisikia. Baada ya Kile kilichomkuta Paulo akielekea dameski alijitoa kumjua Kristo. Alihitaji ufunuo zaidi na zaidi wa Kristo na kusudi lake hapa duniani.

Tatu, unapaswa kuamua –Hicho ndicho Paulo alifanya. katika **Warumi 15:20** anasema, “*Nikijitahidi.*”

Shauku ya Paulo ilikuwa ni kuwaeleza mataifa upendo wa Kristo. Aliamua kuona mataifa kwamba yanamwabudu na kumkusanyikia Mwanakondoo. Katika **Warumi 15:16** anayaona mataifa ya wayunani kama sadaka yake ya upendo kwa Kristo.

Mwisho, Unapaswa kutabiika kwa jili ya hilo, litafute kwa utaratibu na ufanye shauku ya kitume kuwa ni tabioa yako unayopendelea.

Amua sasa- Nitajali kile Mungu anakijali! Ninampatia Yeye maisha yangu! Walio ni watu hatari sana hapa duniani - ni wanaume na wanawake wenye Shauku ya Kitume!

Mahubiri na John Stott

Yamehaririwa na Josh Harris

1. Chagua Sura na itafakari.

- Soma sura, irudie tena na tena
- Yachunguze, yachambue, Chimbua, elewa kama ndivyo ilivyo.
- hujaitwa kuhubiri mawazo yako lakini umebadilishwa ili “uhubiri Neno” (2 Tim. 4:1-2). Clarence Edward McCartney: “weka Biblia yote kama unavyoweza.”

2. Jiulize maswali ya sura hiyo.

- Ina maanish nini? Au kwa uzuri kabisa jiulize ilikuwa inamaanisha nini pale kabisa ilipokuwa inasemwa au kuandikwa?
- Mwandishi alikusudia kujenga, au kuhukumu, au kuahidi au kuaagiza nini?
- Inasema nini? Ujumbe wake wa awali ni nini? Inamaanisha nini leo?
- Kumbuka: yatofautishe maswali haya lakini yawe pamoja—Ujumbe utakuwa ni safi na wamaana kama utaelewa makusudi yake katika mazingira ya leo. Huwezi kuelewa maana yake ya kwanza kama haujazama kuitafuta asili yake.

3. Omba ufunuo wa Roho mtakatifu.

- Muda wote unaposoma tamani sana ukweli wa mafunuo ya Roho mtakatifu. Kama Musa, “Ninaomba nioneshe utukufu wako” (Kutoka 33:18), na Samwel, “Sema Bwana maana mtumishi wako anasikia” (1 Sam 3:9).
- Stott: “Nimeona kuwa inafaa sana kuanda mahubiri yangu nikiwa katika magoti Biblia ikiwa mbele yangu kwa njia ya maombi.
- R.W. Dale: “kazi bila maombi ni kufuru na maombi bila kazi ni ufedhuli.”

4. Tambua wazo lililo na nguvu katika sura hiyo.

- Kila sura inakusudi maalumu, nakiri kusudi kuu.
- Mahubiri si hotuba yanamakusudi ya kufikisha jumbe muhimu
- watu wanaweza kusahau mambo yote ya ujumbe lakini wakakumbuka wazo kuu kwa sababu mambo yote ya mahubiri yanatakiwa yasadie watu kuelewa ujumbe na kuiona nguvu yake.
- Utakapokuwa umejua kusudi la sura iweke katika “kundi la pendekezo.”
- J.H. Jowett: “Ninashawishiwa kusema kwamba hakuna mahubiri yaliyo tayari mpaka tujue kusudi lake kwa ufupi, sentesi nzito iwe rahisi. Nimeshagundua kwamba kupata sentensi ni vigumu sana lakini ni moja ya faida na kazi nzuri sana katika kujifunza kwangu ...Kila hubiri

linalotakiwa kuhubiriwa ni lazima sentensi yake iwe imeeleweka na kuwa nyeupe kama mwezi usiozungukwa na mawingu.”

- Ian Pitt-Watson: “kila hubiri lazima liwe laini na limeainishwa katika kusudi lake.”
- Usikwepe maonyo ya kusubiri wazo kuu lililotawala lijifunue. Unapaswa kuwa tayari kuomba na kutafakari wewe mwenyewe kwa kina katika andiko hilo na hata chini yake mpaka usifikie hatua ya kujifanya unajua au mjanjamjanja bali kuwa mtumishi mtii.

5. Yapange masomo yako kwa kulitumikia wazo kuu

- Lengo si ujuzi bali mpangilio unaowezesha kifungu kiweze kuleta mabadiliko.
- tupilia mbali masomo yasiyoingiliana
- weka masomo saidizi ili kuonesha na kuisaidia wazo.
- Sheria za msingi kwa ajili ya mchanganuo wa mahubiri: Kiache kifungu kijitetee. Liache lijifungue lenyewe kama ua kwenye jua la asubuhi.
- Uwe sahihi na maneno yako. Haiwezekani kuhararisha ujumbe bila kujua maneno sahihi.
- maneno ya kutumia:
 - maneno rahisi na wazi . Ryle: “Hubiri kana kwamba unapumua.”
 - maneno yaliyojificha . yatajenga sura zisizo wazi katika ufahamu.
 - maneno ya kweli . Kuwa makini katika mafafanuzi na uwe ni mtu wa kujilinda katika matumizi ya vilinganisho.
 - C.S. Lewis: Usiwaeleze watu wajisikieje bali wahubiri watu wao wenyewe wajihisi kama walivyopokea.
 - Usitumie maneno makubwa kwa ajili ya somo.

6. Kumbuka nguvu ya Kufikiri—Elekeza!

- Kutafakari: Nguvu ya fahamu ambayohutunza vitu visivyoonekana inauwezo wa kuwakilisha vitu kana kwamba vinaonekana kwa wengine. (Mzinga)
- tambua kwamba wanadamu huwa ni wazito sana kupokea mawazo ya kudhania—tunapaswa kuyabadili na kuwa taswira na mifano.
- Wekeza nguvu zako kwenye vielelezo vinavyofafanua wazo lako kuu.
- weka vielelezo kama madilisha yaingizayo mwanga katika somo letu na uwasaidie watu kuona zaidi na kushukuru.
- Kuwa makini na mifano inayovuta hisia sana (kwao badala ya somo) au itakayowatoa watu katika kusudi kuu.

7. Ongeza tangulizi wako

- Ni vyema ukaanza na kiini ili kuepuka kuingiza ujumbe katika utangulizi.
- Stott: Utangulizi mzuri husaidia mambo mawili. Kwanza, unaleta mvuto, huamsha hisia, udadisi na hamu pia. Pili, Hueleza kusudi na kuwaongoza wasikilizaji kwenda kupokea.
- Usifanye utangulizi uwe mrefu sana au mfupi sana. “Watu wanatabia ya kujisahau na kuanza kueleza mengine. Jengo halifurahishi mara sana kama halina sehemu ya kufikia au sehemu ya

kuingilia.”

8. Weka hitimisho lako

- Hitimisho mara zote huwa gumu sana . epuka mzunguko usio na mwisho bila kutua. Pia epuka kutua ghafla.
- Hitimisho sahihi huambatana na jinsi ya kutenda. (Si kila utekelezaji usubili mwishoni—tkifungu kinapaswa kufanyiwa kazi kadri navyokielezea.)
- hata hivyo, ni kosa kuonesha hatima yako mapema sana, kama utafanya hivyo utapoteza mategemeo ya watu. Ni vizuri ukaendelea kuvuta kidogo. Na hatafu hatima ukaiacha kwa Roho Mtakatifu kwa ajili ya utekelezaji.
- Lihimize kongamano katika kutenda, mategemeo yetu tunapohitimisha ujumbe si kwamba watu waendelee kukumbuka au kuelewa au kufurahia mafundisho yetu bali watende. Ikiwa hakuna samasi basi hakuna ujumbe!
- matumizi sahihi ya ujumbe wako yanategemea sifa ya kifungu. Wazo kuu linatupeleka ni kwajinsi gani watu watende kwa mwitikio. Je wito ni watoba au niwakuwahimiza katika kuamusha Imani zao? Je inahamasisha ibada, utii, wito wa ushuhuda au ni changamoto za kuabudu? Kifungu chenyewe ndiyo hueleza mwitikio tunaouhitaji.
- Angalia aina ya kundi lako. Ni vizuri ukaiacha akili yako ikaliangalia kundi lililombele lina aina gani ya watu na umusih Mungu akuoneshe kila mtu anahitaji nini kutoka katika kifungu hicho. Angalia mahitaji yao ya kipekee, udhaifu wao, uimara wao na hata majoribu.

9. Uandike ujumbe wako

- Usichelewe kufika katika hatua hii ! andika katika karatasi, usiuchanganyechanganye (hili ndilo jaribu langu).
- Unapoandika unaweza kwenda kwa mpangilio.

10. Uhariri tena

- Unapopitia tena hugusa lengo (dakika 40-45) kama ilivyomuhimu kwa vitu vingine ambavyo hufanya. Kama utasema machache watu watatupilia mbali.
- Bila kujali ondoa mambo yasiyohitajika. Angalia ni sehemu zifi utasimamia sana.
- Punguza yasiyohitajika —na hasa nukuu ndefu.

11. Uombee ujumbe wako

- Tumia dakika 30 kabla haujaondoka kanisani kuuombea ujumbe wako.
- Stott: “Tunahitaji kuomba mpaka ule ujumbe uwe halisi kwetu, utukufu utuangazie, moto uwake ndani ya mioyo yetu na kuanza kuiona nguvu ya Mungu ndani yetu.”

Kuandaa Hubiri kutoka katika Neno la Mungu

Mahubiri ya Biblia ni ujumbe ambao mambo yake muhimu hutoka moja kwa moja katika maandiko kwa njia ya kutafakari. Huu ni Ufafanuzi. Wahubiri wengi wako kimafumbo zaidi hawafafanui yaani kuweka wazi. Wanasona neno Bila kutafuta kweli kutoka katika Neno hilo.

Mahubiri mazuri husikilizwa.. Dakika tatu muhimu muhubiri alizonazo katika miguu yake 1st Ni dakika tatu na Tatu za mwisho! Unadakika tatu za kuwavuta wasikilizaji wako waweze kukusikiliza vinginevyo hutawapata kabisa! Anza na utangulizi utakao wafanya wakusikilize. Utangulizi huu uwe unalingana na Kichwa cha somo unalokwenda kulihubiri.

Mahubiri mazuri ya kwenye Biblia yako wazi hayachanganyi kama yatafanyiwa mazoezi. Kila kipengele muhimu kitakachotokana na mstari unaosoma kitakuwa na vipengele vitatu:

1. MAELEZO
2. MATUMIZI
3. VIELELEZO

Kwa mfano: Ngoja tuchukue mstari rahisi wa Yohana 3:16

“Kwa maana Jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa mwana wake wa pekee, ili kila mtu amwaminie asipotee bali awe na uzima wa milele.”

Maandalizi: Jaribu kama unaweza kueleza hubiri lako katika sentensi moja. Kwa mfano ngoja tuliweke hubiri hili katika mstari unaoitwa, **Habari nzuri iliyosimuliwa**.

Sentensi Muhimu: Msitari huu unatueleza habari nzuri za mtu ajuaye kupenda. Upendo mkuu, zawadi kuu, na uamuza mkuu ambao ulimwengu umewahi kusikia.

Sasa waweza kutengeneza mchanganuo unaoeleza, na kutumia na kuelekeza kweli hizi.

I. Mpendaji mkuu...Kwa maana jinsi hii Mungu..

Maelezo: (Nani, Nini, Wapi, na jinsi gani ya ujumbe.)

Hapa ndipo unapojobu maswali ya msingi:

1. Iliandikwa kwa nani
Rejea katika Historia

Kwa nini Mungu aliwaambia

Nini ilikuwa maana yake?

Kumbuka: Yesu anayasema maneno haya kwa Nikodemo, Mtawala na kiongozi wa dini. Katika mistari inayoendelea Yesu anatumia kielelezo (Msati wa 14,15) cha Musa akimwinua nyoka wa shaba kule jangwani kuonesha msalaba kama udhihirisho wa upendo wa Mungu.

2. Sura inasema nini?

Ichunguze sura hiyo kwa kutumia tafasiri mbali mbali.

Rejea katika comentari

Angalia neno hilo katika rejea za Biblia

Fuatilia rejea hizo.

3. Ilitokeaje?

4. Inamanish nini kwetu leo?

Tafuta kanuni za milele katika mazingira ya kawaida. Katika mstari huu jaribu kuelezea vitu hivi. Elezea Mungu ni nani (1st Yohana 4:8.) kitu chochote kinachowenza kukuletea maana kiweke. Mungu ni wa haki, warehema, ni mwenye hasira n.k. lakini Mungu ni upendo na upendo lazima uonekane.

Matumizi: (haya maneno “Kwa hiyo katika ujumbe wako ”).

Baada ya maelezo tunakuja kwenye matumizi. Ni kama vile tu kwenye eneo la maelezo yaani *Nani, Nini na Wapi* katika mahubiri. Katika sehemu ya matumizi katika ujumbe muhubiri hueleza kweli za Kiroho kwa wasikilizaji wake. Hujibu neno ambalo halijaswemwa yaani “Kwa hiyo” kwa wasikilizaji. Anaweza kuuliza “nini mtazamo wako kuhusu Mungu?” Wakikuyu wa Kenya kwa miaka mingi wamekuwa wakimuita Mungu ni, “Mungo”, na wanaamini kwamba anaishi katika mlima Kenya! Muhubiri anaweza kusema, “Unajua kwamba Mungu ni Upendo?”

Matumizi hufanya ujumbe uwe maalumu sana. Yesu na Manabii wote walifanya hivi. Walieleza matumizi ya Kweli za Kiroho kwa wasikilizaji wao. Petro siku ya Pentekoste aliwageukia wale wayahudi walio muuwa Yesu na akasema, “Yesu huyu... *mkamsulubisha kwa mikono ya watu wabaya mkamwuua Na Petro akawaambia, “Tubuni...* (Matendo 2: 23-38)

Jambo muhimu hapa ni kwamba mahubiri lazima yawekwe katika matumizi ya kweli. Kama mtu ataondoka bila kujua Mungu anamwhitaji afanye nini yavezekana mtu hyo akawa hakuwa anasikiliza au Muhubiri hakufanya kazi yake vizuri.

Kielelezo: (Mtazamo “Madirisha ya ujumbe”)

Sasa hapa tunataka hadithi, picha itakayoutuonesha kweli. Vielelezo ni madirisha yanayoruhusu kweli ya Mungu kuingia katika roho zetu. Hata kama msikilizaji wako atasahau mahubiri yako anaweza kukumbuka hadithi. Yesu alilifahamu hili na akawa anahubiri kwa kutumia mifano ambayo wangeweza kukumbuka. Luka 15 ni mahubiri ya mfano. Anawaeleza mafarisayo habari za mtu aliyekuwa na wana wawili ili aweze kuwafundisha neema ya Mungu na upendo wake. Katika Yohana 3:16 Muhubiri anaweza kutoa mfano unaoonesha Mungu ni Upendo.

II. Upendo mkuu...Aliupenda ulimwengu...

Maelezo: Kun aina mbalimbali za upendo. Neno la upendo huu ni “Agape” yaani upendo usio na masharti. Ni Mungu pekee anaweza kuona makosa yako na mahitaji yako. Kwa sababu sisi tunashitakiwa na dhamiri za dhambi tunahitaji aina hii ya upendo. Hii ni neema kutoka katika moyo wa Mungu. Kumbuka kwamba upendo wa Mungu unaonekana katika maisha yote ya mwanadamu. Aliupenda ulimwengu wote, hakuacha hata mmoja.

Matumizi: Upendo wa Mungu umeshagusa ulimwengu wako? Mungu anaweza kukupenda na moyo wako ukashindwa kumgusa kwa sababu ya dhambi na kutoamini. Kuna shimo kubwa katika moyo wa mtu na ni Mungu pekee anaweza kulijaza shimo hilo.

Kielelezo: Sasa hapa tunahitaji mfano tena yaani dirisha litakaloruhusu mwanga upenye. Iwe ni hadithi nzuri, shairi, misemo au kitu chochote kinachoweza kueleza kweli hii.

Na inaendelea hivyo hivyo katika kila pointi, Maelezo, mtumizi na vielelezo. Ni mfano mzuri huu wa kuandaa Mahubiri kutoka katika Biblia.

Jambo Moja muhimu-Matumizi mbalimbali

Wazo la kukusaidia hapa. Si kila hubiri lazima liwe na mambo muhimu matatu, na wala si kwamba ni lazima liwe na mawili. Kuna mahubiri mengine huwa na wazo moja. Kwa mfano Hii Yohana 3:16 Mstari unaweza kuwekewa wazo moja tu likabebba mambo yote yaani, “Jinsi Mungu anavyowapenda kupita upeo walio potea”. Ikiwa utaamua kutumia pointi moja waweza kuzibadili sehemu zako hizo tatu kwa kutumia Maelezo, Matumizi na vielelezo kwa namna nydingine.

Unachanganya

Kuna wakati unaweza kutumia vielelezo viwili kwa pamoja, au maelezo, halafu kielelezo na matumizi. Unaweza kuyachanganya kama unahisi yataeleweka. Wasikilizaji wako na jinsi wanavyosikia inategemea wewe mwenyewe jinsi unavyowasiliana nao.

Kwa mfano: katika tamaduni za kiafrica watu wanapenda masimulizi. Kwasababu hili ni jambo la mila walilorithi. Na jinsi waafrika walivyo katika fahamu zao ni tofauti na mila za magharibi.

Kwa hiyo kama wanaokusikiliza ni watu wa Africa unapaswa kutumia hadithi nyingi na halafu ingia katika matumizi ili waweze kuitumia hiyo katika maisha yao halisi.

Waweza pia kutumia maelezo katika kutoa mamlaka ya Biblia katika vielelezo vyako na jinsi ya kuyaishi au matumizi.

Mwisho, Kila hubiri linahitaji liwe na mwisho yaani **hitimisho**. Mwisho au hitimisho ni pale unapowauliza wasikilizaji wako kupokea au kuchukua hatua. Nawaomba wafanye kitu kulingana na utii wa neon la Mungu. Hitimisho ni pale unapowaeleza wanapaswa kufanya nini. Unapaswa kuwa mfupi, unaowafanya waamue na ueleweke katika kile unachokieleza wafanye. Hatua hizi hutokana na hotuba zao, inaeleza kile ujumbe umekuwa ukieleza.

III.Hali halisi ...Ulimwengu

Eleza: Hapa unaweza kuwaeleza wasikilizaji wako kwamba Mungu anapenda watu wote, makabila yote, mataifa yote, wenyе dhambi wote-bila kujali rangi, kabilia, mazingira. Rejea katika maandiko ili kuuimarisha mstari huu. Tazama Warumi 5:8; Luka 19:10; Warumi 6:23; na mingine mingi.

Matumizi: Waeleze wasikilizaji wako kwamba waweza kuandika jina lako hapa. Mungu anakupenda sana kwamba hata akamtoa mwana wake wa pekee kwa ajili yako. Yesu akafa kwa ajili ya kukusamehe na wokovu wako.

Kielelezo: Sasa unawapa kielelezo kizuri juu ya wokovu huu kwa kutumia hadithi inayolingana na hoja yako ya wokovu.

Labda unaweza kutumia hadithi za mwana mpotevu katika Luka 15.

IV. Karama kuu... Akamtoa mwana wake wa Pekee

Unarudia tena hatua zilezile za Maelezo, matumizi na wakati mwingine kielelezo yaani mfano mmoja tu unahitajika bila maelezo mengi.

V. Sharti la Muhimu...Kwamba Kila amwaminie

Vi. Wokovu mkuu... asipotee bali awe na uzima wa milele

Hitimisho:

Hapa unatafuta mwitikio wa jinsi ya kufikisha habari njema. Kwa hiyo mwisho wako una nguvu katika matumizi. Hii ni “*kwa hiyo*” ya ujumbe wako. Katika hitimisho hili ndipo unapomwomba mtu achukue hatua. Labda hapa waweza kueleza inamaanisha nini maana ya kumpokea Yesu. Unaweza kuwaongoza kusali sala ya Toba inayomwalika Yesu aingie katika mioyo yao na waweze kuzaliwa tena.

Ifanyie kazi- Utaimarika

Unataka kuwa mjumbe wa Mungu? Ikiwa ndiyo unapaswa kushughulika katika uandaaji wako. Fanya mazoezi, jifunze, na ulitafakari neno la Mungu. Muhubiri ni msemaji wa Mungu. Kadri Roho wake anavyosema kweli ndani yako unapaswa kujifunza kuyasema haya kwa watu kwa Lugha inayoleweka. Msihi Mungu aifanye sauti yako iwe sauti ya Nabii kwa kizazi chako. Yeye anashauku ya kuwabariki manabii wake

TUMEZALIWA ILI TUZAE

Mwanzilishi wa *The Navigators*, kwa jina Dawson Trotman, wakati moja aliandika kijitabu alichokiita *Born To Reproduce*. Nilisoma kijitabu hicho mnamo mwaka wa 1960. Mwandishi huyo anazingatia kwamba tumkeokolewa ili tufanye wengine kuwa wafiasi wa Kristo. Alafu tufuate agizo kuu la Kristo la “kwenda kufanya watu kuwa wanafunzi.” (Mathayo 28:19,20). Itakuwa makosa makubwa tukifikiri kwamba Kristo alitoa agizo hilo bila mpango. Je ingwezekanaje kwa wafiasi wachache kufanya mataifa kote ulimwenguni kuwa wanafunzi?

Kuna wale wanaothani kwamba agizo kuu ni mpango wenyewe. Lakini agizo hili lina mbinu ambayo Kristo amekusudia kutumia kuushinda ulimwengu. Hebu angalia agizo hili kwa makini:

- **Enendeni** = mwito wa kushuhudia na kueneza injili
- **Mkawafanye kuwa wanafunzi** = mwito wa kuwandaa waamini
- **Mimi nipo pamoja nanyi siku zote** = ahadi ya nguvu zake
- **Kuwafundisha** = mwito wa kujizalisha kwa wote tuliyowaandaa

Kusema kweli, muda wote ambao Kristo alikuwa pamoja na wanafunzi wake aliutumia kwa kuwatayarisha kwenda kueleza ulimwengu habari njema katika jina lake. Alikuwa akiwasajili katika shule ya ufuasi. Kitabu kimoja chenye maana kilichoandikwa na Robert Coleman, *The Master Plan Of Evangelism*, kinatuonyesha wazi wazi kwamba Kristo alikuwa na mpango na makusudi kwa yote aliyofanya na wafiasi wake kumi na wawili. Kitabu hicho cha Coleman, kwa ufupi kinaonyesha mbinu ambayo Yesu alitumia, ambayo ni:

- Uteuzi
- Kuchangamana
- Kufanywa wakfu
- Kuongezeka

Uteuzi

Mbinu ya kwanza ambayo Yesu alitumia lilikuwa kuchagua watu waliofaa. Je, umegundua kwamba Yesu alikuwa na ubaguzi katika kuchagua wanafunzi wake “kumi na wawili?” Hakuita watu wote, ama mtu ye yote tu. Alichagua watu wachache. Hawakuwa watu wa maana katika ulimwengu, lakini aliwachagua

wamfuate. Walikuwa watu “wanono” (*fat – faithful, available, and teachable*). Kristo alikuwa na mpango katika kuchagua wanafunzi hao kumi na wawili. Hawakuwa watu timilifu, au walio na uwezo maalumu. Yesu aligundua uwezo uliokuwa ndani yao, alafu akajenga makusudi yake ndani yao.

Ingawa hivyo, tunastahili “kwenda” na kushuhudia wote watakaosikiliza. Tubatize atakayeamin. Kisha tumfanye kuwa mfuasi. Tunaweza kujifunza kutoka kwa Kristo. Hata hakuweza kufanya Yudasini kuwa mfuasi mwaminifu. Ili mpango huu ufanikiwe itakulazimu kuchagua watu watakaokufuata na kujifunza kutoka kwako. Mchungaji anaweza kuongoza kanisa, lakini hawezi kufanya wote kuwa wafuasi. Anaweza kufuata mfano wa Yesu kwa kuchagua watu wawili au watatu, akiwa katika maombi.

Kujumuika

Taratibu yake ya pili ilikuwa chimbuko la “kuwa naye.” Mtu moja kwa jina Coleman aliandika zaidi kuhusu mbinu hiyo. Alisema kwamba Kristo alikuwa na nia ya kuwa na wanafunzi wake karibu naye kwa miaka mitatu. Hata kama wangalisahau walikokwenda, ama waliokutana nao, wangalimkumbuka daima! Kujumuika na Kristo kungebadilisha watu hao milele. Agizo la “nifuate” lilikuwa mpango makusudi ya

Kristo kuwa kielelezo kwa wafuasi hao kumi na wawili. Walielewa na kushika kadiri walivyofundishwa. Kuwa na Yesu kila siku kuliwavutia. Hatimaye walimfia Kristo. Kristo alielewa chimbuko la “kuwa naye” kama la kufaa katika uongozi.

Nasi pia tunahitaji kuiga hila hiyo ya “kuwa nami.” Mtu hawezi kuiga mtindo wako wa maisha isipokuwa tu kwa kuwa nawe sana. Jinsi inavyofaa katika kulea watoto, ndivyo inavyofaa katika kulea wafuasi wa kiroho. Wazazi wanavyopata muda wa kutosha wa kukaa na mtoto wao, ndivyo wanavyomwezesha mtoto kutowasahau milele katika maisha yake. Ufuasi “unashikwa” “unavyofundishwa.” Ilisemekana kwamba wafuasi wa kwanza “walitambulika kwamba walikuwa na Yesu.” Anayehitaji kuwa kiongozi ni lazima awe na muda wa kuwa na wanafunzi wake vile Kristo alivyokuwa na muda na wanafunzi wake. Ili kuzaa kiroho, ni lazima atambue kwamba itamgharimu muda na kazi nyangi iliyona uchungu.

Kufanywa wakfu

Azimio la Yesu lilihusu mwito wake kwa wale aliochagua “kutafuta kwanza ufalme”. Mambo ya muhimu yana maana sana kwa mfuasi. Katika Luka 14 Yesu anatoa mifano yanayohusu kugharamika. Mara tatu, Yesu alisema, “*huwezi kuwa mwanafunzi wangu*” isipokuwa unipende kuliko watu, mahali, au vitu. Mpango wake unahitaji watu watakatifu, wenye nidhamu katika kutembea naye. Kwa miaka mitatu walisafiri naye na akawaonyesha kujitolea kwake kwa ufalme wa Mungu. Aliwahimiza kuiga mfano wake. wake.

Tunawajibika kuishi maisha yaliyowekwa wakfu ikiwa tutaongoza wengine. Ni vigumu kuongoza mtu kwa mambo ya roho ikiwa hujawahi kupitia unapomwelekeza kupita. Huwezi kuongoza wengine kuogelea, kama hujui kuogelea. Unaweza tu kumwongoza mtu mwingine kuwa karibu na Mungu ikiwa wewe pia u karibu na Mungu. Kwa jinsi gani? Mtu atagundua ukweli wako atakapoendelea kuwa nawe. Unapomwambia aombe, naye hakuoni wala kukusikia ukiomba, basi hawezi kuona umuhimu katika maombi. je, unadhani kuwa wale wanafunzi kumi na wawili waliweza kusahau nyakati za maombi pamoja na Yesu? Hasha! Walikuwa na shauku, na kutamani kumjua Mungu jinsi walivyomwona Yesu akiomba kwa Baba yake. Kufanya wengine kuwa wanafunzi ni kuwa mwanafunzi kwanza. Kisha uwaambie wengine kuwa wanafunzi.

Mbinu katika kuongezeka

Kuona kwa Kristo ufalme wa Mungu ndani ya wavuvi, watoza ushuru, waziloti na watu wengine wa kawaida kunastajabisha sana. Aliona ulimwengu ukibadilishwa kutokana na shuhuda zao. Watu wengine hawangeona uwezekano huo. Ingawa hakuna hata moja wa watu hao aliywahidi kusafiri zaidi ya maili mia moja kutoka kwao, Yesu aliwaagiza kuambia “mataifa yote” juu yake! Alikuwa na ratiba ambayo ilihu mtu kuleta mtu mwingine kwake. Hii ni mbinu inayohusiana na kuongezeka kiroho.

Je, hii inawezekanaje? Ni rahisi sana. Watu wachache wameijaribu kwa kweli. Ni hivi: mtu anaweza kumwongoza mtu mwengine kwa Yesu; kisha akamfundisha kwa mwaka moja jinsi ya kuleta mwengine kwa Yesu. Wakati huo pia anaweza kuongoza mtu mwengine kwa Yesu. Yule aliyefundishwa naye anamwongoza mtu wake wa kwanza kwa Kristo. Katika kipindi cha mwaka moja watakuwa watu wanne peke yao.

Taratibu hii yaonekana kutofaa katika kuuleta ulimwengu kwa Yesu. Si wachungaji wengi wanaoweza kujenga kanisa jinsi hiyo. Unaweza kudhani ulimwengu huwezi kufikiwa jinsi hiyo.

Hebu fikiri tena. Katika mwaka wa pili, kutakuwa na wafuasi wanane, kwa sababu kila moja atakuwa amemlata mfuasi mwengine na kumfundisha kwa mwaka moja. Katika miaka kumi ijayo kutakuwa na wafuasi 1,024 wanaotumia mbinu iyo hiyo. Itimiapo miaka ishirini, kutakuwa na wafuasi 1,048,576 wa Yesu. Hii si mbaya sana. Ama vipi? Kila moja wao akileta moja na kumfundisha, basi kwa miaka thelathini tu kutakuwa na wafuasi 1,073,741,824! Katika kizazi kimoja, kwa miaka arobaini, kutakuwa na

wafuasi bilioni moja ambao watakuwa wameokoka. Hebu fikiri tena hii ratiba ya Bwana kwa sekunde moja. Ukfikiria idadi hii, kanisa limekuwa na muda wa kutosha tangu Kristo atuachie ratiba hii ya kuleta ulimwengu kwake mara mia moja zaidi! Katika kizazi cha kwanza tu, kanisa lingetimiza agizo kuu la Yesu kupitia kwa wanafunzi wake kumi na wawili peke yao. Ratiba hii si mbaya. Watu waaminifu ndio hawajaijaribu bado.

Tunaelewa kwamba kuna matatizo yanayoambatana na ratiba hii ya kuongezeka kiroho. Ni vigumu kwa wote unaowafundisha kuwa waaminifu katika kuleta wengine kwa Kristo kila mwaka, hata ingawa wanastahili kufanya hivyo. Je, ni vigumu? Hasha! Mtume Paulo aliongeza maisha yake kwa Timotheo, Luka, Tito, na Trofimo. Yeye, kama mwinjilisti, alivuta watu wengi kwa Yesu. Lakini alileta halaiki ya watu kwa Yesu kupitia kwa wale aliofundisha. Aliwaambia waumini wa Thesalonike “*Nanyi mkawa wafuasi wetu na wa Bwana... hata mkawa kielelezo kwa watu wote waaminio... maana kutoka kwenu, neno la Mungu limevuma, si katika Makedonia na Akaya tu, ila na kila mahali imani yenu mliyo nayo kwa Mungu imeenea*” (Thesalonike 1:6-8).

Hebu tufafanue kwamba ni vyema tuelewe ratiba ya Yesu ya kukaribisha ufalme. Hatukuitwa ili tuongoze watu kuwa Wakristo, kuwabatiza na kuwaorodhesha kuwa washiriki wa kanisa, halafu tuwasahau. Tunahitaji kuwfanya wanafunzi. Mtu moja kwa jina Dawson Trotman alieleza vyema aliposema, “Shughuli haiwezi kuchukua nafasi ya kuongezeka, na kuongezeka haiwezi kuchukua nafasi ya shughuli.” Kristo ametoa mwito ‘tuwafanye wafuasi na kuwafundisha.’ Tumezaliwa ili tujizalishé kwa wengine. Tufuate mfano wa Yesu aliujizalisha kwa wale aliowachagua.

Je, Unafanya Nini?

Je, umejitolea kufuata ratiba ya Yesu? Kama sivyo, basi, unatumia uwezo wako vibaya. Wakati utafika ambapo utachunguza maisha yako kama umetenda kitu cha maana katika ulimwengu huu. Yesu alisema tuombe “*kwamba tuzae matunda ya kudumu*” (Yohana 15). Yeye mwenyewe aliombea “matunda” ya wafuasi wake alipoombea watakaoamini kupitia kwa ushuhuda wao (Tazama Yohana 17:20). Yesu, kwa hakika, alikuwa akiomba kwamba wanafunzi wake wawe watu wa kufanya wengine kuwa wafuasi!

Nilipokuwa kijana mdogo, kiongozi mmoja aliyekomaa kiroho alinitia changamoto. Nilimwona kwenye kongamano na kumsalimu nikisema “waendelea vipi?” Naye akanijibu hivi, “sitakuuliza unavyoendelea, lakini wengine wanaendelea vipi kwa sababu ya yale umekuwa ukiyafanya?” Nilipigwa na butwaa. Maneno yake yalipenya katika moyo wangu. Maneno yake yamekaa nami kaatika miaka ambayo nimemtumikia Yesu. Tunastahili kuishi maisha kama hayo tukiwa wafuasi wa Kristo. “Wengine wanaendelea vipi kwa sababu ya vile umekuwa ukifanya?” Hilo ni swali la Bwana wetu kwa yejote aliye mfuasi wa kweli. Je, unazaa matunda yatakayodumu? Je, unaweza kuelekeza kidole chako kwa Timotheo

na kusema, "Hii ni juhudi yangu ya kusaidia kutekeleza agizo kuu katika uhai wangu? Hawa wanaume na wanawake ni kazi ya maisha yangu."

Niko Pamoja Nanyi Daima

Hatimaye nenda katika jina lake kama umejazwa na Roho Mtakatifu na upako wa nguvu zake. Yesu anafurahishwa tunapajaribu kutimiza ratiba yake. Atatutangulia, na kuongea kuitia kwetu. Una ahadi ya baraka hiyo. *"Basi enendeni, mkafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru minyi, na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahar*

Mchungaji kama mfanya Wanafunzi

Wito wa Mchungaji

Kuwa mchungaji unapswa uwe ni “wito wa Mungu” na si kazi au utalaamu. Kuwa mchungaji kiukweli ni karama. Paulo mtume anaeleza huduma tano walizo nazo viongozi wa kanisa katika **Waefeso 4:11-12** “*naye alitoa wengine kuwa mitume na wengine kuwa manabii na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na walimu. Kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu hata kazi ya huduma itendeke hata mwili wa Kristo ujengwe ...*” Tunaona viongozi hawa wanatolewa na kristo kwa kanisa. Wamekirimiwa na wameitwa kwa ajili ya kuutumikia mwili wa Kristo (kanisa.) Kila kiongozi aliyekirimiwa na kuitwa anakazi maalumu ya kufanya.

Mchungaji/Mwalimu

Kipekee kazi ya mchungaji imeelzwa kama “*Mchungaji/mwalimu*.” Ni karama iliyounganishwa. Kiukweli mchungaji ni mchungaji wa kondoo za Mungu, kanisa. Anapaswa kufanya kile mchungaji wa kondoo anafanya kwa kondoo. Anaziongoza, anazilinda, anazilisha na kuzijali kama mchungaji mwenye upendo. Pia anakazi ya pili ya uzifundisha mamabo ya thamani ya ufalme na kweli ya ufalme. Katika jukumu lake la kufundisha anazilisha kondoo mkate wa uzima – neno la Mungu. Hii mara nyingi inafanyika kupitia kazi ya mchugaji kama muhubiri wa Neno la Mungu. Hata hivyo kuna mambo mengi unapoitwa mchungaji zaidi ya kile tunachoziyeza kondoo kufanya katika mahubiri. Anapaswa kuwakomaza watakatifu wawe watu wazima ambao wataimarika na kuwafundisha wengine kufanya huduma. Uzoefu unaonesha kwamba hewezi kulifuasa kundi kwa njia ya mahubiri. Yanasaidia, nanisehemu ya mafundisho lakini hayawezi kuwakomaza watu na kuwa wafiasi wa Kristo waliokomaa. Paulo anachokisema katika hii **Waefeso 4:11-13** inataka mchungaji awe ni mfanya wanafunzi. Mchungaji anataswa kuwa mwezeshaji, ili aweze kujizalisha mwenyewe kwa wengine.

Mwalimu/Mkufunzi

Makanisa ya Africa yamejaa mahubiri na si mafundisho na hakuna kabisa ukufunzi. Hata hivyo kufanya wanafunzi ni kitu kingine ambacho Kristo amewaita viongozi wa kanisa wafanye. Yesu akawa mfano kwa ajili yetu. Alikuwa na wanafunzi kumi nambili na alitumia miaka mitatu akiwaandaa kuupindua ulimwengu, jambo jema zuri ambalo lilifanywa na Yesu kama mfano. Mfano huu ulihusisha pia kuhubiri na kuwafundisha. Yesu akawajenga waweze kuibeba huduma yake atakapokuwa ameondoka.

Kama tulivyoona katika kitabu cha Kiongozi Mfuasi (Ukurasa 155-157) Yesu alikuwa na mkakati wa kuwafundisha wale kumi na mbili. Tunaweza kujifunza kutoka katika mkakati wake na kuzifanyioa kazi leo katika kuyaongoza makanisa yetu. Katika kitabu chake kizuri, Mpango kazi wa Uinjilisti, Robert Coleman anaonesha mpango ambao Yesu aliifuata akiwa na wanafunzi wake. Kuna mambo manne klatika Kitabu hicho:

1. Uteuzi

Njia ya kwanza ya Yesu kristo ilikuwa ni kuchagua watu sahihi. Naona umeshaona jinsi yesu alivyokuwa makini kwa watu aliowachagua ili wawe wanafunzi wake “kumi na mbili?” hakuwaita kila mtu au mtu yejote. Aliwaita wale aliowachagua wachache. Hawakuangalia kwa mtazamo wa kidunia bali aliita watu wa kawaida kabisa, lakini walikuwa ni watu ambao angeliweza kuambatana nao wakamfuata. Walikuwa ni watu ambao ni “ waaminifu, wanaopatikana na kufundishika”. Kulikuwa na moango jinsi Yesua anavyochagua watu wale kumi na mbili. Hawakuwa ni watu kamili au watu mashuhuri kama dunia inavyotaka lakini yesu aliona umuhimu wao na akajenga kusudi lake ndani yao.

Vivyo hivyo kila mchungaji anapaswa kuomba na kuangalia watu atakaowachagua na kuwa wanafunzi wake. Mtume Paulo aliona vilre Yesu alivyokuwa akifanya na akanukuu. Paulo alijua njia pekee ya kutimiza utume mkuu lililo katika **Mathayo 28:19** ni kufanya kama vile Yesu alivyofanya – Kufundisha watu wengi. Paulo alikuwa anayejizalisha. Paulo anamwambia Timtheo kijana wake katika huduma, “*Na mamabo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine.*” (**2 Timotheo 2:2**) Hapa tunamwona mchungaji Paulo aliyepanda makanisa mengi sana alikuwa akifanya kazi njia alizotumia Yesu katika kuchagua watu atakaowekeza kwao.

Mchungaji- Timotheo wako yuko wapi?

Hata hivyo tunapaswa “kwenda” na kuwashuhudia wale wote watakao tusikiliza. Pia tunapaswa kuwabatiza hao waumini wapya. Jambo linalofuata ni kuwfanya wanafunzi baadhi yao. Hapa ndipo tunaweza kujifunza kutoka kwa Kristo. Hata yesu mwenyewe hakuweza kuwa na wanafunzi wazuri mfano Yuda. Paulo hakuweza kumfanya mwanafunzi Yohana Marko. Kuwa mtu unayechagua ni jamboi zuri sana kwenye mpango huu. Tafuta mtu atakayeambatana na wewe pia atajifunza kutoka kwako. Mchungaji anaweza kuongoza kundi lakini hawezikulifanya kundi lote wawe wanafunzi. Anachoweza kufanya ni kile yesu alifanya. Kwa maombianaweza kuchagua watu wawili au watatu walio na moyo wa Mungu wanaotaka kujifunza kutoka. Kila mchungaji anapaswa kusema huyu ni Timotheo wangu!

2. Jumuiya

Njia nyingine ya kristo ilikuwa ni “**Kuwa naye**”. Dr. Coleman katika kitabu chake amesema mengi sana katika mkakati huu. Anasema ulikuwa ni mpango wa Yesu kuwa na hawa kumi na mbili karibu naye kwa muda wa miaka yote hii mitatu. Hata kama wangesahau walienda wapi, au walikutana wapi lakini walau wamkumbuke! Hii ni “Kuungana” na kristo kitu ambacho kingebadili watu hawa. Agizo la “Mnifuate” ulikuwa ni mpango na kusudi la kuwafundisha hawa kumi na mbili. Waliweza “Kushika” mambo mengi kadri walivyokuwa wakifundishwa. Kitendo cha kuwa na yesu karibu kila siku kwa mahusiano ya karibu sana ilibadili mioyo yao. Walikuwa tayari hata kufa kwa aili ya Yesu. Kristo alielewa uongozi wa kanuni ya “*Jumuiya yaani kuwa nao*” .

Sisi nasi hatuna budi kulipokea hili la kanuni ya “Kuwa name”. Huwezi kujizalisha maisha yako kwa wengine bila kuwa na muda wa kutosha na mtu huyo. Hii ni kweli katika kulea watoto na ni kweli katika maswala ya kiroho. You. Wazazi wanaotumia

muda wa kutosha na watoto wao mara zote watoto wao watawaweka katika miyo yao milele. Ufuasi ni “kushika” vya kutsha kadri unavyoweza Uunapofundisha”. Ilikuwa inasemekana kwamba, “*Waliwatambua kwamba wamekuwa na Yesu.*” Mtu anayetaka kuwaongoza wengine unapaswa kupatikana wakati wote kama Yesu alivyokuwa kwa walio wake. Kujizalisha kiroho ni mchakato wa kuzaa na ni jambo linalohitaji muda na wakati mwengine ni kazi ya maumivu.

3. Kuwekwa Wakfu

Mpango wa Yesu pia ulikuwa ni kuwafanya wale watu aliowaita “*kuutafuta kwanza Ufalme*” kiwe kipaumbele chao kama wanafunzi. Katika Luka 14, Mifano ya Yesu ilikuwa ni kuhesabu Gharama. Mata tatu katika Luka 14, Bwana wetu anasema, “*hamwezi kuwa wanafunzi wangu,*” hadi pale mtakaponipenda kuliko watu, mali na vitu. Mppango wake unawale ta watu wafike katika sehemu ya utakatifu waweze kuenenda naye. Zaidi na zaidi ile miaka mitatu walisafiri pamoja akawapa Fursa ya kuona jinsi ya kujitoa katika kazi ya Mungu na akawahimiiza wawe kama Yeye alivyokuwa. Na sisi Pia tunapaswa kuishi matakatifu ili tuwaongoze wengine. Ni kanuni ya uongozi wa kiroho kwamba huwezi kuwaongoza wengine na kuwapeleka sehemu ambayo hujawahi kwenda au kufika. Huwezi kuwasaidia watu watoke kwenye kuzama ikiwa wewe hata kuogelea hujui.. Huwezi kumwelekeza mtu mwengine akae karibu na Mungu hali mwenyewe mwenyewe uko mbali na Mungu. Kwa nini? Kwasababu yuko muda mwangi na wewe atakukamata tu.” Ikiwa unamwambia aombe lakini anakuona au hasikii ukiomba hawezi kuomba na kuyaweka maombi kipaumbele chake. Unadhani wale kumi na mbili walishau masaa yao ya maombi na Yesu? Kamwe! Yesu alipokuwa akimwomba Baba hivyo na hawa kumi na mbili walitaka kumjua Mungu zaidi kama Yesu alivyokuwa karibu naye! Kuwafanya wengine wawe wanafunzi unapaswa wewe uwe mwanafunzi kwanza.

4. Kanuni ya Kujizidisha

Ni jambo la kushangaza kwamba yesu aliwaangalia watu hawas wa kawaida. Wavuzi, watoza ushuru, mazelote, na watu wa kawaida kabisa na kuona ufalme wa Mungu ndani yao. Aliona kitu ambacho hakuna ambaye alikuwa amekiona akaona ulimwengu ukiokoka kwa ajili ya ushuhuda wao. Hakuna hata mmoja wao ambaye alikuwa kasafiri maili nyingi kutoka nyumbani kwake. Lakini bado Yesu aliwaagiza waende kwenye mataifa yote wakahubiri! Lazima alikuwa na Mpango. Alikuwa nao. Maono yake ilikuwa ni kwakila mtu kumfikia mtu mmoja amfundishe kumfikia mtu mwengine mmoja. Mpango huu ni kujizalisha kiroho. Ni kanuni ya kujizidisha.

Ni kwa jinsi gani hili linawezekana na je linafanikiwa? Ni rahisi sana kwamba wachache wameshajaribu. Na ikafanikiwa kama hivi. Ikiwa mwanafunzi atamleta mtu mmoja na akatumia mwaka mzima anamfundisha mtu huyo kumleta mtu mwengine kwa Yesu muda si mrefu Yule mtu atamleta mtu mwengine. Mwishoni mwa mwaka huyu mwanafunzi atakuwa na mtu wake. Huyu naye aliye kuja anaanza kumfundisha huyu aliye mleta ili alete mtu mmoja kwa Kristo. Mwishoni mwa mwaka watakuwa ni wane. Ukiangalia ni kama mpango huu hauendi katika mchakato wa kuufikia ulimwengu. Ni wachungaji wachache ambaoi wanamfumo wa kujenga kanisa kwa utaratibu huu. Unaweza kusema kwamba hawa hawataufikia ulimwengu.

Tafakari tena. Sasa **mwaka wa pili** watakuwa ni watu wanane, kwa sababu kila mtu ataleta mtu mmoja. Kwa muda wa **miaka kumi** watakuwa ni **1,024** wakifanya mkakati ule ule. **Miaka ishiri** dunia itakuwa na wafuasi **1,048,576** wa yesu Kristo. Hii si mbaya si ndivyo? Sasa kila mtu atafundisha na kuleta mtu mmoja kwa muda wa **miaka Thelathini** watakuwa ni watu **1,073,741,824!** Katika kizazi kimoja, **miaka arobaini**, zaidi ya **Trioni moja** watakuja kwa Kristo katika wokovu! Tafakari juu ya Mpango kazi kwa sekunde kadhaa. Ujue hii idadi ya watu trioni moja ni hesabu inayoogopesha. Kumbuka tumekuwa na muda wa kutosha tangu yesu alipotupa agizo kwa hiyo dunia tungkuwa tumeifikia zaidi ya mara 100! Kanisa lingekuwa limeshatimiza utume mkuu katika kizazi cha kwanza kupitia kwa wale kumi na mbili tu. Siyo mpango mbaya isipokuwa watu hawajafanya kwa uaminifu.

Mafunzo/ Ujuzi

Ikiwa mchungaji anataka kutimiza wito wake anapaswa kujifunza kufundisha na kuwafunza wengine. Paulo anamwambia Timotheo (Mwanafunzi wake) “*Kila andiko lenye pumzi ya Mungu lafaa kwa mafundisho nakwakuwaonya watu makosa yao na kwakuwaongoza na kwakuwaadibisha katika haki.*” **2nd Timothy 3:16** Angalia faida hii “*kuwaongoza katika haki*”

Mchungaji ni mkufunzi! Anapaswa kujifunza namna ya kuendeleza “Ujuzi” katika kanuni zake. Hii hasa inamaana gani?

Kwa mfano: Ikiwa mchungaji ni mwanamaombi hilo ni jambo jema; lakini hadi awafundishe wengine kuomba vinginevyo atawenza kukamilisha mambo madogo sana katika swala la nguvu ya maombi. Anawafundishaje watu wake kuomba?

ANAWAONESHA JINSI YA KUOMBA! Hadi waombe pamoja naye, wajifunze jinsi ya kuomba, wamsikie akiomba vinginevyo hawawezi kuwa na hamu ya kuomba. Yesu alitumia muda mwangi katika maombi na watu wake. Baada ya kumwangalia akiomba na kusikia akiongea kwa baba yake wanafunzi wake wakalia wakimwambia “*Bwana, tufundishe kuomba kama hivyo!*” (**Luka 11:1**)

Kuna ujuzi mwangi ambaeo mchungaji anaweza kuwapa wanafunzi wake. Kile anachojua kufanya anaweza kumfundisha mwagine kufanya. Anaweza kuwafundisha kushuhudia, kuomba, kuongoza wengine, kutumika kwa unyenyekevu, kuwa wakili mwema, kumtumaini Mungu na hata kuwa mfanya wanafunzi.

Kanisa la Afrika

Kila mchungaji wa Africa anayo maamuzi ya kufanya. Anaweza kuendelea kuliongoza kanisa lake kiutamadunia wa kiafrika au anaweza kuamua kuwa mchungaji wa Kibiblia akiwaongoza watu wake kama Waefeso 4. Kama ataamua kuwa mwanafunzi basi wa Biblia mamabo yafuatayo yatatokea kwake kama katokeo.

1. Matimotheo wake (wakiume na wakike) watakuwa ni kituo chake. Atajizidisha kwa wengine.
2. Hawa wanafunzi wapya ni wazee muhimu, wainjilisti na hata wachungaji wa kupanda makanisa. Kupitia hii hali ya kupanda makanisa anakuja kuwa ni kiongozi wa kitume na askofu kwa mtazamo wa Biblia. Anakuwa ni mlezi wa wengi.

3. Atakuwa ni mfano wa makanisa mengine ya kiafrika kwamba kuna njia nyingine kubwa zaidi ya kuwa zaidi ya dhehebu. Watu wa kiume na kike wanapoanza kujiongeza au kujizalisha Neno litaeneo na Mungu hakika atakuwa kazini.
4. Kufanya wanafunzi utakuwa ni urithi halisi wa mchungaji. Nyuma yake ataacha watu waliobadilika, viongozi waliokomaa, na waibeba kazi aliyoianzisha. Ikiwa hatafanya wanafunzi kazi itakufa atakapokufa. Ni rahisi hivyo.

Ni kizazi gani unachoishi kwa ajili yake?

Kiongozi anayefanya wanafunzi haishi kwa ajili ya izazi cha leo. Yeye anaishi kwa ajili ya baadae ni kiongozi anayewaza ya kesho. Anataka kuacha utamaduni uliobadilika nyuma yake atakapoondoka. Kwakufundisha kizazi cha wanafunzi wa Yesu akiondoka anaacha jeshi amabalo litabadili mila na desturi kwa miaka mingi ijayo. Kile anachofanya sasa na Timotheo wake itakuwa kama wimbi pembezoni mwa bahari linalochimba kingo za bahari.

Kwa hiyo mxhungaji wewe ni aina gani ya mchungaji unataka uwe? Ninakusihi umfuate Kristo, Paulo na Petro, Tito, timotheo na viongozi wengi wa Agano jipya waliobadili ulimwengiu wao kwa kufanya wanafunzi wa ulimwengu mzima.

Ufalme Wa Mungu Na Upandaji Makanisa

Pius Kutto na Barry Wood

Maana; Tunamaanisha nini tunaposema “KANISA?

Ekklesia –Katika Kiyunani, maana ya neno hili ni ... ”*wale walioitwa..*” Katika Utamaduni wa kiyunani ilimaanisha ni kusanyiko la wananchi Angalia **Matendo 19:32,39 na 41** mahali ambapo *Ekklesia* ni kusanyiko la wananchi.

Katika Uyunani wa Agano la kale(Septuagint) Ni kusanyiko la Waisraeli jangwani **Matendo 7:38.** Katika Agano Jipyu ni jamii ya Wakristo, watakatifu walio duniani au mbinguni au sehemu zote mbili.

Yesu na ndugu zake=KANISA. Katika **Mathayo 16**, Yesu alitumia neno *ekkelesia* akaita ni “KANISA LANGU”-KUSANYIKO

WAEBRANIA 2:12(inanukuu **Zaburi22:22**)”...*akisema Nitahuburi jina lako kwa ndugu zangu katikati ya KANISA nitakuimbia sifa...*”

Mwandishi wa WAEBRANIA anashikanisha maneno hayo na Bwana Yesu ambaye anawaita washirika wa KANISA lake “NDUGU ZANGU” na anasema “*ataimba sifa katikati ya kusanyiko*” ambalo ni KANISA.

Kwa hiyo - ni kusanyiko la walio itwa., wale alio wajua tangu asili ili wafananishwe na mfano wa MWANA WAKE, walio itwa, wakahesabiwa haki na kutukuzwa. **Warumi 8:29-30**

Yohana 6:68 Kanisa la kweli ni wale wasiojikwaa na maneno ya Yesu.

Yohana 5:24; *Amin amin , nawambia, Yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yeye aliye nipeleka yuna uzima wa milele;bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani.*

Hawa ni wanaume na wanawake chini ya Ufalme na utawala wa Mfalme Yesu. Wapo katika ufalme wa Mungu na Neno lake ndilo katiba ya kuwaongoza.

JE UFALME WA MUNGU UNA UHUSIANO GANI NA KANISA?

MAANA; Tunaweza kuueleza ufalme wa Mungu kama ‘*watu wa Mungu, mahali pa Mungu, chini ya utawala wa Mungu*’.

Mahali popote unapoona watu wa Mungu, wakiishi chini ya utawala wa Mungu,wakitumika mahali pa Mungu(makusudi na mapenzi) unaweza kupata Ufalme. Hata hivyo,haya hufanyika tu pale wanapokuwa mahala pa Mungu(wakifanya mapenzi na makusudi yake) na chini ya utawala

wake. Wakati mfalme anatawala kwa njia ya wanawe, ufalme wa Mungu unakuwa umefika duniani. Hii ndio ilikuwa maana ya Yesu aliposema;’ *Ufalme wa Mungu uko ndani yenu.’***Luka 17:21**

Kielelezo: Ikiwa waumini 20 wamekusanyika pamoja lakini wote wako kimwili, Mwili wa Kristo uliokimwiri na kiroho, Mfalme hata udhihirisha uwepo au Utukufu wake.

Lakini ikiwa hawa 20 wafuasi wa Kristo ni Mwili wa Kristo uliojazwa na Roho Mtakatifu, wao watakuwa ni kituo cha Mfalme na utawala wake. Wanaweza kuonesha ufalme wa Mungu duniani kupitia wao. Wamepewa fungu za ufalme wa mbinguni (**Mathayo 16:19**)Ni watu wa Mungu ,mahali pa Mungu, Chini ya utawala wa Mungu.

Katika mfano huu ufalme na kanisa watakuwa sawa kama wanavyototakiwa kuwa.

Kuutambua Ufalme

Kanisa la mahali halitakiwi ni kama Taasisi iliyotengenezwa na wanadamu . Ama shirika la kufanya biashara za Mungu.Kanisa linatakiwa ni kuwa mahali duniani ambapo utapata MFALME akifanya kazi yake ya kutawala na kuongoza kupitia watu wake. Mfalme Yesu Wakati akitawala ,mapepo huondoka, wagonjwa hupona,waliopotea huokoka maana ufalme umekuja katika utukufu. Hili lina sipaswa kuwa ni lengo la kila mchungaji na watu wote - kuona UFALME ukija wakati wanakutana kwa ajili ya ibaada, maombi , sifa na mahubiri.

Mambo ya Kuchukua

1. Tuna fahamu ya kuwa injili tunayo ihubiri ni ya Ufalme . Tuna tangaza ya kuwa Mfalme ame kuja na ameleta Ufalme wake. Mfalme Yesu anatawala mionganii Yeye na pia kupitia Kanisa lake. Atarudi tena ili kujenga ufalme wake hapa duniani.
2. Kupanda kanisa si kukusanya watu wachache pamoja ili mchungaji awe na kazi na baadae akusanye sadaka ili aweze kujinufaisha mwenyewe. Kupanda kanisa ni kujaribu kusimika UFALME wa Mungu ndani ya kijiji au jamii Fulani ya watu. Ina hitajika kuwa safari ya kiroho, ilio zaliwa katika maombi, inayosukumwa na mahubiri yenyе nguvu na kufanya ufatiliaji wa wale wanaokoka na kuwafundisha kwa mafundisho ya Biblia.
3. Tufahamu kuwa KANISA NA UFALME WA MUNGU havifanani.Wote waliopo katika UFALME ni mali ya KANISA, lakini si washiriki wote wa kanisa la mahali ni mali ya ufalme UFALME wa MUNGU. Ndio maana kondoo wa Mungu wana sitahili kilishwa, kulindwa na kuongozwa. Kondoo ni wanyama dhaifu sana wanasitahili mchungaji la sivyo watapotea. Kupanda makanisa hakuwezi kufaulu bila ya mchungaji kuwepo wa kulinda kundi jipya. Kumuandaa mtu kuwa mchungaji ni muhimu kwa manufaa ya kundi au jamii mpya. Mchungaji anatoa mafundisho na muongozo kwa wana kondoo ili waishi maisha ya KIFALME na kuwafikia wengine kwa injili.

“Nitalijenga kanisa langu ...” KANISA LINA JENGWA NA YESU.

Mathayo 16:18 Hapa tunapata tamko la kwanza la neno KANISA(EKKLESIA).

1. Ni Kristo tu anaweza kupanda kanisa lake. Kanisa halijajengwa kwa Simoni Petro! Petro kwa msaada wa Roho Mtakatifu aliruhusiwa kumowna Yesu Kristo kama Kristo,
2. Yesu alimwahidi amjenge yeye kama kanisa kwamba milango ya kuzimu haitalishinda. Akapewa funguo za ufalme kufunga na kufungua.

Utendaji: Vivyo hivyo kila mtu ambaye amepewa ufunuo wa Kristo kama Mwana wa Mungu na kuamini ufunuo huo amezaliwa mara ya pili na amepewa mamlaka ya kujengwa kama kanisa na funguo zile zile ambazo Petro alipatiwa. Wanajukumu la kufunga na kufungua*Walipo wawili au watatu wamekusanyika kwa jina Langu name nitakuwa katikati yao. Na chochote utakachokifunga au kukifungua duniani na mbinguni vivyo hivyo ...***Mathayo 18:18**

3. Kristo ni kichwa cha kanisa ambalo ndiyo mwili wake -**Waefeso 5:23, Col 1:18**

4. Kanisa pia ni nyumba ya Mungu -**Waebraenia 3:6**

KANISA SI NINI

-Si jengo lenye mnara mrefu juu na vioo vyeusi .

-Si taasisi au dhehebu lililo tengenezwa na mwanadamu. Ila ni mwili uliyo hai; Mwili wa Kristo duniani.

Si kila mshiriki wa kanisa la mahali katika dhehabu fulani. Ila ni watakatifu halisi wanao nyenyekea kwa utawala wa Kristo.

KUPANDA KANISA

Katika Agano Jipyta tuna ushahidi tosha kwamba KANISA lilitutana katika nyumba mbalimbali. **1wakoritho 16:19; 'Akila na Prisila wanawasalimu sana katika Bwana, pamoja na kanisa lililoko ndani ya NYUMBA yao'**

Wakati kanisa kule Yerusalemili likuwa na mazoea ya kukutana sana hekaluni, Paulo alikodisha shule ya Tirano kule Efeso. Kanisa katika Agano Jipyta likuwa na uzoefu sana wa kukutana majumbani. Hili haliwezi kuzuiliwa. Nyumbani ni mahali na mazingira mazuri na bora ya kupanda kanisa. Hau hitajai kutumia fedha kulipia nyumba, au kununua vyombo vya mziki au kuwa na kwaya.

Matendo 16:13-15 tuna soma kuhusu Lidia; alifungua moyo wake;,,, **ayatunze maneno yalio nenwa na Paulo..kama mmeniona kuwa mwaminifu, kwa Bwana, ingieni nyumbani mwangu mkakae,,**

Ina onekana kanisa la nyumbani lilikomalia katika nyumba hii na hapa ndipo wandugu walikuwa wakikutania. ***40..Nao wakatoka gerezani wakaingia nyumbani mwa Lidia, na walipo kwisha kuonana na ndugu wakawafariji wakaenda zao...***

MIFANO YA KIBIBILIA YA UPANDAJI WA KANISA MANYUMBANI

MATENDO 2;42 Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na kataka kuumega mkate na katika kusali...46..Na siku zote kwa moyo mmoja walodumu ndani ya hekalu, wakimega mkate nyumba kwa nyumba na kushiriki chakula chao kwa furahana kwa moyo mueupe... Matendo 20:20-21 Paulo alihubiri hadharani na kufundisha nyumba kwa nyumba

HATUA SABA ZINAZOFAA KATIKA KUPANDA KANISA

Kuna hatua saba katika kupanda kanisa ambazo zikitiliwa maanani na kutiwa katika matendo tunaweza kuwa na matokeo mazuri sana yasiyo na mwisho katika jamii zetu.

1. MAOMBI

- Kutaneni na kuomba na kukubaliana ili mapenzi ya Mungu yafanyike –Mathayo 18:19-20
- Ombeeni nafsi ziokolewa-**2 Petro3:9**
- Waombee waliopotea kwa majina yao,;- **Yohana 6:44,65 na Zaburi 2:8, Matayo 7:7**

2. UINJILISTI

Wafikie jamii kwa njia ya kuonesha sinema na kwa kutumia miche miraba

-Tengeneza waumini wapya na anza kuwa fuatilia haswa wale walio omba sala ya toba. Pata majina na tarifa zao za mahali wanako toka.

Fanya urafiki wa karibu nao. Watembelee na kuwa himiza juu ya imani yao mpya.

Waalike mahali ushirika wa nyumbani unapo kutania hhata kama ni hapo kijijini kwao.

3. Kulea

Anza kulea waumini wachanga kwa kuwapa maziwa safi ya NENO la Mungu **1Yohana 2:12-14** Wafahamishe ya kwamba dhambi zao zimasamehawa kwa sababu ya JINA LAKE, na wasaidie kuufikia ufahamu wa Baba. Wafundishe ukitumia HUTUA ZA MAISHA MAPYA KATIKA KRISTO kitabu cha kwanza na kile cha pili ili wakomae. Wasajie kujua kanuni za Baba Mungu zilizoorozeshwa katika **Waebrania 6:1-2** kwenye kitabu cha maisha mapya ndani ya Kristo.

4. Kufanya Wanafunzi

Hakikisha kila mmoja wao amefundishwa Neno la Mungu na si kwenye hudma kubwa au kiongozi au mtu mkubwa.

- Wafundishe misingi na kanuni za Neno la Mungu ili waweze kukomaa.
- Wafundishe kulijua neno la Mungu Yaani Rhema - **Warumi 10:17**

4. Kufundisha na Kuimalisha

Wafundishe jinsi ya kijisomea Bibilia, Wape kazi ya ziada ya kusoma vifungu, kuomba na kushiriki na wengine imani yao mpya.

Enenda nao wakuone ukifanya, waruhusu wafanye huku ukiwaangalia, washukuru wakifanya vyema, wasahihishe kwa njia ya upendo wa Yesu wanapokosea.

5. KUPANDA KANISA

Wanapo endelea kukomaa kiuwezo na idadi ikiongezeka waweke katika makundi madogo madogo ili kuwaruhusu kuwajibika. Waletee vijiji vipya ambavyo havijafikiwa.

6. Kuchipuka kwa huduma Mpya

Unapo pokea watenda kazi wapya wanao wajibika , huduma mpya zinaanza kuchipua. Karama zao za Kiroho zitaanza kuonekana.Uongozi hufuata karama. Hivi ndivyo mtu anaweza kujizalisha ndani ya mwengine. Kwa njia hii wengi wanafikiwa na kuwa na uhusiano wa moja kwa moja na Yule kiongozi wa wanfunzi. Wanapo ongezekwa zaidi wanaweza kijiunga na dhehebu lilio sajiliwa rasmi katika nchi au wanaweza kujisajili wenyewe pia kulingana na sheria ya nchi yao. Ukweli ni kwamba bado Yule kiongozi wa wanfunzi atakuwa na usemi kwao haswa kutoa muongozo wa kiungu. Viwanja na amajengo yanatapatikana kulingana na Bwana avyobariki.

7. Watoto/Matimotheo

Hawa ni watu unawenza kuwahesabu katika huduma. Wameletwa na Mungu na wewe umewathibitisha. Unatembea nao katika uhusiano wa Baba na motto kama vile Paulo alivyotembea na Timotheo, Tito n.k. hawa ni watu watakaoendeleza huduma hii.

Hawa si watu amba ni kwa ajili ya msahara. Hawa ni wana/ watumwa wa Kristo waliuo na Urithi. Wanawenza kuchukua kazi kutoka kwako na kuiboresha sana kama vile ilivyokuwa kwa Eliya na Elisha.

Hata kama haupo bado unawenza kuwa na uhakika kupitia watu hawa. Hiki ndicho tunachokiita ni urithi – Ni limbuka la mwisho linaloweza kuendeleza kazi hata kama utakuwa umetwaliwa na Bwana. Neema na Amani iwe nanyi.

Mambo makuu kuhusu Viongozi Wema

1. Wanafahamu kwamba uongozi ni ushawishi

Uongozi ni vitu vingi, lakini asili yake ni ushawishi na hali ya kuweza kushawishi wengine. Kiini cha neno “ushawishi” haswa ni “kutiririka ndani” ya wengine. Kiongozi ni yule ambaye kwa kumaanisha “hutiririka ndani” ya wengine. Umaarufu wake kama kiongozi unategemea ushawishi wake. Kipimo cha uongozi wako unategemea idadi ya watu wanaoshawishika na uongozi wako kila siku, kila juma, kila mwaka, na maishani **mwote**.

2. Wanafahamu kuwa uongozi ni kitu cha kuendelea

Imesemekana kwamba viongozi hawaundwi bali huzaliwa. Hi ni ukweli nusu. Kuna wale wanaozaliwa na uwezo katika ungozi, lakini viongozi shupavu katika uliwengu wanafahamu kwamba uongozi huchukua muda kukua na inahitaji nithamu. Uongozi hukuzwa kila siku. Haikui kwa siku moja. Kwa hivyo uwe na bidii katika kuimarisha uongozi wako. Kuimarisha ujuzi wako katika uongozi kutakupa nafasi mwafaka wa ushawishi. Musa alianza kwa kumwambia Mungu, “Lakini Bwana, mimi ni kigugumizi, nitakwendaje kwa Farao na kuongea?” Baada ya kufundishwa na Mungu, na kuwa na imani, akaliongoza taifa! Alikuzwa ndani ya kazi. Unaweza kuzidisha ushawishi wako ikiwa utaweka akili yako na moyo wako kufanya hivyo.

3. Wanafahamu kwamba ni wewe tu unayeweza kuweka kiwango katika ushawishi wako

John Maxwell anaita, “Kanuni ya kifuniko.” Je, unataka kuwa na ushupavu wa namna gani kama kiongozi? Uamuzi wako **utatoa** mwelekeo na ushawishi wako na hatma yako kama kiongozi. Unaweza kuzidisha uongozi wako na ni wewe tu unayeweza kuamua kuhusu ushawishi wako. Inamaanisha kwamba uwezo wako unakutegemea. “Haya funga behewa kwa nyota, fungua macho na lahaul, umepata!” Watu wengi wenye uwezo mkubwa wanafanya mambo madogo madogo kwa sababu hawatambui uwezo walio nao. Usipunguze uwezo wako au yale ambayo Mungu anakusudia kuititia kwa maisha yako kwa kuwa mvivu au kwa kukosa kuitikia mwito zaidi.

4. Wanafahamu kwamba mafuta yanayompa nguvu ni bidii ya moyo wake.

Viongozi wana bidii katika mwelekeo wao. Wana moto ndani yao inayowasukuma kufanikiwa. Kiongozi “humalizwa” na maono yake au shauku yake, na ni sharti ashirikishe wengine. Uongozi hufundishwa na pia huigwa. Uwezo mwingu wa kiongozi uko katika hisia zake, kama vile tu **uko** katika akili na uwezo wake. Ni heri shujaa wa vita kuliko askari ambaye amefundishwa juu ya vita lakini hana moyo wa kupigana. Shauku hutangulia mipango kila wakati. Shauku na mipango huhitajika ili kuwe na ufanisi, lakini ni vigumu kumzuia kiongozi mwenye shauku.

5. Wanafahamu kwamba viongozi ni Waelekevu na Wenye maono

Nikiwa rubani wa ndege yangu, nilimuuliza mke wangu kama angelipenda kuendesha ndege. Alinijibu kwa kusema “ndiyo.” Baada ya kushika duara ya kupindia ndege kwa dakika chache, aliniambia hivi: “Naweza kuendesha ndege lakini sijui ninakoelekea.” Hii inatuambia kwamba mtu ye yote anawenza kuendesha ndege, lakini ni rubani tu anayeweza kuipa mwelekeo. Viongozi ni kama rubani wa ndege. Wana maono na mwelekeo. Kusema kiongozi ana mwelekeo na pia ni rubani ni kusema kwamba ni mtu “anayefikiria makuu.” Kwa kawaida wao huwaachia watu wengine kushugulikia mambo madogo

madogo. Hiyo ndio sababu wasimamizi si viongozi. Wasimamizi hushughulikia tu mambo madogo madogo ya kila siku. Kiongozi anaona maono makuu kuliko “mkate wetu wa kila siku.” Anafikiri jinsi ya kutengeneza mikate ya kutosha kulisha ulimwengu!

6. Wanafahamu kwamba viongozi wamejifunza mambo ya kutanguliza

Yesu alituambia tutafute kwanza ufalme wa Mungu na haki yake (Mathayo 6:33). Hivi ndivyo ilivyo na viongozi shupavu. Wanafahamu [vyema](#) kuweka mambo ya maana mbele. Viongozi wana uwezo maalum wa kuzingatia mambo ya staha. Hawatou jasho kwa mambo madogo madogo. Kuweka kipa umbele mambo ya staha, mda wako na uwezo wako ni kuwa na kipawa kizuri katika uongozi.

7. Wanafahamu kwamba viongozi ni Watumishi, na si mabwana

Katika kitabu kimoja kionachouza sana kiitwacho *Good to Great* tunajifunza kuwa mashirika yanayofahamika sana yana kiongozi ambaye ni mtumishi kwa watu wake. Hii ndiyo kanuni ya Yesu katika uongozi. Katika kitabu cha Yohana 13, tunaona kisa cha Yesu akiwa mtumishi kwa wanafunzi wake. Anawauliza hivi, “mnajua kwa nini nimefanya hivi?”. Kiongozi mwema ni yule ambaye hawezi kuuliza wafuasi wake kufanya chochote ambacho yeye mwenyewe hawezi kufanya. Wanajeshi wengi husimulia hadithi za jemedari waliowaongoza kwenda vitani. Akiwa amejiweka hatarini, yeye huongoza vitani. Kama vile Mel Gibson katika “*Brave Heart*” ambapo anamwonyesha William Wallace, bila woga, akiongoza watu wake katika pigano. Viongozi si mabwana, ila ni watumishi. Viongozi si nyapara au wasimamizi, bali ni wasaidizi katika unyenyekevu. Uongozi wao ni kutoka chini kwenda juu, wala si kutoka juu kwenda chini.

8. Wanafahamu kwamba watu watamfuata mtu kabla kujitolea kufuata maono yake

Mara nyingi viongozi chipukizi huwa na shauku sana kuhusu maono yao na hujaribu sana kushawishi watu wengine kukubali maono hayo na kuyafuata. [John](#) Maxwell anauita Kanuni ya “kununua.” Lakini watu wanapokosa kufuata au “kununua” maono yake, anashangaa ni kwa nini. Hi ni kwa sababu watu hifuata kiongozi kabla kukubali au kufuata maono yake.

Hebu fikiri jinsi Yesu alivyoongoza wafuasi wake. Alikaa nao kwa miaka mingi ili wamfahamu, wampende, na kisha wajitolee kumfuata. Hapo ndipo aliwapa maono yake. Viongozi shupavu wanafahamu kwamba watu humfuata MTU mwenye maono kabla kufuata maono yake. Kwa kuwa mnyenyekevu, mwenye maadili mema na mwelekeo, kiongozi ni kama sumaku anapovuta watu kwake. Kisha anawashurutisha kufuata maono yake.

9. Wanafahamu kwamba kiongozi ni lazima avutie moyo wako kabla kuitisha msaada wako

Viongozi shupavu wanafahamu kwamba siri ya kupata [wafuasi](#) ni kuaminika. Watu hawavutiwi sana na wazo la mtu, ila wanavutiwa na roho yake. Watu watakufuata wanapokuamini. Yesu alijua hivyo, na kabla kuwaliza wanafunzi wake wamfanyie kitu kama “kujitwika msalaba na kumfuata,” alihakikisha kwamba roho zao zilikuwa karibu naye. Kila wakati viongozi wakristo chipukizi huuliza watu misaada ya fedha na miradi bila kwanza kuwavutia, kwa uaminifu wake, wale wanaotafuta misaada kutoka kwao. Kwa mfano, mchungaji mwafrika anaweza kusikia kwamba huyu “mzungu” anawapenda waafrika na kwamba anasaidia makanisa na wachungaji kwa fedha. Kwa hivyo, bila hata kumfahamu huyu “mzungu,” anaanza kumtumia barua pepe kuhusu “maono yake” ya

kujenga makao ya watoto yatima. “Mzungu,” akisha pata taarifa ya mradi unaohitaji fedha kwa ajili ya watoto yatima, anafikiri hivi, “Ni nani huyu mwafrika ambaye simfahamu na ananiomba fedha? Simfahamu na hali anahitaji nimpe fedha za kutegemeza kazi yake.” Hebu nikuambie kwamba Yesu hangelifanya hivyo. Kiongozi mwema ni lazima aaminike kwamba kabla kuomba watu wengine kushikilia maono yake.

10. Wanafahamu kwamba watu humfuata mtu wanayemheshimu

Hii inaitwa “Kanuni ya Mzee” katika Afrika. Kwa lugha ya [Kiswahili](#), “Mzee” ni mtu aliye na umri mkubwa na mwenye hekima. Yeye ni mkomavu na anaheshimika na wengi kwa hekima yake na yale ambayo amepitia katika maisha. Tamaduni za Kiafrika zina heshima kwa wazee. Tamaduni za kizungu huona wazee kama watu wasio na maana. Ingawa hiyo, kanuni katika uongozi ni kwamba watu hawatamfuata mtu wasiyemheshimu. Watu wanaweza kumwogopa kwa heshima na kuambatana naye, lakini kushika maono yake itakuwa [vigumu](#) ikiwa hawamwamini na kumheshimu. Kwa hivyo kiongozi mwema anaelewa kwamba itamgharimu muda na bidii kabla watu kumheshimu. Ujumbe wa maisha yake ni msingi katika uongozi wake. Kuongoza ni kwa tabia.

11. Wanafahamu kwamba uongozi bora hutokana na uzalishaji

Kiongozi shupavu anaweza kumwangalia mtu na kuona jeshi kubwa nyuma yake. Anajua kwamba akimtia moyo mtu huyo, na kumfunza kuongoza wengine, basi anaweza kujizalisha kwake kama mfuasi wake. Kiongozi anaweza kuona kwamba hesabu ya kuzidisha ni bora kuliko ya kuongeza. Itambidi kujizalisha kwa wengine ikiwa anahitaji kusambaza maono yake. Dawson Trotman, kiongozi shupavu wa wanaume wakristo, alikuwa na uzoefu wa kusema, “Utendaji [hauwezi](#) kuchukua nasafi ya kuzaa, na kuzaa kuchukua nafasi ya kuzalishana.” Mtume Paulo, ambaye pia ni kiongozi shupavu, alimwambia mfuasi wake chipukizi Timotheo kujizalisha kwa watu wengine waaminifu (2

Timotheo 2:2).

Usijiulize umekuwa ukifanya nini, bali jiulize, “watu wengine wanafanya nini kwa sababu ya yale nimekuwa nikifanya?” Viongozi wanazaliwa ili wazalishane. Yesu aliangalia wanafunzi wake kumi na wawili na kuona ulimwengu wote ndani yao! Aliwafunza na kuwapa Agano Kuu “kwenda na kufanya mataifa yote kuwa wafuasi...” Alielewa haja ya kiongozi kujizalisha.

12. Wanaacha sifa njema

Shauku ya kuzalisha maono yako kwa maisha ya wafuasi wako hutokana na haja ya kuacha sifa njema ukisha toweka. Kiongozi shupavu si yule anayeishi kwa “sasa,” bali anaishi kwa ajili ya kizazi kijacho. Katika Yohana 17, tunamwona Yesu akiwaombea wanafunzi wake, akisema, “*Siombi kwa ajili ya hawa tu, Baba, lakini nawaombea pia watakaoamini kwa ajili yao.*” Hebu ona kwamba alikuwa akiishi kwa kwa sifa njema kwa ajili ya vizazi vijavyo ambao wangeokolewa kutokana na uaminifu wa wafuasi wake. Viongozi shupavu wote huamini kwamba mwelekeo wao na maono yao yanafaa kupokezwa kwa vizazi vijavyo. Kwa hivyo viongozi hutoa muda wao bora kwa watu wao bora. Wanatazamia mabadiliko kwa siku za usoni. Wanaona maisha mema kutokana na wafuasi wao, walio na wafuasi wao, na wafuasi wao. Inawezekana kuwa unatengeneza sifa njema sasa au umeipuzilia mbali.

KIONGOZI MTUMISHI

Wakati moja niliona kibonzo cha mtoto mvulana, aliye kuwa kiongozi wa skauti ambaye alipeleka kikundi chake cha wavulana kukwea mlima, ambapo alipotea na kuuliza kama ye yote kati yao alikuwa na dira (*compass*). Jambo la kwanza kwa kiongozi aliye bora ni kwamba lazima awe na uwezo wa kuongoza. Mtume Paulo alitaja vipawa mbali mbali vya Roho Mtakatifu, ikiwapo kipawa cha “uongozi”. **Warumi**

12:8 inatuambia, “*mwenye kusimamia kwa bidii.*”

Tunaweza kujifunza mengi kuhusu uongozi kwa kumtazama Yesu anavyoongoza wanafunzi wake. Ukweli ni kwamba kipawa cha uongozi ni Yesu kiongozi anayeishi maisha yake ya uongozi ndani ya maisha ya mtoto wa Mungu aliye na kipawa.

Imesemekana kwamba viongozi huzaliwa; hawatengenezwi. Hii ni kweli kabisa kwa kiongozi Mkristo. Baada ya kuzaliwa mara ya pili, Roho humpa kipawa cha uongozi. Alizaliwa upya ili aongoze.

Kuongoza kwa Tabia

Anayetamani kuongoza wengine kwa utumishi kama Mkristo lazima ajifunze kutoka kwa Kristo. Kristo hakuongoza kwa matakwa yake mwenyewe, ama kwa imla au vitisho, bali kwa maadili. Yesu alifundisha

wanafunzi wake kumi na wawili jinsi ya kuongoza kwa kufuata wema wa Mungu na maadili ya Bibilia. Yesu alitumia tabia yake kama mwongozo katika kufundisha jinsi ya kuishi kwa maadili ya milele.

Yesu Alivyoongoza Watu

Ustadi wa Yesu kama kiongozi wa watu ni kwamba alikuwa kiongozi mtumishi. Aliongoza kwa

kutumikia wengine. Upole wake, upendo wake, na moyo wa kutumika uli wavutia wote aliowaongoza. Yesu hakupima ukuu wa mtu kwa watumishi aliokuwa nao, bali kwa wingi wa watu aliotumikia. Kwa kweli, Yesu alitimiza unabii wa Isaya kwamba Masihi atakuwa “*mpole na mnyenyeketu wa moyo*” (**Isaya 53**). Masihi atakuwa mfalme, lakini mfalme mtumishi! Paulo anatuambia kwamba Kristo alikuja “*kwa namna ya mtumwa*,” (**Wafilipi 2:6,7**). Hii ndiyo impendezayo Kristo. Ni nia yake na maisha yake. Anaongoza watu kwa kuwa kiongozi ambaye ni mtumishi.

Kutawadha

Miguu

Yohana 13:4 kuendelea imenukuu ujumbe wa maisha ambayo Yesu aliwapa wanafunzi wake alipokuwa

karibu kuondoka duniani. Aliwatawadha miguu. Aliwafundisha kwa mfano wake mwenyewe. Hawangeweza kamwe kusahau mfano huu ulioonyeshwa na Mfalme wa Utukufu aliyepiga magoti na kutawadha miguu ya wapendwa wake kwa unyenyekevu. Hebu tujifunze kanuni za milele kutokana na Yesu kutawadha miguu michafu:

1. Unyenyekevu Ni Kiini cha Uongozi Wa

Utumishi

Kumwona Yesu akitawadha miguu yao iliyonuka ilikuwa funzo tosha katika unyenyekevu. Yesu ambaye

alikuwa amejivika kitambaa cha kupangusa miguu kama mtumwa wa kawaida aliosha miguu yao ili wajue kwamba njia ya kuelekea juu iko chini! Njia ya uongozi wa kweli unapatikana katika unyenyekevu. Kongozi lazima awe tayari kufanya kazi duni ili kutia wengine moyo wa kutumika. Si vyema kiongozi kuuliza watu wengine kufanya kazi asichokuwa tayari kufanya mwenyewe. Roho wa Kristo ndani yako atakupa unyenyekevu wake kwa kutimiza maneno haya “*Basi nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa wakati wake*” (**1 Petero 5:6**).

2. Mtumishi Kiongozi haambiwi

kutumika

Mfano tunaoona wa Yesu akiwa tu na kitambaa cha kupangusa miguu ni wa moyo wa kujitolea. Hakuna

aliyemuuliza kufanya kazi hii duni, bali alichagua kuifanya mwenyewe. Anaona hitaji na kulitimiza. Wanafunzi wake hawakuwahi kudhani kwamba siku moja wangalimwomba Yesu kuosha miguu yao Ndio sababu viongozi shupavu ni wale walijitolea bila kushurutishwa. Wanavutia watu wengine kwa mfano wao. Kujitolea kwa Kristo, hata msalabani, kunatuvutia sana kuwa kama yeye.

3. Kiongozi Mtumishi

habagui

Jambo la ajabu ni kwamba Yesu aliosha miguu ya Yudas, akifahamu vyema kwamba alikuwa msaliti!

Hili ni tendo la upendo na rehema kwa wingi. Viongozi shupavu ni wale wanaotumikia wote wanaohitaji utumishi wao, bila kubagua. Upendo wa utumishi hauna kifani. Tunaweza kujifunza kutokana na mfano wa Kristo.

4. Viongozi Watumishi huva mavazi ya Kaki

Kwa kuva kitambaa cha kupangusa miguu, Yesu alikuwa tayari kufanya kazi chafu iliyohitaji kufanyika.

Hili ni tendo la pendo. Tendo hili linatukumbusha kuna kujifunza zaidi katika *kutenda*, kuliko *kusema*.

Uongozi unahusiana sana na *tunavyotenda*, kuliko *tunavyowaambia* wengine kufanya. Yesu alikuwa “mionganii” mwa wanafunzi wake, akichangia sehemu muhimu katika maisha yao ya kila siku. Aliwaongoza kwa kuwatumikia kila siku. Kiongozi yu tayari kufanya lolote ili kufanya wengine bora zaidi.

Sam Walton, ambaye ni mwanzilishi wa Maduka ya Wal-Mart alifahamika sana kule Bentonville Arkansas iliyomakao makuu ya Wal-Mart. Alifahamika kwa sababu hata baada ya kuwa immoja kati ya matajiri wakuu ulimwenguni, aliendelea kuendesha gari lake la *pick up* iliyokuwa imedumu miaka kumi. Alisema kwamba kuendesha gari hilo lilimkumbusha kuwa mnyenyeketu na kumkumbusha alikotoka. Viongozi huva nguo za kaki.

5. Viongozi Watumishi hupeana bila kutarajia kurudishiwa

Yesu hakuuliza wanafunzi kama wangependa kuosha miguu yake. Kuna funzo hapa. Mtumishi hadai

atumikiwe kwa kuwa ametumika. Hii haihusiani na kupata kutoka kwa watu wengine kwa kuwa umewapa. Viongozi shupavu wanauia mema kwa wengine bila kujinufaisha wenyewe. Wanaona

“picha kubwa,” bila kuona tu ulimwengu wao mdogo.

6. Viongozi Watumishi ni sharti wajifunze kupokea na kupeana

Petero alimwendea Yesu na kusema, “*Bwana hutanitawadha miguu!*” Ombi hili halionekani tu kuwa

ombi lenye heshima, bali pia laonekana kuwa lenye kiburi, ndipo likasababu Yesu kumrekebisha Petero. Kristo angependa tuelewe kwamba ni vyema viongozi wakubali utumishi kutoka kwa wengine.

Tunahitaji unyenyekevu wa kuruhusu wengine watuhudumie jinsi tunavyowahudumia.

7. Viongozi Watumishi wana Utu sawa na

Kristo

Baada ya kutawadha wanafunzi wake kumi na wawili miguu, Yesu aliwambia hivi, “*Basi ikiwa mimi,*

niliye Bwana na Mwalimu (ujumbe wa maisha), nimewatawadha miguu, imewapasa vivyo kutawadhana miguu ninyi kwa ninyi” (**Yohana 13:14,15**). Ujumbe huu ni wazi kwa wote watakaoufuata. Tutakuwa watu wa maana ikiwa tutafanya wengine jinsi Kristo alivyofanya. Yeye ni kielelezo katika uongozi wa maisha ya Ukristo; aliongoza watu kwa kuwa kielelezo. Hakuwaambia tu wapende adui zao, bali yeze mwenyewe aliwapenda adui zake kwa hakika. Alimfanya mtoza ushuru wa Kirumi kuwa mfuasi! Alikula chakula cha jioni na Zakayo aliyekuwa amedharauliwa. Alimsamehe mwanamke aliyepatikana akizini. Kielelezo chake kilikuwa fundisho tosha.

Viongozi Watumishi huongoza wengine

Kiongozi inamaana “yule anayesimama mbele mbele ya wengine” katika lugha ya Kiyunani.
Kiongozi

wa kiimla huwaambia wengine kufanya yale ambayo yeze mwenyewe hataki kufanya. Kiongozi wa kweli

si wa namna hiyo. Yeye huchukua mstari wa mbele. Anasema “nifuate mimi na mfano wangu. Fanyanifanyavyo. Nitakuonyesha namna ya kufanya.” Hivyo ndivyo Kristo aongozavyo watu. Anakuambia uchukue msalaba wako kila siku. Kisha anaenda kufa msalabani kwa ajili yako! Si ajabu watu walimpenda. Wangali wanamfuata. Lazima tuwe vielelezo kwa kuwa katika mistari ya mbele, kama viongozi watumishi.

Viongozi Ni Watu Wenye Maono

Yesu aliona ufalme wa Mungu; akanuia kuuliza wafuasi wake kuungana naye katika maono ya kuuleta

ufalme huo hapa duniani. Aliona uwezo iliyokuwemo ndani ya wale watu kumi na wawili aliyowachagua. Alikuwa akifikiri kuhusu wokovu wetu alipowaita (**Tazama Yohana 17:18-20**). Kwa kuwaongoza, allinuia kuleta ulimwengu wote kwake. Robert Coleman, katika kitabu chake kitiwacho *The Master's Plan of Evangelism*, anaona ono hili kama sehemu ya uongozi wa Kristo. Kila kiongozi mwema lazima awe na hatima katika mpangilio wake. Viongozi huona mambo ambayo wengine hawaoni. Hii inaweka wazi tofauti baina ya viongozi na wasimamizi. Msimamizi anaangalia

mambo ya kawaida ya kila siku. Hao si viongozi wa watu. Hao ni wasimamizi wa wafanyakazi! Pana tofauti kubwa kati yao.

Mwitu

Mbaya

Kuna mfano maarufu unaoeleza tofauti kati ya viongozi na wasimamizi. Mfano huu ni wa kundi linaloondoka kwenda safarini. Kisha linajikuta katika mwitu wenyewe mimea mirefu kuliko ndovu. Msimamizi anawakusanya ili watengeneze njia. Anapeana panga na maji kwa wafanya kazi walio choka, na kuwaangalia vyema wanapajaribu kutengeneza njia. Msimamizi huyu anaweka fikira zake zote kwa kuelekeza watu. Kisha kiongozi anajitokeza. Anakwea mti mrefu na kuchunguza eneo hilo, alafu anamwambia msimamizi, “acha kukata! Unaenda njia mbaya.” Huyo ndiye kiongozi, kwa maana anaona picha kubwa na kuongoza kwa jia inayofaa.

Viongozi Watumishi ni watu wa kujitolea

Yesu alijitolea katika kufuata ono lake. Alimpa Baba Mungu yote aliyokuwa nayo katika siku zake zote.

Ni tabia njema kiongozi kuzingatia mwito wake na maono yake, bila kuupoteza kwa urahisi. Anapanga kazi yake na kutekeleza mipango yake.

Ni mtu aliyepagawa na anayokusudia kufanya, kwa sababu kuna wengi ambao wangependa kumzuia na kumvunja moyo. Kiongozi ana imani kwa kile afanyalo wakati ambapo wengine hawajali. Kiongozi ni lazima aulize wafuasi wake wajitolee alivyojitlea mwenyewe. Yesu aliwaambia watu wake hivi, “ikiwa mnanipenda, tiini amri zangu”.

Tunazungumza kuhusu kuwajibika. Viongozi watu wao kuwajibika katika maono yao, mipango yao, au mwito wao. Anawajibika, na kwa hivyo anahitaji watu wake kuwajibika.

Viongozi Watumishi Wamejitolea kwa Ubora

Kiongozi ana lengo. Yesu, ambaye ndiye kielelezo chetu, alikuwa na lengo. Milele alikusudia mambo

mawili: 1) Kazi ya Baba yake (tazama **Luka 22**). 2) Kumpendeza Baba yake (tazama **Yohana 8:29**). Tunastahili kujitosa katika wazo hili la kumtumikia Mungu kwa ubora. Ubora unatokana na shauku ya moyo unaotamani kumpendeza Baba wetu wa Mbinguni. Ubora ni kuwa na juhudhi kwa mambo uliyoitiwa na Mungu kufanya. Tunawajibika kufundisha wanaume na wanawake kuzingatia ubora mapema maishani.

Kukuza viongozi watumishi mapema kutatuwezesha kuwa na kizazi cha viongozi watakaobadilisha ulimwengu.

Tunaona mtindo huu wa kukomaa kwa viongozi:

- Viongozi chipukizi – wana kati ya miaka 18-25
- Viongozi wenge bidii – wana kati ya umri wa miaka 25-40
- Viongozi thabiti – wana miaka 40 na zaidi.

Ujumbe kwa Maisha Yako

Hatimaye Yesu alionyesha hali kamili ya kiongozi. Maisha yake yalikuwa ujumbe kamili. Wengi walimkumbuka siku nyingi baada ya umati kusahau maneno na matendo yake. Wanafunzi wake walitaka kuwa kama yeye. Hiyo ni sifa njema. Tuwe “Kristo” kwa wengine jinsi wamwonavyo.

Huwezi kuongoza tofauti na uishivyo. Tembea jinsi unavyozungumza. Jinsi ulivyo huzungumza zaidi kuliko ufundishavyo. Kiongozi wa kweli husema, “nifuate, nimewahi kufika hapo.” Anaishi anavyowaambia wengine wafanye.

Utangulizi

Ushirika Wa Huduma Ya Ufalme

Mtandao Wa Makanisa

Maelezo

“Basi utafuteni kwanza ufalme wa Mungu, na haki yake, na hayo yote mtazidishiwa.” Mathayo 6:33

Ushirika wa Huduma Ya Ufalme (KINGDOM MINISTRIES FELLOWSHIP) ni ushirika wa makanisa na huduma ulio na mtazamo wa kutenda kazi pamoja katika kuendeleza na kupanua ufalme wa Mungu katika mikoa yetu ya Kiafrika na hata ulimweng mzima . Si dhehebu wala haitatokea kuwa dhehebu bali inashirikiana na madhehebu na Waumini wanaoamini **Yohana 3:3**, “...Hautaweza kuingia ufalme wa Mungu hadi uzaliwe mara ya pili.”

Ufalme wa Mungu

Ufalme wa Mungu ni kanuni ya mamlaka ya milele ya Mungu mwenyezi juu ya viumbe na vitu vyote (Tazama **Zaburi 103:19**). Tunauingia ufalme kwa njia ya kuzaliwa upya (**Yohana 3:5-7**), pia unajulikana kama “Ufalme wa Mbinguni.”

Ufalme wa Mungu unatawala uumbaji wote mbinguni na duniani. Ufalme wa Mungu ni , kwa hiyo, ulimwengu mzima katika kwamba unahusisha malaika walioumbwa na hata wanadamu. Ni wa milele, kama Mungu alivyo wa milele, na ni kiroho—unapatikana kwa waumini waliozaliwa mara ya pili. Ni mahusiano “*Kuzaliwa kwa Roho*” (**Yohana 3:5**), na tunaujasiri wa uhakika kwamba ni hivyo kwasababu Roho hushuhudia pamoja na roho zetu (**Warumi 8:16**).

Mungu nimwenye mamlaka, yuko mahali pote, anajua yote na ni matawala wa viumbe vyote.. Hata hivyo mwonekano “Ufalme wa Mungu” unajumuisha mfumo ule uliokatika Mungu na ni wa milele.

Ufalme wa Mungu ni nini hasa? Graeme Goldsworthy anaueleza kama “*Watu wa Mungu G , katika sehemu ya Mungu, chini ya utawala wa Mungu ,* ”Ni kanuni ya Mungu duniani na katika kanisa lake. Kanisa la Kristo ni la kiulimwengu. Linahusisha waumini wote walioitwa toka duniani na kuingia katika ufalme wake.

HUDUMA

Huduma ni karama zilizotolewa na roho Mtakatifu kwa ajili ya kazi za kanisa. Karama hizi hushirikiana kwa ajili ya kulijenga kanisa kwa sababu kanisa hujijenga lenyewe kulingana na **Waefeso 4:16.**

Sisi tulio wengi hufanya mwili mmoja

Warumi 12:5 inasema “...kila kiumbe kinategemea kiungo kingine.”

1 Korintho 12:12-13 inasema “*T kama vile mwili ni mmoja na una viungo vingi na viungo vyote vya mwili ule navyo ni vingi ni mwili mmoja vivyo hivyo na Kristo. Kwa maana katiika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja kwamba tu wayahuidi kwamba tu wayunani ikiwa tu watumwa au ikiwa tu huru nasi sote tulinyweshwa Roho mmoja.*”

Ushirika wa Huduma ya Ufalme inatazamia kutoa vyanzo muhimu kwa ajili ya watu na kanisa kutambulika, kuunganikana na kushirikiana na wengine walio na shauku moja kwa ajili ya uinjilisti,, ufuasi/ubaba, serikali ya kanisa la kibiblia, ndoa za kibiblia na huduma zingine.

USHIRIKA

Ushirika wa Agano jipya ni uhusiano kati ya walioamini ambao kwa nje hushirikiana na Kristo na wao kwa wao katika kutimiza mapenzi ya Mungu duniani. Ushirika katika maana ya agano jipya ni umaja wa ndani unaoonekana kwa nje kukamilisha mapenzi ya Mungu.

Ushirika wa Agano jipya una umuhimu katika njia mbili zifuatazo:

1. Ushirika wa Agano jipya ulitokea kiasili kama matokeo ya kulisimamisha kanisa.

Roho Mtakatifu aliwashukia watu hawa na kufanya moja wa ndani na uumbikaji wao wa asili ulikuwa ni kutumikiana kwa nje. Hii imelezwa katika **Matendo 2:44-47.**

Utendaji huu wa pamoja katika kutimiza mapenzi ya Mungu uliendelea katika kanisa kwa kufanya mambo mengi kama uzalishaji wa uongozi, kazi mbalimbali, kusaidia wahitaji, kutenda huduma mbalimbali za Roho, kusaidia wamisionari walioitwa kwa huduma mbalimbali, maombi ya ushirika na makundi ya kuabudu.

2. Ushirika ni njia muhimu ya kukamilisha makusudi ya Mungu kwa ajili ya kanisa. Paulo anaeleza makusudi ya Mungu kwa ajili ya kanisa katika **Waefeso 3:8-11.**

Katika sura hii Mungu ana mpango wa milele na kanisa linajukumu la kufanya Katika kukamilisha mpango huo . Kusudi la kanisa kama lilivyoelezwa katika msitari wa 10 ni kuuonyesha ulimwengu hekima mbalimbali za Mungu na kuonesha kila jambo la utukufu wake ili kila mtu aone.

Waefeso 4:16 inatuambia kwamba hakuna mtu awezae kutenda peke yake katika kutimiza mpango ili kuonesha kusudi la Mungu katika dunia, kwa sababu Mungu hutenda na kupitia wat wake katika jamii. Asili ya mpango wa Mungu unahimiza uwezo wa kimungu katika watu wake kuonesha kusudi lake ulimwenguni. Ili Mungu aweze kudhahirika katika ulimwengu huu kila

mtu katika kanisa hapaswi tu kutenda bali anapaswa aungane na wengine wanaotimiza majukumu yao pia. Njia ya muhimu tunayoitumia katika kufanya hili ni ushirika, ushirika wetu katika kutimiza Kusudi lake. Ni pale tunapotenda pamoja ndipo inawezekana kutimiza mpango wa Mungu. Na ndiyo maana ushirika wa kweli ni Muhimu sana katika kanisa.

1st Korintho 12 inaonesha wazi kwamba kila muumini katika kanisa niwamuhimu kwa kazi yake. Kwa sababu ya umuhimu wa Ushirika hakuna anayeruhusiwa kujiondoa katika utendaji wa Mwili wa Kristo, Kanisa.

Halafu tunaona kwamba tendo la ushirika yaani udhihirisho wa nje wa mapenzi ya Mungu ndani yetu situ ya asili bali ni muhimu katika kukamilisha kusudi la Mungu kwa kanisa. Kwa jinsi gani, Twaweza kutenda ushirika?

Kufanya Ushirika

Waweza kushirikiana kwa kutambua lengo la mtandao wa KMF network na kuchukua sehemu muhimu ambayo waweza kuwa ni Baraka kwa wengine katika kanisa. Watu wengi hawajihusishi katika kanisa kwa sababu hawaoni kusudi lililo wazi. Kusudi letu ni konesha utukufu wa Mungu ulimwenguni kwa njia zote nyingi alizotuelekeza katika Biblia. Tunashiriki pamoja katika utukufu wa Mungu, kwa kufanya kwa njia yake na kufanya kwa pamoja.

Waweza kufanya ushirika kwa kuchukua nafasi unayoiona kwa ubora waweza kusaidia lengo hili. Waweza kutambua ni wapi waweza kuweza kwa kutambua karama yako ya Roho na uwezo wako wa asili na kujua hitaji la kanisa. Waweza kuwa Baraka kwakusaidia mahali unapoona kwamba kanisa linaweza kuwa ni Baraka. Ikiwa hujui karama yako waweza kutenda kwa kufuata uwezo wako wa kawaida. Unapotenda na wengine karama yako itadhihirika na utaona sehemu ya kutenda katika kanisa kulingana na uwezo na karama yako.

Hebu tufanye kazi pamoja. Kila mta ashirikiane kama ilivyokawaida kama vile ilivyokuwa kwa kanisa la kwanza ili kwamba hekima za Mungu zijulikane kwa njia ya kanisa lake.

Makanisa

Ushirika wa Huduma ya Ufalme (KMF) inaamini kwamba (1) makanisa ya mahali katika Agano la kale ni yale yanayojitawala na kujiongoza (2) huduma hufanyika kwa nguvu na kwa usahihi katika kanisa la mahali si kwa njia ya udhehebu. KMF inafanya kazi na makanisa ili kuondoa hali ya udhehebu inayokamata makusanyiko ya mahali na kulenga katika kuujenga falme wa Mungu pamoja. Japo baadhi ya madhehebu yanang'ang'ania kwamba kila kusanyiko la mahali ni mkono wa huduma ya dhehebu, , KMF inaamini kwamba Kristo ndiye kichwa cha kanisa . KMF inashikilia kwamba "makao makuu" ni mkono wa kanisa la mahali y. KMF winafanya kazi na makanisa ya mahali kuimarisha huduma zao kwa ufasihii kwa njia ya ushirika kwa ajili ya kazi ya Ufalme wa Mungu.

TAMKO LA MAONO

Maono ya Ushirika wa Huduma ya Ufalme ni kutimiza Agizo la utume wa Bwana wetu (Mathayo 28:19-20) kwa kuwaandaa wachungaji na viongozi katika makanisa ya Waafrika. Tutakwenda, tutaleta, tutafuasa na kuwafundisha wengine kujizidisha kwa njia ya kufanya wanafunzi wengi.

TAMKO LA UJUMBE

Ujumbe wetu wa KMF ni kutimiza Agizo la Bwana wetu Yesu Kristo kwa njia zote za kiblia kwa njia ya kushirikiana na kungana na mashirika, makanisa, huduma na hata watu kwa maandiko sahihi yaliyothibitishwa kiimani yanayokubaliana na neno la Mungu.

Ushirika Wa Huduma Ya Ufalme

Tamko la Imani

- 1. TUNAAMINI** Biblia ini Neno la Mungu lililovuviwa, na ni mamlaka yetu ya pekee katika Imani na utendaji katika maisha ya kikristo. Lafaa kwa mafundisho, na kwakuonya, kuongoza na kuadisbisha katika haki. (**2nd Timotheo 3:16**)
- 2. TUNAAMINI** katika Roho mtakatifu kama alivyotamkwa katika tamko la mitume. Kuna Mungu mmoja aliye katika utatu na ameunganishwa katika nafsi ya Baba, Mwana na Roho mtakatifu wote ni kitu kimoja ni ni wa milele.
- 3. TUNAAMINI** katika Yesu Kristo kama Mwana wa pekee, mwokozi na Bwana wetu. Kifo cha mateso yake kwa ajili ya dhambi zetu ni njia pekee ya msamaha wetu na uzima wa milele.
- 4. TUNAAMINI** watu wote wamepotea na wanahitaji neema ya ukombozi ya Mungu. Kuna mpatanishi mmoja kati ya mwanadamu na Mungu, na huyo ni Kristo, Bwana. Wokovu ni kwa njia ya neema ya Mungu kwa njia ya Imani katika kazi ya kristo katika Kifo chakekuzikwa na kufufuka kwakwe.
- 5. TUNAAMINI** kwamba ubatizo wa maji mengi ni ushuhuda wa kanisa kwa kuzaliwa upya kwa muumini. Wokovu hauokoi bali ni tendo la hadhalani la kukiri na kuonesha utii kwa kristo na ushuhuda kwa wengine kwa njia ya kufufuka na kristo na ufufuko wa maisha ya muumini katika Kristo.

6. **TUNAAMINI** tuko chini Kristo katika kupeleka Injili hadi mwisho wa nchi hadi pale kila taifa litakapokuwa limesikia habari njema za Mungu za wokovu. **Mathayo 28:19-20 , Marko 16:15**
7. **TUNAAMINI** historia yote inaelekeza katika utukufu wa kurudi kwa Kristo kuweka ufalme wake. Tnaomba ufalme wako uje na tnategemea kurudi haraka kwa mfalme kwa kufanya sehemu yetu ya kutimiza utume mkuu katika maisha yetu.
8. **TUNAAMINI** Roho mtakatifu amevuvia kwenda, kuleta, kufuasa, na kufundisha watu wengi iwezekanavyo; kusaidia kutimiza agizo kuu katika kizazi hiki. Njia yetu ni Huduma ya watu teule ambapo tunafundisha viongozi muhimu abao hutoka na kwenda kufundisha wengine.
9. **TUNAAMINI** katika huduma tano za uongozi ndani ya kansa la mahali kulingana na **Waefeso 4:11-13**; Mungu atainua watu waliokirimiwa Mitume, manabii, Wainjilisti, wachungaji na walimu ili kulikamilisha kanisa.
10. **TUNAAMINI KATIKA BABA/UWEZO WA MAHUSIANO YA MWANA.**
Uwezo wa kuinua wana katika huduma watakounganshwa katika neema kwa uwezo wao kutoka katika viongozi wao, na sikutoka katika shirika au taasisi “theocratic rule” bali kwa uelewa wa karama za Roho na mahusiano ya Agano. Eliya na Elisha, Paulo na timotheo ni mifano mizuri ya Ulezi wa baba na Mwana . Uhirika wa umoja unaonekana katika upako kwa kugahamu mwili wa Kristo na kazi ya kila kiungo (**Waefeso 4:15-16**).
11. **TUNAAMINI KATIKA NDOA YA KIKRISTO YA MKE MMOJA NA MME MMOJA.**
Watu wawili huishi kama kitu kimoja katika Kristo na kwa ajili ya kristo wanaweza kufanya mengi kwa kumtumikia bwana katika ndoa yao na huduma
12. **TUNAAMINI KWAMBA Ushirika** ni mahusiano baina ya walioamini ambao hujionesha wao kwa nje wakishirikiana na Kristo na wao kwa wao katika kukamilisha mapenzi ya Mungu duniani. Si swala la kwa pamoja bali kutenda kazi pamoja katika kukamilisha mapenzi ya Mungu.
13. **TUNAAMINI KATIKA KUWEKEWA MIKONO NA VIONGOZI KWA NJIA YA HUDUMA ZILE TANO.** Viongozi wa kanisa na wito wao ni vema wakathibitishwa kipindi hiki cha kuwekewa mikono. Tazama **Mdo 6:6; Mdo 13:3. 41**

Shabaha Ya Ushirika wa Huduma Ya Ufalme

- Kulileta kanisa, wachungaji kwenye mtandao wa pamoja uliowekwa kwa ajili ya kusudi la kujenga ufalme wa Mungu pamoja katika bara la Afrika
- Kutekeleza Agizo kuu la kristo, kufundisha, kuhubiri na kufanya wanafunzi katika mataifa yote Mt 28:19-20 na 16:15.

- Kufanya makongamano ya wanaume na wanawake teule mpaka maono ya watu teule yapandwe katika miyo ya watu teule kwenye mikoa mbali mbali ya Africa.
- Kuhamasisha na kuandaa makundi na kufanya uinjilisti wa mlango kwa mlango kwa kutumia kasha la Injili katika makanisa yetu yote ya KMF na hivyo kuendeleza mwili wa uinjilisti wa Kristo
- Kupanda na kueneza makanisa na kuwaangalia waumini wapya, kuwakomaza katika ufuasi ili nao wajizalische.
- Kufanya makongamano na semina za mahali na za jumla kwa ajili ya kanisa kimtandao.
- Kutumia nafazi zinazopatikana kuwfafikia watu kwa Injili na kuwafundisha viongozi wetu kufanya vivyo hivyo.
- Kuyaongoza makanisa yetu kutokufanya mapenzi au ngono zembe kwa kuonesha mikanda mashuleni, katika wizara mbalimbali na hata katika jamii kwa kuweka vikundi vya upendo halisi mashuleni na makanisani.
- Kwa kufanya au khamasisha vipindi ya HIV/AIDS mashuleni, makanisani na katika jamii katika mikoa yote iliyoungana.
- Kufundisha na kuandaa Mwili wa Kristo (makanisa ya huduma ya KMF) kwa njia yoyote inayowezekana.
- Kuwaafundisha kila mkristo katika huduma yao waliyoitiwa na Mungu /Kusudi/Kipaji/karama kwa kutumia wachungaji na viongozi wengine walio katika mtandao.
- Kuhamsisha na kuendeleza vifaa vya mafundisho katika mitandao ya mikoani na kuendeleza uzalishaji wa manabii, wainjilisti, na mafundisho ya uchungaji na uinjilisti.
- Kutoa uangalizi na ulezi wa Kiroho, ushauri na katika huduma iliyokatika makanisa na hata shirika lililo katika Agano na mtandao wa KMF.
- Kutoa maelekezo kwa watenda kazi wa jamii maendeleo ya jamii kwa njia ya mtandao wa makanisa.
- Kusimamisha na kuendeleza uhusiano imara na huduma, huduma za mashule, vyuo na Wizara ulimwenguni kuendeleza na kuimarisha ukuaji wa kiroho wa huduma na kusaidiana na serikali na washilika wengine wa maendeleo katika elimu na shighuli za maendeleo kuwezesha tabia sahii za maadili na uaminifu wa watu.
- Kuandika na kusambaza maandiko ya Kikristo na vipeperushi vya kuwezesha mawasiliano kwa ajili ya mafundisho kwa wachungaji , kanisa na jamii.
- Kufanya miradi maalumu kama vile miraji ya maji safi, program za elimy ya wachungaji, Maabara za matibabu n.k..
- Kusimamia na kutengeneza vyanzo muhimu ili kufikia dira iliyotajwa hapo juu kwa kushirikiana na mashirika, makanisa na watu binafsi.